# USAWIRI WA MWANAMKE KATIKA NYIMBO ZA SIFO ZA WAKAMBA

NA

KIMONDIU DORCAS KASIVA

C50-7355-2016

TASNIFU HII IMEWASILISHWA KWA AJILI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI WA KISWAHILI KATIKA IDARA YA ISIMU NA LUGHA CHUO KIKUU CHA MACHAKOS

OKTOBA, 2019

**UNGAMO**

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe wala halijawasiliswa kwa utahini wa shahada ya uzamili katika chuo chochote kingine.

| | |
|---|---|
| Sahihi……………………………………… | ……………………………… |
| Kimondiu Dorcas Kasiva | Tarehe |
| C50-7355-2016 | |

IDHINI YA WASIMAMIZI

Tasnifu hii limewasilishwa kwa utahini wa shahada ya uzamili kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Machakos.

| | |
|---|---|
| Sahihi……………………………………… | ……………………………… |
| Dkt. Makoti V. Saidi | Tarehe |
| Idara ya isimu na lugha | |
| Chuo Kikuu cha Machakos | |

| | |
|---|---|
| Sahihi……………………………………… | ……………………………… |
| Dkt. Larry Ndivo | Tarehe |
| Idara ya isimu na lugha | |
| Chuo Kikuu cha Machakos | |

## TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa familia yangu: Mume wangu mpendwa, Dkt. Charles N. Muli, watoto wangu wapendwa Danstone Muli, Justice Kimondiu na Carnelian Baraka. Asanteni sana kwa uvumilivu wenu.

SHUKURANI

Awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai, uzima, afya, nguvu na maarifa yaliyoniwezesha kuandika na kuikamilisha kazi hii. Amenijalia fursa ya kuifanya kazi hii na kuyaridhisha matamanio yangu.

Shukurani maalumu ni za wasimamizi wangu, Dkt. Makoti V. Saidi na Dkt. Larry Ndivo ambao walinifaa sana kwa ushauri wao, uelekezi na zaidi ya yote, uvumilivu wao. Wamenitia moyo hasa, kwa kuwepo nilipowahitaji na kunihimiza nilipolemewa.

Kadhalika, napenda kuwashukuru wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Machakos, hasa wahadhiri wa idara ya Isimu na Lugha kwa kunipa taaluma iliyoniwezesha kukamilisha kazi yangu ya uzamili. Pia ninawashukuru wasomi wenzangu kwa ushirikiano wao katika masuala ya kiusomi na ya kijamii. Kwa kweli, wamekuwa marafiki wa dhati kwa kunipa moyo katika muda wote wa masomo tulipokuwa pamoja. Hawa ni Juliana, Muia, Angela miongoni mwa wengine.

Shukurani za pekee kwa familia yangu. Namshukuru mume wangu, Dkt. Muli, kwa kuwa mhimili mkuu katika maisha yangu na halikadhalika, masomo yangu. Pia nawashukuru wanangu, Muli, Kimondiu na Baraka kwa kunivumilia na kuniunga mkono katika masomo yangu. Ufanisi huu pia ni zao la wazazi wangu, marehemu Stephen Kimondiu na Beth Mwikali. Baba, Mungu akujalie pumziko la milele. Mama nakuombea daima. Nawashukuru pia wakwe zangu, Jonathan na Joyce kwa kunihimili, nia njema na sala zao.

## YALIYOMO

UNGAMO ..... i

SHUKURANI ..... iii

YALIYOMO ..... iv

IKISIRI ..... viii

ABSTRACT ..... ix

ISTILAHI ZILIZOTUMIKA ..... x

SURA YA KWANZA ..... 1

UTANGULIZI ..... 1

1.1 SUALA LA MADA ..... 1

1.1.1Historia ya Jamii ya Wakamba na Mifumo yao ya Kijamii ..... 1

1.1.2 Mpangilio wa Jamii ya Wakamba ..... 3

1.1.3 Mahusiano ya Kiuana ..... 5

1.1.4 Dini ..... 7

1.1.5 Mfumo wa Kiuchumi ..... 9

1.2 SUALA LA UTAFITI ..... 14

1.3 MADHUMUNI YA UTAFITI ..... 15

1.4 MASWALI YA UTAFITI ..... 15

1.5 SABABU ZA KUTEUA MADA ..... 16

1.6 UPEO WA UTAFITI ..... 17

1.7 MISINGI YA NADHARIA ..... 17

1.7.1 Nadharia ya Ufeministi ..... 18

1.7.1.1 Mihimili ya Nadharia ya Ufeministi ..... 20

1.7.2 Ufeministi wa Kiafrika ..... 22

1.8 HITIMISHO ... 24

SURA YA PILI ... 25

YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA YA UTAFITI ... 25

2.1 UTANGULIZI ... 25

2.2 MAANDISHI KUHUSU UTANZU WA NYIMBO ... 25

2.2.1 Maana ya Nyimbo ... 25

2.2.2 Nyimbo za Sifo ... 26

2.3 MASUALA KUHUSU WANAWAKE ... 32

2.4 HITIMISHO ... 37

SURA YA TATU ... 38

MBINU ZA UTAFITI ... 38

3.1 UTANGULIZI ... 38

3.2 MUUNDO WA UTAFITI ... 38

3.3 ENEO LA UTAFITI ... 38

3.4 WALENGWA WA UTAFITI ... 39

3.5 MBINU ZA USAMPULISHAJI NA SAMPULI ... 39

3.6 VIFAA VYA UTAFITI ... 40

3.7 UKUBALIFU NA UTEGEMEO WA VIFAA VYA UTAFITI ... 40

3.7.1 Kalamu na Karatasi ... 40

3.7.2 Rununu ... 41

3.7.3 Kipakatalishi na Wavuti /Tovuti ... 41

3.8 MBINU ZA KUKUSANYA DATA ... 41

3.9 MAADILI YA UTAFITI ... 42

3.10 HITIMISHO ... 42

SURA YA NNE ... 43

UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA ........ 43

4.1 UTANGULIZI ........ 43

4.2 KUHUSU WATUNZI ........ 44

4.3 USAWIRI WA MWANAMKE ........ 45

4.4 USAWIRI CHANYA WA MWANAMKE ........ 46

4.4.1 Mwanamke Kama Anayewajibika ........ 46

4.4.2 Mwanamke Kama Mchumi ........ 48

4.4.3 Mwanamke Kama Mshauri Mwema ........ 49

4.4.4 Mwanamke Kama Mkombozi ........ 51

4.4.5 Mwanamke Kama Mlezi wa Familia ........ 54

4.4.6 Mwanamke Kama Mwenye Mapenzi ya Dhati ........ 61

4.5 USAWIRI HASI WA MWANAMKE ........ 66

4.5.1 Mwanamke Kama Mshirikina ........ 66

4.5.2 Mwanamke Kama Asherati ........ 69

4.5.3 Mwanamke Kama Mwenye Tamaa ........ 75

4.5.4 Mwanamke Kama Mgomvi ........ 79

4.5.5 Mwanamke Kama Mtu wa Mipango ya Hadaa ........ 81

4.6 MAUDHUI KATIKA NYIMBO ZA SIFO ZA WAKAMBA YANAYOAKISI HALI HALISI YA MWANAMKE KATIKA JAMII YA WAKAMBA ........ 86

4.6.1 Elimu ........ 87

4.6.2 Ndoa ........ 92

4.6.3 Uchumi ........ 103

4.6.3.1 Mwanamke Mkamba Katika Biashara ........ 103

4.6.4 Ukombozi wa Mwanamke Katika Utamaduni ........ 107

4.6.5 Uongozi ........ 112

SURA YA TANO ..... 117
HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ..... 117
5.1 UTANGULIZI ..... 117
5.2 HITIMISHO ..... 117
5.3 MAPENDEKEZO YA UTAFITI ..... 121
5.4 MCHANGO WA UTAFITI ..... 122
MAREJELEO ..... 123
KIAMBATISHO I ..... i
KIAMBATISHO II: ..... iii
KIAMBATISHO III ..... v
KIAMBATISHO IV ..... vi
KIAMATISHO V ..... viii
KIAMBATISHO VI ..... vii
KIAMBATISHO VII ..... viii
KIAMBATISHO VIII ..... ix
KIAMBATISHO IX ..... x
KIAMBATISHO X ..... xii
KIAMBATISHO XI ..... xiii
KIAMBATISHO XII ..... xv
KIAMBATISHO XIII ..... xvi

## IKISIRI

Utafiti huu ulihusu usawiri wa mwanamke katika nyimbo za sifo za jamii ya Wakamba. Ulikusudia kuchunguza iwapo mwanamke anadunishwa katika nyimbo hizi, anadunishwa vipi na iwapo anatetewa katika jamii dhidi ya imani dunishi za mfumo-dume. Duniani mwanamke hudharauliwa na kudunishwa kwa sababu ya jinsia yake. Imani hii dunishi imo katika itikadi na tamaduni zinazohimiliwa na mfumo-dume unaompa thamani kubwa mwanamume huku ukimdhalilisha mwanamke. Imani hii dunishi ni pamoja na kuozwa mapema, kuonewa kwa wanawake tasa, kunyimwa nyenzo za kujiendeleza miongoni mwa nyingine. Kwa hivyo, utafiti huu ulichunguza usawiri wa mwanamke katika nyimbo teule kumi ambazo ni: *Ngungu na muoi* (Tasa na mchawi) wa Kakai Kilonzo, *Nyinyia wa Ndetei* (Mama wa Ndetei) wa Kijana Mumo, *Kavola Kamengele* (Polepole Kamengele) wa Ancent Munyambu, *Nyinyia Wa Syana* (Mama Watoto) wa Dickson Mulwa, *Mother* (Mama) na *Kana Nzula* (Mpenzi Nzula) za Bosco Mulwa, *Aka* (Wanawake) wa Justus Myello, *Aka ma town* (Wanawake wa mjini) wa Danny Mutuku, *Aka ni ma mithemba* (Aina mbalimbali za wanawake) wa Wanginga *na Syoka mami* (Rudi mama) wa John Muasa. Utafiti ulihakiki nafasi ya mwanamke katika jamii na jinsi anavyosawiriwa katika nyimbo hizi. Tulitumia nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ilioasisiwa na Filomena Steady. Nadharia hii ilitokana na ufeministi wenyewe ili kuhakiki masuala ya ufeministi katika jamii yenye utamaduni wa Kiafrika. Madai ya nadharia hii ni kutambua uwezo wa mwanamke, ukombozi wa wanawake na mwito wa kuwapa wanawake nafasi sawa na wanaume katika nyanja za kijamii, kisiasa, kielimu, kiuchumi na kidini katika muktadha wa jamii inayotawaliwa na ubabedume. Utafiti huu ulihusisha ukusanyaji wa kimakusudi wa sampuli kutoka maduka ya kuuza kanda za video mjini Machakos. Sampuli hii ilijumuisha nyimbo kumi (10) za watunzi tisa (9) wa kiume pekee ili kuchunguza mchango wao katika suala hili la ukombozi wa mwanamke. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa kutumia uchanganuzi elezi na takwimu elezi. Utafiti ulibaini kuwa watunzi wa nyimbo hizi za sifo za Wakamba wamemsawiri mwanamke kwa njia zilizo chanya japo kuna wale waliomsawiri kwa njia hasi. Matarajio yetu ni kuwa utafiti huu utasaidia jamii kubadilisha maoni yao na inavyodhaniwa kuhusu nafasi ya mwanamke katika jamii. Pia utachangia katika taaluma ya fasihi simulizi na fasihi simulizi ya jamii ya Wakamba. Walimu na wanafunzi wa vyuo vikuu na shule za upili watafaidika na utafiti huu.

**ABSTRACT**

This research investigated how a woman is portrayed in these retrogressive beliefs within the patriarchal systems through selected Akamba praise songs. Worldwide a woman is demeaned and discriminated against because of her gender. These negative beliefs are to be found within the ideologies and culture that are supported by patriarchal systems and which place high value on man while attaching low value on woman. The demeaning and discriminative beliefs include early or forced marriages, discrimination against barenness, denied access to means which can result into future self support like education and so on. This research analysed the position of a woman in the Akamba society and how she is portrayed as it emerges in the following songs: *Ngungu na muoi* (The barren woman and the one who is witch) by Kakai Kilonzo*, Nyinyia wa Ndetei* (Mother to Ndetei) by Kijana Mumo*, Kavola Kamengele* (Slowly Kamengele) by Ancent Munyambu, *Nyinya wa Syana* (Mother of our children) by Dickson Mulwa, Mother and *Kana Nzula* (Nzula Baby) by Bosco Mulwa, *Aka* (women) by Justus Myelo, *Aka ni ma mithemba* (Women are of different calibers) by Wanginga, *Aka ma Town* (Town women) by Danny Mutuku and *Syoka Mami* (Come back mother) by John Muasa. This work examined and evaluated how various themes in these songs have demeaned and defended a woman against negative beliefs. In analyzing these songs we were guided by the theory of African Feminism. African Feminism came about due to the claims that western Feminism did not take into account the particular issues black women face especially gender relations. Purposive sampling was used to select ten songs from music stores in Machakos Town. Descriptive analysis and Descriptive statistics was employed to analyse the collected data. Reseach has shown that some of the Kamba artists have praised women positively through their songs although there are others who have portrayed them negatively. We hope that this research will deconstruct these negative beliefs and it will be of a great help to the entire society to have a positive perspective on the position, contribution as well as the roles of a woman in the society. This research will again, contribute in enriching oral literature of Kamba community in general and teachers as well as students of Kiswahili will benefit immensely.

## ISTILAHI ZILIZOTUMIKA

**Chanya**: Mtazamo mwema wenye kuleta matumaini.

**Hasi**: Mtazamo mbaya usio na matumaini.

**Itikadi**: Ni mwelekeo wa kimawazo unaodhibiti jinsi kikundi cha jamii fulani kinavyoukabili, kuufasiri na kuuelewa ulimwengu wao.

**Jinsia**: Ni masuala yanayoambatana na mambo yanayohusu mwanamume au mwanamke.

**Mfumo-dume**: Mchakato wa kijamii unaompendelea mwanamume na kumdunisha mwanamke.

**Santuri**: Chombo chenye umbo la sanduku cha kuchezea muziki wa sahani za santuri.

**Sifo**: Ni tungo za kusifu ambazo hutoa sifa nzuri au mbaya za mtu kutokana na matendo yake.

**Ubabedume**: Ni mfumo wa kijamii ambao humtukuza mwanamume na kumdhalilisha mwanamke.

# SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI

Katika sura hii, ilishughulikia masuala ya kimsingi yanayofaa kuzingatiwa. Masuala haya ni pamoja na usuli, suala la utafiti, malengo na maswali yaliyoongoza utafiti pamoja na sababu za kuchagua mada. Aidha, sura hii ilishughulikia upeo wa utafiti na misingi ya kinadharia iliyoongoza utafiti huu.

## 1.1 SUALA LA MADA

Wakamba ni wanajamii wanaoishi mkoa wa Mashariki wa nchi ya Kenya (Mathooko, 2014). Mahali wanapoishi panaitwa Ukambani (Ndeti, 1972). Wakamba wako katika kundi la Wabantu liitwalo Wabantu wa Mashariki, ambalo kulingana na wanahistoria walipitia Kaskazini kutoka Shungwaya. Jamii ya Wakamba hupatikana katika kaunti za Machakos, Kitui na Makueni. Wengine wamo katika eneo la Mwea kaunti ya Embu, Shimba Hills, Kinango na Mariakani kaunti ya Kwale na pia sehemu za Taita Taveta na Mombasa (Kitavi, 1992). Wakamba wamepakana na Wagikuyu, Wambeere, Waembu na Watharaka upande wa Magharibi.

### 1.1.1Historia ya Jamii ya Wakamba na Mifumo yao ya Kijamii

Senkoro (1987), anaeleza kuwa historia huipa sanaa uhai na mwelekeo. Ili kuelewa fasihi ya jamii yoyote ile ni muhimu kufahamu historia yake. Maoni ya Senkoro yalichochea msukumo wa kuchunguza historia ya jamii ya Wakamba ili kuelewa nyimbo za sifo pamoja na mabadiliko yanayozikumba kwa mujibu wa mabadiliko ya kijamii.

Wakamba ni jamii moja katika makundi kadhaa ya Wabantu (King'ei, 1982). Kundi la Bantu ndilo kubwa nchini Kenya na lililo na makabila mengi yaliyo na uhusiano wa karibu. Wabantu wa Kenya wako katika makundi mawili. Kuna wale wanaoishi Magharibi mwa Kenya na wale

wanaopatikana Mashariki mwa Kenya. Wabantu wanaopatikana Magharibi mwa Kenya ni pamoja na Abakuria, Abaluyia, Abagusii na Abasuba. Makundi ya Wabantu wanaopatikana Mashariki mwa Kenya, yamegawanywa katika makundi mawili, yaani Wabantu wa Kati na Wabantu wa Pwani.

Wakamba walikuwa wakifuga mifugo na pia walikuwa wawindaji. Walikuwa wakitumia mitego kuwatega wanyama wadogo ili kupata chakula. Kufikia mwishoni mwa karne ya kumi na sita, Wakamba walianza kuhama kutoka sehemu zilizokuwa karibu na mlima Kilimanjaro kutokana na uvamizi wa *Akavi* (Wamaasai) (Nurse &Spear, 198). Sehemu hii ilikuwa jangwa. Haikuwa na miti ya kuwasetiri kutoka kwa Wamaasai wakati wa vita vya kuviziana. Kwa hivyo, wakahamia sehemu za Kyulu Kaunti ya Makueni.

Sehemu waliyohamia ya Kyulu ilikuwa na mawe makubwa na haikuwa na maji ya kutosha kwa mifugo wao (Ndeti, 1972). Kufikia karne ya kumi na saba, Wakamba wakahama sehemu ya Kyulu hadi Kibwezi ambapo pia walikumbana na ukavu kutokana na ukosefu wa mvua. Kufikia mwishoni mwa karne ya kumi na saba, Wakamba wakahamia sehemu iliyoko karibu na Nzaui. Kwa mujibu wa Andrew & Salvadori (1980), sehemu ya Nzaui ilikuwa kavu na yenye mawe makubwa. Wakamba wasingeweza kulisha mifugo yao kutokana na ukosefu wa lishe na maji.

Kulingana na Ndeti (1972) na Nzioki (1982), ongezeko la jamii hii na matatizo mengine kama uvamizi wa jamii ya Wamasai, lilisababisha Wakamba kuhamia sehemu za kaunti ya Machakos na wengine Kitui walipohama Nzaui. Kufikia mwanzoni mwa karne ya kumi na nane, wakahamia Milima ya Mbooni wakitafuta lishe ya mifugo yao. Milima ya Mbooni (yenye kumaanisha eneo lenye nyati) ilikuwa na mchanga wenye rutuba kwa hivyo, Wakamba wakaanza kilimo pamoja na ufugaji (Wambua 2013). Vile vile, Wakamba walikuwa wakiwinda

nyati ambao walikuwa wengi sehemu hizo. Baada ya kuishi Mbooni kwa muda karibu karne moja, baadhi yao walihamia sehemu za Wamunyu, Iveti na Kitui kutokana na ongezeko la watu (Ndeti 1972, Musyimi, 2011).

Katika maeneo haya, Wakamba wakaanza kufanya biashara na watu kutoka pwani, Wagikuyu, Watharaka, Wambeere na Wataita. Walikuwa wakibadilishana bidhaa zao kama mishale iliyokuwa na sumu, vibuyu vya ugoro miongoni mwa bidhaa nyingine. Wakamba walipata wimbi, mtama, maharangwe na mahindi kutoka katika jamii nyingine kama vile Wagikuyu na Waembu (King'ei, 1982).

Kwa sasa, Wakamba wanaishi katika kaunti za Kitui, Machakos na Makueni nchini Kenya. Eneo hili lote wanamoishi Wakamba hujulikana kama Ukambani. Hata hivyo, Kieti na Coughlin (1990) wanasema kwamba, kuna Wakamba ambao wanapatikana katika sehemu nyingine kama Mwea katika kaunti ya Embu, sehemu za pwani hasa Shimba hills, Kinango na Mariakani katika kaunti ya Kwale, sehemu za Taita Taveta na Mombasa.

### 1.1.2 Mpangilio wa Jamii ya Wakamba

Katika jamii ya Wakamba, ukoo ulikuwa ni taasisi muhimu. Wanajamii waliokuwa katika koo mbalimbali walitegemeana kwa hali zote za maisha. Ukoo ulihusu watu ambao walikuwa wa nasaba moja kutoka kwa mzazi mmoja wa jadi (Kimilu, 1962). Wanaukoo fulani walikuwa na uhusiano wa karibu kiasi kwamba, waliitana kaka na dada. Koo ishirini na mbili zilikuwa zimebainika vyema katika jamii hii. Mfano: Atangwa, Aanziu, Auani, Atwii, Aombe, Ambua, Amuunda, Akitutu, Aiini, Akitondo, Aumoni, Amwitu, Ethanga, Ekuua, Euani, Anzauni, Aoini, Amutei, Amiwani, Amwei, Akanga na Amuuti (Wambua, 2013). Koo za Wakamba zilihakikisha mshikamano wa kijamii na kuwapa Wakamba nafasi ya kujitambulisha kama jamii. Ni katika

mfumo huu ambao yeyote katika jamii aliegemea wakati wa tatizo lolote lile. Mfumo wa kiukoo uliwapa wanajamii mshikamano ambao uliwawezesha kukabiliana na baadhi ya matatizo kama jamii moja (Kimilu, 1962).

Nyimbo zilitekeleza majukumu muhimu katika utamaduni wa Wakamba. Majukumu haya yalikuwa ni kuabudu, kufariji, kukosoa, kuelekeza na kuhifadhi historia. Wanajamii walifanya kazi pamoja kwa ushirikiano. Walisaidiana kulingana na koo. Katika jamii ya Wakamba, ukoo ulikuwa ni taasisi muhimu.

Jamii ya Wakamba ilikuwa na mafunzo ya kijamii. Mafunzo haya yalipitishwa kupitia fasihi simulizi yao kama vile ngano, vitendawili, methali pamoja na nyimbo miongoni mwa fasihi simulizi pana ya jamii ya Wakamba. Umuhimu wa fasihi ni kupitisha mafunzo ya kijamii kulingana na Njogu na Chimera (1999) na Wamitila (2003) ambao wanashikilia kuwa, fasihi ni zao la jamii na hutungwa ili kuelimisha, kuonya, kukosoa na kuburudisha jamii miongoni mwa dhima nyingine katika jamii. Fasihi simulizi ya Wakamba ilichukua nafasi muhimu katika mafunzo ya kijamii ambayo yalipitishwa kutoka kizazi hadi kingine kwa njia ya mdomo (Kimilu, 1962; Mbiti, 1969).

Jamii ya Wakamba ilihusika katika kumwandaa kila mwanajamii kulingana na mfumo wa maisha na maadili ya kijamii. Kwa mujibu wa Kimilu (1962), kupotoka kwa wanajamii hasa kuasi mila na tamaduni kulitokana na kutopata mafunzo kuhusu maadili ya jamii ya Wakamba. Kutopata mafunzo ya kimaadili kulisababisha kubadili dini kutoka dini ya Mwafrika na kupapia dini ya kigeni kama dini ya Kikristo. Kutokana na kupapia huku, wengi wa Wakamba wakakengeuka na kuwa *Asomba* (Wakamba wasomi wanaotomia lugha ya Kiingereza).

Uongozi katika jamii ya Wakamba ulilenga misingi ya ukoo. Wazee *(atumia*) ndio waliotwikwa jukumu la kuiongoza jamii na kushughulukia mambo ya kidini kama vile matambiko ya kijamii na kafara miongoni mwa mengine (Nzioki, 1982). Kulingana na King'ei (1982), umri, ndoa na uadilifu ndivyo vigezo vilivyotumika kuwateua viongozi. King'ei anasema kuwa *atumia ma kivalo* walikuwa wazee wenye umri wa kuanzia miaka hamsini na ambao walikuwa na tajriba kuhusu maisha ya wanajamii. Waliongoza sherehe za kidini kama kutoa kafara pamoja na uongozi wa sherehe za tohara na mazishi katika jamii. Katika jamii ya Wakamba ni wazi kuwa shughuli muhimu za kijamii hazikumhusisha mwanamke. Jambo ambalo linaonyesha mwanamke kupewa nafasi ya pili.

Baraza la juu kabisa la uongozi lilikuwa kundi la *atumia ma kisuka*. Hawa ni wazee waliokuwa na umri wa kuanzia miaka sitini. Walikuwa wamestaafu katika shughuli nyingi za kijamii. Waliachiwa hasa shughuli za kuongoza sherehe za kidini hususan utoaji wa kafara na sherehe za utakasaji. Aidha, waliongoza sherehe za ulaji wa viapo maarufu kama *ithitu* katika jamii hii. Wazee hawa vile vile waliamua kesi nyeti kama mauaji na kesi za uchawi. Mwanamke hakuhusika katika mambo haya, hili linaonyesha jinsi mwanamke alivyokuwa hatambuliki tangu jadi.

### 1.1.3 Mahusiano ya Kiuana

Jamii ya Wakamba ilikuwa, na hata sasa ni ya kibabedume. Mwanamume ndiye aliyekuwa kiongozi wa familia na mmiliki mali. Urithi ulikuwa ni kwa mwanaume pekee. Hata hivyo, kutokana na utetezi mwingi unaoendelea kuhusu mtoto wa kike, wanaume wameanza kuona umuhimu wa kuwarithisha mabinti zao. Wanawake katika jamii ya Wakamba wana hadhi duni. Hali hii inaendelea kubadilika kadri maendeleo katika jamii yanavyozidi kupatikana.

Mwanamke alipaswa kumnyenyekea mumewe na kuwa na heshima kwa wanaume wote kwa jumla. Mwanamke akikosewa na mume wake, imani za jamii hazikumkubali kukabiliana na mumewe moja kwa moja. Alipaswa kutumia mtu ambaye anaweza kuwa mwanamume marika na mumewe kusuluhisha tofauti hiyo (Naomi, 2016).

Ndoa ilimfanya mwanamke kuwa mali ya mumewe. Alipolipiwa mahari, kwa mujibu wa jamii hii, mwanamke sasa alikuwa mali ya mume wake. Jukumu la kimsingi kabisa mke akiolewa, ni kupata watoto. Anatarajiwa kupata watoto na hasa wa kiume ili kuendeleza kizazi cha mwanamume na ukoo mzima. Mwanamke ambaye alishindwa kupata watoto alidharauliwa na wanajamii kwa kuitwa *nthata* (tasa). Mumewe aliruhusiwa kuoa tena ili kupata mtoto wa kiume. Mke huyu tasa alinyimwa haki za kimapenzi na mumewe na hakuwa na ruhusa ya kurudi kwao au kuolewa tena. Alikaa kwa mume wake akihudumu kama kijakazi (Nzioki, 1982).

Jamii ya Wakamba leo imebadilika pakubwa. Mabadiliko haya yamesababishwa na mfumo wa uongozi, msisimko wa teknolojia mpya ya mawasiliano, elimu ya Kimagharibi, kukua kwa miji na viwanda, maendeleo ya kiuchumi, dini miongoni mwa mifumo mingine (Kavyu, 1980; Kieti, 1999; Kilauni, 2007; Wathome, 2009).

Wakamba wengi kama ilivyo katika jamii nyingi za Kiafrika wameathiriwa kwa kiasi fulani na mabadiliko haya na pia fasihi simulizi yao imeathiriwa. Nyimbo na ngoma za kitamaduni zimeathiriwa na mabadiliko haya na hata nyingine kusahaulika (Kilauni, 2007; Wathome, 2009). Kubadilika huku kunatokana na sababu kwamba, nyimbo ni miongoni mwa vipengele vya utamaduni wa jamii ambao kila siku huendelea kuzaliwa, kuathiriwa na kubadilika kadri maisha yanavyobadilika.

### 1.1.4 Dini

Jamii ya Wakamba ilikuwa na dini yao kama Waafrika wengine. Ilikuwa na imani katika miungu kabla ya majio ya wakoloni. Wakamba walitoa kafara katika maeneo maalumu yaliojulikana kama *mathembo* (Wambua, 2013). Walishiriki katika dini yao kufuatana na mafunzo waliyopata kutoka kwa mababu zao. Jamii ya Wakamba ililinda na kudumisha heshima zote za dini na utamaduni wao kwa kuweka miiko na ushirikina. Watoto walifunzwa dini yao wakiwa wadogo na mafunzo yaliendelea hadi uzeeni. Kila mwanajamii alishirikishwa katika sherehe tofauti za kidini ambazo zilikuwa sehemu ya maisha yao (Kieti na Coughlin, 1990).

Wakamba waliamini kuwepo kwa miungu ambao walikuwa wakiabudu. Miungu hao walipewa majina mbalimbali. Baadhi ya majina haya yalielezea utendakazi wao hasa; *Mulungu* (Mungu), *Mumbi* (muumbaji), *Mwatuan*gi (anayeumba vidole vya binadamu) na *Ngai* (anayegawa) (Wambua, 2013).

Katika jamii ya Wakamba, imani kwamba Mungu mkuu yuko kila mahali ipo kama ilivyokuwa tangu enzi za mababu zao. Matukio yote ya ulimwengu yaliaminika kuwa na uhusiano na Mungu. Iliaminika kuwa, tukio lolote baya lilitokana na adhabu ya Mungu kwa binadamu kutokana na matendo yake maovu.

Pepo wabaya nao waliaminika kuishi katika sehemu fiche kama pangoni, misituni na mahame (Kavyu 1980). Wanajamii hawa waliogopa sana pepo wabaya na athari zake. Sehemu hizi zilikuwa zikiogopwa na watu sana hasa nyakati za usiku. Pepo wazuri waliaminika kuishi katika *ithembo* (eneo la kutolea kafara). Kafara ilitolewa chini ya mti mkubwa ujulikanao kama *kiumo* (mgumo). Pepo wazuri waliaminika kuishi katika mti huu na ilikuwa mwiko kuukata (Mbiti 1969). Wazee walioheshimika na *awe* (waganga) walitwikwa jukumu la kuunganisha binadamu

na Mungu. Suala hili linaonyesha kuwa, mwanamume ndiye aliyepewa majukumu muhimu katika jamii ya Wakamba. Mchango wa mwanamke haukutambulika katika kuunganisha watu na Mungu. Huku ni kudhalilishwa kwa mwanamke.

Wakamba waliamini na hata sasa, wanaamini kuwa watu waliokufa bado wana mchango katika matukio ya watu walio hai (Somba 2000). Wanaheshimiwa, kusujudiwa na kuogopwa. Haya yalidhihirika wazi kutokana na sherehe za mazishi alizofanyiwa mtu akiaga dunia. Inaaminika kuwa hata mtu akifa hasa wazazi, wao huendelea kuishi na aila yao na kuwakinga kutokana na mikosi. Utoaji wa kafara ulikuwa mojawapo ya njia za kumshukuru na kumtuliza Mungu. Wanajamii walitoa kafara ili kuomba msamaha kwa Mungu (Nzioki, 1982).

Kulingana na Nzioki (1982), mbuzi au kondoo wa rangi moja bila madoadoa yoyote ndiye aliyetolewa kafara kwa sababu alidhihirisha usafi. Sehemu mbaya za kondoo huyu zilitengewa pepo wabaya. Mababu walipewa kiwango fulani cha chakula au kinywaji kabla ya mwanajamii yeyote kula au kunywa. Hii ilikuwa ishara ya kuwatambua mababu. Kitendo hiki kilijulikana kama *kuthemba.* Mtu akila ua kunywa bila kuwatambua mababu iliaminika kuwa angenyongwa na chakula kile. Babu ni mzazi wa kiume ambaye ni mzaa baba au mama. Kitendo cha kuwatambua mababu kinaonyesha kuwa, ni wale tu wa kiume. Wale wa kike hawakutambuliwa. Jambo hili linamweka mwanamke katika daraja ya pili baada ya mwanamume.

Ingawa Wakamba wanaamini kuwepo kwa Mungu na wanamwabudu, kuenea kwa dini ya Kikristo na Kiislamu kumeathiri pakubwa dini asilia ya Wakamba. Wakristo na Waislamu waliozieneza dini hizi za kigeni waliwatisha Wakamba kwa kuwaambia kuwa wataenda motoni kwa kufuata mila, desturi, utamaduni na itikadi zao. Mafunzo haya yalisababisha kupotea kwa baadhi ya mila za jamii ya Wakamba.

### 1.1.5 Mfumo wa Kiuchumi

Kwa mujibu wa Chacha (1997), kuna uhusiano mkubwa kati ya uchumi na fasihi. Kulingana naye, hali ya uchumi huathiri sanaa iliopo. Mfumo wa uzalishaji mali ukibadilika nayo fasihi hubadilika katika harakati za kudhihirisha mabadiliko hayo. Kwa hivyo, hali ya uchumi huelekeza fasihi. Kulingana na Senkoro (1987), chimbuko la sanaa ni mazingira halisi ya jamii. Kabla ya majio ya wakoloni, jamii ya Wakamba ilikuwa ni wawindaji na wakusanyaji matunda na mazao mengine ya mwituni. Walitegemea sana nyama kutoka wanyama wa porini kama vile nguruwemwitu, paa, nyati miongoni mwa wengine.

Kila shughuli ya kijamii ilikuwa na nyimbo maalumu zilizoandamana nayo. Nyimbo hizo na ngoma walizocheza ziliwapunguzia makali ya maisha kwa kuwaburudisha (Nzioki, 1982). Katika jamii ya Wakamba, tajiri (*muthwii)* alikuwa ni yule mwenye ng'ombe wengi, wanawake na watoto wengi (Kieti, 1999). Mwanamke kuwa kama kigezo cha kupima utajiri wa mwanamume kunaonyesha udhalilishaji wa jinsia ya kike. Ng'ombe na mbuzi walithaminiwa sana kwa sababu walitumiwa katika shughuli ya ulipaji mahari. Aidha, wanyama hawa walitumiwa katika utoaji wa kafara ili kutuliza au kushukuru miungu yao (Mbiti, 1969). Vile vile wakati wa sherehe zozote kama vile za tohara, harusi na mazishi, ng'ombe na mbuzi walichinjwa ili wanajamii washerehekee pamoja.

Mbali na ufugaji, Wakamba walishiriki katika shughuli nyingine za kiuchumi kama uchongaji, utengenezaji wa mizinga, utengenezaji wa mapambo wakitumia madini ya aina ya chuma na pia biashara ya uhunzi (Nzioki, 1982). Hadi leo Wakamba wangali wanashiriki katika shughuli hizi kiuchumi na wanatambulika kwa biashara ya uchongaji katika sehemu ya Wamunyu katika Kaunti ya Machakos. Uchongaji na utengenezaji wa vinyago ulishika kasi baada ya vita vya

kwanza vya dunia. Walijifunza uchongaji huu kutoka kwa Wamakonde wa nchi ya Tanganyika (Nzioki, 1982). Uhunzi na uchongaji ilikuwa kazi ya wanaume nao wanawake walifinyanga vyungu na kusuka vikapu *(syondo*). Shughuli hii inaendelea hadi leo katika jamii ya Wakamba (Naomi, 2016).

Kabla ya kuja kwa wakoloni, Wakamba walikuwa wakifanya biashara na jamii za pwani na Waarabu. Walisafiri kutoka Kitui na Machakos hadi pwani. Kivui Mwenda ni miongoni mwa wanaojulikana sana katika jamii ya Wakamba. Aliwaongoza katika biashara hii (Wambua, 2013). Wakamba waliwauzia Waarabu pembe za ndovu*, ivai* (mishale yenye sumu), ngozi za chui, asali, vinyago walivyochonga miongoni mwa bidhaa nyingine (Kavyu, 1980). Waarabu nao waliwauzia nguo, mapambo na nyaya za shaba walizotumia kutengeneza mitego ya wanyama na mapambo (Kimilu, 1962). Wakamba walishiriki biashara na jamii jirani kama vile Wakikuyu, Waembu, Wamasai na Wambeere. Katika biashara hii walibadilishana mazao ya shambani na vifaa vya uchongaji.

Hivi sasa, Wakamba wanategemea kilimo cha mseto kikiwa ndicho uti wa mgongo wa uchumi wao. Vyakula vya kitamaduni kama vile kunde, mbaazi, mtama, mawele, viazitamu bado vinakuzwa. Mahindi na maharagwe ni baadhi ya vyakula ambavyo hutumika sana katika jamii hii. Wakamba wanafuga wanyama kama vile mbuzi, ng’ombe na kuku. Ng’ombe na mbuzi bado wanatumika katika shughuli za ulipaji mahari kama ilivyokuwa katika jamii kabla na baada ya majilio ya wakoloni.

Wakamba kama jamii wana fasihi simulizi yao. Fasihi simulizi ni utanzu muhimu wa fasihi katika jamii kwani utamaduni wa jamii inayohusika hujidhihirisha kupitia utanzu huu (Wamitila, 2003). Wakamba ambao ndio watafitiwa katika uchunguzi huu, hueleza hali ya maisha yao,

utamaduni wao, imani na mila zao kupitia tanzu za fasihi simulizi. Wanaeleza maoni yao na mitazamo yao kupitia tanzu mbalimbali za fasihi simulizi kama vile ngano, methali, vitendawili, misemo, mafumbo, nyimbo miongoni mwa nyingine. Katika jamii ya Wakamba, fasihi simulizi ni hai na huelezea mielekeo na falsafa kuhusu maisha ya watu (Ndeti, 1972). Fasihi simulizi huibuka katika hali halisi ya maisha ya kila siku. Kulingana na Simiyu (2007), nyimbo kama utanzu wa fasihi simulizi huendelea kupata mabadiliko ya kijamii kadri jamii inavyoendelea kubadilika. Anaendelea kueleza kuwa mabadiliko yanayoikumba jamii kwa njia moja au nyingine hujidhihirisha katika fasihi.

*Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004: 463) inaeleza "wimbo" kuwa ni maneno yanayotamkwa kwa sauti ya muziki. Wakamba kama jamii nyingine za Kiafrika, wana nyimbo mbalimbali ambazo huandamana na matendo mbalimbali ya maisha yao. Kila shughuli ya jamii ina nyimbo zinazoandamana nayo. Nyimbo hizi wanapocheza huwapunguzia makali ya maisha kwa kuwaburudisha (Nzioki, 1982). Nyimbo hizi zilikuwa na maudhui yaliyoegemea mambo kama vile ushindi wa vita, kuzaliwa, kupashwa tohara, harusi, maombolezi, kulima, kulisha mifugo, kulea mwana, kupumzika, kuliwaza na takribani shughuli zote za binadamu (King'ei,1982). Wimbo ni fani muhimu katika jamii ya Wakamba kwa kuwa inatumika katika shughuli nyingi za kijamii. Shughuli hizi ni kama vile kazi, michezo, mapumziko na sherehe mbalimbali kama vile kuzaliwa kwa mtoto, kupewa jina, jando na harusi.

Nyimbo hutekeleza majukumu mbalimbali katika jamii ya Wakamba, kama vile kushauri, kuliwaza, kusifu, kusuta, kuonya miongoni mwa mengine. Wakamba vile vile, wana nyimbo za sifo ambazo hutumika kutoa sifa za mtu ziwe nzuri au mbaya. Wamitila (2004:128), anaeleza sifo kuwa ni tungo za kusifu. Sifo huweza kumsifu mtu kutokana na matendo yake ya kishujaa

au ya kijasiri. Wamitila (aliyetajwa) anaendelea kusema kuwa, sio sifo zote ambazo hutoa sifa nzuri au chanya, zipo nyingine ambazo hukashifu au kutoa sifa kinyume, kuumbua, kunyambua, kukosoa na kadhalika. Nyimbo hizi hunuia kuwaweka wanajamii katika hali inayokubalika na jamii husika. Katika tasnifu hii, nilichukulia nyimbo za sifo kuwa nyimbo zozote zinazoeleza sifa ya mtu chanya au hasi.

Mfano mzuri wa wimbo wa sifo katika jamii ya Wakamba ni ule aliotungiwa Kisoi Munyao aliyeukwea Mlima Kenya siku ya sherehe ya kwanza ya Uhuru ili kuipandisha bendera ya taifa huru la Kenya mwaka wa 1963 ulioitwa *Kisoi wa Munyao alisa kiima kitalisika* (Kisoi Munyao kaukwea mlima usiokweeka). Mfano wa wimbo wenye sifa hasi ni ule wa *Mutindi* ulioimbwa na John Mutua. Msanii huyu anatoa sifa za Mutindi kupitia ubeti huu:

| | |
|---|---|
| *Mutindi ni wa Kaseve,* | Mutindi ni msichana kutoka Kaseve, |
| *Mwiiti mukola wi metho mailye ta mwaki,* | Ni mkora, macho yake yanafanana na moto, |
| *Matuku ikumi na eli Ndisemba* | Tarehe mbili mwezi wa Disemba |
| *Ambumbaniisye mikola navuwa muno.* | Alipanga njama na wakora wakanichapa nusura waniuwe |

Jamii ya Wakamba hii leo imebadilika pakubwa. Mabadiliko haya yamesababishwa na mfumo wa uongozi, msisimko wa teknolojia mpya ya mawasiliano, elimu ya kizungu, kukua kwa miji na viwanda, maendeleo ya nyanja mbalimbali za kiuchumi, dini miongoni mwa mabadiliko mengine (Kilauni, 2007). Wakamba wengi kama ilivyo katika jamii nyingi za Kiafrika wamehama mashambani na kwenda kuishi mijini. Mabadiliko haya yameathiri kwa kiwango fulani fasihi simulizi yao. Nyimbo katika jamii ya Wakamba pia zimeathiriwa na mabadiliko haya kwa sababu nyimbo za kitamaduni nyingine zimesahaulika (Kilauni, 2009). Nyimbo za sifo za Wakamba zilizotungwa na watunzi hawa zinaakisi mabadiliko haya.

### 1.1.6 Utetezi wa Mwanamke

Ndani ya mapito ya historia mwanamke amekuwa akipigania kuboresha nafasi yake katika jamii. Vita hivi vimeendeshwa katika majukwaa mengi kwa kutumia njia nyingi. Pamekuwepo na mashirika mbalimbali ya kimataifa ambayo yamejitokeza kutetea haki za kimsingi za mwanamke. Mfano, mnamo mwaka wa 1995, kulikuwa na kongamano la nne la Umoja wa Mataifa juu ya wanawake mjini Beijing Uchina ambalo lilijadili haki za wanawake. Uzito wa kumlinda mtoto wa kike unadhihirishwa na kutengwa kwa siku maalum duniani kama siku ya mtoto wa kike, ambayo ni tarehe kumi na moja mwezi wa kumi kila mwaka. Vile vile, kuna siku maalum ya kimataifa ya wanawake inayoadhimishwa Machi nane kila mwaka, pia kuna siku ya akina mama inayosherehekewa kila mwezi wa Mei.

Jamii inapitia mabadiliko ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Katika nchi mbalimbali, Kenya ikiwemo, suala la wanawake na uongozi halijapiga hatua kubwa katika jamii nyingi. Katiba ya Kenya 2010, inaamuru thuluthi moja (1/3) ya nafasi zote serikalini kupewa wanawake likiwemo Bunge lakini haijatimizwa. Hii ina maana kuwa nafasi ya mwanamke katika uongozi bado ni finyu. Sababu hii ilitushawishi kujikita katika uchunguzi wetuTulijiuliza je, wanaume wanatambua uwezo wa mwanamke?

*Katiba ya Kenya* 2010, sura ya nne sehemu ya pili, ibara ya ishirini na saba, inaeleza kuwa wanawake na wanaume wana haki sawa zikiwemo usawa wa nafasi katika siasa, uchumi, utamaduni na kijamii. Ijapokuwa katiba ya Kenya ilipitisha haya, bado nafasi ya mwanamke ni finyu katika nyanja mbalimbali kama vile nafasi za uongozi serikalini. Kwa hivyo kupitia sheria pekee huwezi kumtetea mwanamke mpaka pawe na utetezi wa dhati wa mabadiliko ya kifikra katika jamii. Bado mwanya ungali upo katika harakati za kumkomboa mwanamke. Kutokana na sababu hii, utafiti huu ulinuia kudadisi iwapo mwanamke amepewa nafasi chanya au hasi kupitia

kwa nyimbo za sifo za Wakamba zilizotungwa na watunzi wa kiume pekee ili kubaini mchango wa mwanamume katika suala la kumkomboa mwanamke. Watunzi hawa nao ni: Bosco Mulwa, Kakai Kilonzo, Wanginga, Danny Mutuku, John Muasa, Dickson Mulwa, Ancent Munyambu, Kijana Mumo na Justus Myello ambao ni watunzi wa nyimbo za Kikamba ambazo wamemzungumzia mwanamke kama mhusika mkuu. *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004:300) inaeleza kuwa "nafasi" ni palipo patupu na ambapo panaweza kuwekwa kitu. Ufafanuzi huu ukiwekwa katika muktadha wa jamii una maana kwamba kila mmoja ana mahali pake alipotengewa na jamii. Wanawake kama wanajamii, wana nafasi yao katika jamii ambayo wanastahili kutekeleza. Kwa kuteua nyimbo hizi za watunzi hawa, kazi hii ilichunguza jinsi ambavyo mwanamke amesawiriwa na nafasi anayopewa kama ni chanya au ni hasi katika jamii ya Wakamba.

## 1.2 SUALA LA UTAFITI

Utafiti huu ulidhamiria kutathimini usawiri wa mwanamke katika fasihi simulizi ya Wakamba katika kipera cha nyimbo za sifo. Tamaduni nyingi duniani humtweza mwanamke huku zikimkweza mwanamume. Baadhi ya dhuluma anazofanyiwa mwanamke ni pamoja na kuchapwa, kuozwa mapema, kudhulumiwa kutokana na utasa, kunyimwa nafasi ya kujiendeleza kielimu, kunyimwa urithi na kutoshirikishwa katika maamuzi miongoni mwa nyingine.

Utafiti huu ulidhamiria kuhakiki usawiri wa mwanamke katika jamii ya Wakamba iliyotawaliwa na imani dunishi ya kiubabe-dume kupitia nyimbo hizi za sifo. Yego (2013), anasema kuwa kuna majukumu ambayo hata kamwe mwanamke hatakikani kulalamika kwa kuwa ni mojawapo ya hulka zinazomfanya kuitwa mwanamke. Tulichunguza, je wanawake wa jamii ya Wakamba wanapewa majukumu ya hulka au wanakandamizwa kupitia nyimbo za waimbaji wanaume?

Kwa hivyo, lengo letu ni kuchunguza iwapo utetezi huu wa mwanamke umefaulu kumwekea thamani yoyote kupitia nyimbo za sifo zilizotungwa na watunzi wa kiume. Tulichunguza pande zote mbili hasi na chanya. Kuna watunzi wa kazi za fasihi wanaotetea nafasi ya mwanamke. Mfano, Mazrui katika tamthilia ya *Kilio cha Haki* (1981), Said katika riwaya ya *Chozi la Mwanamke* (2009), Kithaka wa Mberia katika tamthilia ya *Natala* (1997) miongoni mwa wengine. Kwa hivyo utafiti huu, unanuia kudhihirisha mwanamke anavyosawiriwa na kutetewa katika nyimbo za sifo za Wakamba zilizotungwa na watunzi wanaume pekee ili kutathmini iwapo wamempa nafasi chanya au hasi.

## 1.3 MADHUMUNI YA UTAFITI

Utafiti huu ulidhamiria:

a) Kuchunguza jinsi ambavyo mwanamke amesawiriwa katika nyimbo za sifo za Wakamba zilizotungwa na watunzi wa kiume.

b) Kuchunguza iwapo usawiri wa mwanamke wa Kikamba unaakisi hali halisi ya maisha ya hivi sasa karne ya 21.

c) Kutathimini ikiwa jamii ya Wakamba imebadilisha mawazo kuhusu usawiri wa mwanamke kama binadamu sawa na mwanamume.

## 1.4 MASWALI YA UTAFITI

(a.) Mwanamke amesawiriwa vipi katika nyimbo za sifo za Wakamba zilizotungwa na watunzi wa kiume?

(b.) Je, usawiri wa mwanamke wa Kikamba katika nyimbo teule unaakisi hali halisi ya maisha katika karne ya 21?

(c.) Je, jamii ya Wakamba imebadili mawazo na kumsawiri mwanamke kama binadamu sawa na mwanamume kupitia maudhui ya nyimbo hizi?

### 1.5 SABABU ZA KUTEUA MADA

Nyimbo za sifo ni kipengele kimojawapo cha fasihi simulizi, kwa hivyo utafiti huu utachangia zaidi katika fasihi simulizi ya Afrika. Matokeo yake yatakuwa kichocheo kwa watafiti ili waendelee kutafitia kipera hiki katika jamii mbalimbali na kubaini nafasi anayopewa mwanamke katika jamii husika. Pia, inaaminika kuwa, matokeo ya utafiti huu yatakuwa hazina kwa wakuza mitalaa, wahadhiri na walimu katika ufunzaji wa fasihi simulizi kwani ni somo ambalo hufunzwa katika viwango vyote vya elimu hapa nchini Kenya.

Sababu nyingine ya kuchagua mada hii ni hamu ya kujaza pengo la kiusomi baada ya kuzitathmini kazi mbalimbali zilizoshughulikia aina tofauti za udunishwaji na udhalilishwaji wa mwanamke hasa katika misingi ya kijinsia. Watetezi wengi wa mwanamke wanaamini kuwa ukombozi wa mwanamke ni muhimu. Ukombozi huu wa mwanamke hautakamilika bila kushirikisha mchango wa mwanaume katika suala hili. Utafiti huu ulikusudia kuliziba pengo hili kupitia nyimbo za sifo kwani hakuna utafiti mwingine uliofanywa kuhusu nyimbo za sifo za jamii ya Wakamba. Tunaamini kuwa waimbaji hawa ni wanajamii wenye ndoto ya kuboresha jamii hivyo kuangazia nguvu na udhaifu wa jamii husika. Utafiti huu utaongoza uhamasishaji wa watunzi wanaume ili wawe kiunzi muhimu katika kuleta ufanisi kwenye harakati za kumkomboa mwanamke na vile vile kumjenga katika jamii ya ki-ubabedume.

## 1.6 UPEO WA UTAFITI

Utafiti huu ulijikita tu katika usawiri wa mwanamke katika nyimbo kumi teule za sifo za Wakamba ambazo ni: *Ngungu na muoi* (Mwanamke tasa na mchawi) wa Kakai Kilonzo, *Mother* (Mama) na *Kana Nzula* (Mpenzi Nzula) za Bosco Mulwa, *Aka* (Wanawake) wa Justus Myello, *Aka ma town* (Wanawake wa mjini) wa Danny Mutuku, *Aka ni ma mithemba* (Aina mbalimbali za wanawake) wa Wanginga, *Nyinyia wa Ndetei* (Mama Ndetei), *Kavola Kamengele* (Polepole Kamengele) wa Ancent Munyambu, *Nyinyia wa Syana* (Mama watoto) wa Dickson Mulwa na *Syoka mami* (Rudi mama) wa John Muasa.

Tulichunguza tu nyimbo hizi zinavyomsawiri mwanamke katika karne hii ya ishirini na moja.Vile vile, tulirejelea kazi nyingine nyingi kama vile tasnifu mbalimbali za wahakiki pamoja na vitabu vya Kiswahili na majarida ya kiusomi yanayozungumzia suala la wanawake ili kufafanua na kuweka wazi nafasi ya wanawake katika jamii.

## 1.7 MISINGI YA NADHARIA

Kwa kuwa utafiti huu ni wa kudhihirisha usawiri wa mwanamke katika nyimbo za sifo za Wakamba, nadharia itakayoongoza utafiti huu ni ile ya Ufeministi. Kulingana na Wamitila (2002), nadharia ni mawazo, mpango, mwongozo au maelezo yaliyowekwa ili kusaidia kutatua au kutekeleza jambo fulani. Pia ni vyema kuelewa kuwa nadharia yoyote ile ya uhakiki ni nyenzo tu ya kutusaidia kulifikia lengo fulani.

Msokile (1993) anafafanua, nadharia ni mawazo, mpango, mwongozo, maelezo yaliyowekwa ili kusaidia kutatua au kutekeleza jambo fulani. Mawazo ya Msokile yatakuwa kama mwongozo katika utafiti huu ili kufanikisha vyema malengo yaliyokusudiwa.

Massamba (2009:63) anasema, nadharia ni taratibu, kanuni na misingi ambayo imejengwa katika muundo wa kimawazo kwa madhumuni ya kutumia kama kielelezo cha kuelezea jambo. Maoni haya yalisaidia utafiti huu kwa kuchunguza misingi, taratibu, na kanuni zilizowekewa mwanamke ili kumpa nafasi yake katika jamii. Kwa jumla, nadharia ni jumla ya maelezo, taratibu, kanuni, misingi, mwongozo na mpango unaotumiwa na mhakiki au mtafiti ili kumsaidia kuifanikisha kazi yake. Kwa hivyo nadharia ni mawazo, maelezo au mwongozo uliopangwa ili kusaidia kueleza, kutatua au kutekeleza jambo fulani.

### 1.7.1 Nadharia ya Ufeministi

Wafula na Njogu (2007), wanatoa maoni kuwa Nadharia ya Ufeministi hupigania haki za wanawake katika jamii ya ubabedume. Wanadai kwamba mhimili mkuu wa nadharia hii ni kubaguliwa kwa wanawake katika jamii kwa misingi ya jinsia yao ya kike. Hali hii inawaweka miongoni mwa wanyonge katika jamii. Beauvoir (1949), anashambulia asasi mbili za jamii zinazochangia ukandamizaji wa wanawake. Asasi hizi ni za ndoa na tamaduni. Anaendelea kusema kwamba dini inamfunza mwanamke kuwa mnyenyekevu; ndoa inampa mwanamume uwezo mkubwa akilinganishwa na mwanamke, nao utamaduni umemsawiri mwanamke katika njia iliyo hasi na duni.

Mbatiah (2001:87) anaeleza kuwa nadharia ya ufeministi inajishughulisha na utetezi wa haki za wanawake dhidi ya ukandamizwaji katika jamii zenye mfumo uliodhibitiwa na wanaume. Nadharia hii ni mwafaka kwa kazi yetu kwa sababu kimsingi inashughulikia maswala ya wanawake na kupinga dhuluma na maonevu dhidi ya wanawake kwa misingi ya jinsia yao. Kwa hivyo kupitia nyimbo hizi za sifo za Wakamba tutachunguza iwapo mwanamke ametetewa au la.

Mary Wollstonecraft ndiye anayefahamika kuwa mtaalamu wa kwanza kuyazungumzia masuala ya wanawake kwa utaratibu maalumu. Katika kazi yake, *A Vindication of the Rights of Women* (1792), anapendekeza kuundwa kwa jamii mpya iliyo na usawa. Simon de Beauvoir (1949) katika makala iitwayo *The Second Sex* kama alivyonukuliwa na Wamitila (2002) katika *Uhakiki wa Fasihi* ni kuwa Ufeministi ulikuwa wa kuushambulia uana ambao ni dhana ya kitamaduni inayomwangalia mwanamke kama kitu hasi na duni, huku ikimchukulia mwanamume kama binadamu kielelezo.

Eagleton (1986), anasema kuwa kuna tofauti kati ya mwandishi wa kike na kiume. Anaendelea kudai kuwa uandishi wa kiume unabainika kuwa ule wa kawaida na pindi mwandishi wa kike anapoandika basi kunakuwepo na ulinganisho kati ya jinsia hizi mbili. Mawazo haya yanatushawishi kujiuliza iwapo kuna wanaume wanaowatetea wanawake kwa kutoa sifa chanya ama wakati wote humsawiri kama kiumbe duni. Wahakiki na wananadharia hawa wote wanashikilia kwamba mifumo ya kiume katika asasi zinajitokeza katika misingi ya ubabe-dume inamnyanyasa mwanamke na hana budi kuipinga kwa kila njia.

Kulingana na Wafula na Njogu (2007: 92) kuna njia mbili za kuainisha matapo fulani ya nadharia ya ufeministi. Kuna uainishaji unaoangazia maswala ya mwanamke kimaeneo na uainishaji unaozingatia mrengo wa kiitikadi. Uainishaji unaozingatia mirengo hii ulitokana na fahamu kwamba, wanawake wanakabiliwa na matatizo na changamoto tofauti tofauti kutegemea maeneo wanakotoka.

Wanaunisai wenye asili ya ulimwengu wa tatu, hasa bara la Afrika wana mielekeo ambayo inashinikiza upekee wa jamii na tamaduni za Kiafrika. Wanapendelea umuhimu wa kuzamia masuala ya kinisai katika misingi ya tamaduni zenye maono ya kimaendeleo. Upekee wa

kitajiriba, kimazingira na kitamaduni huwatofautisha na wenzao weusi katika ulimwengu wa Kimagharibi (Shitemi, 2008).

Kulingana na wahakiki hawa wa kifeministi, wanawake wa Ufaransa walitilia mkazo matumizi ya lugha, kwamba lugha ilitumiwa kwa kumpendelea mwanamume. Wanawake wa Marekani waliwaunga mkono wale wa Ufaransa.

Wanawake wa Uingereza nao walitia mkazo suala la siasa na historia. Kwa maoni ya wanawake hawa wa Uingereza, ni kwamba wenzao wa Marekani walisisitiza masuala ya hisia. Wanawake wa Afrika nao wakawa na mtazamo tofauti na wenzio wa Ulaya na wale wa Marekani, kwao suala la utamaduni ndilo lililowakabili (Yego, 2013).

Ufeministi wa Kiafrika huchunguza maswala ya kitamaduni yanayomlemaza mwanamke. Aidha hushughulikia maswala ya kijinsia kwa kujikita katika muktadha wa Kiafrika. Lengo kuu la uhakiki wa nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ni kuzua mikakati ambayo itaangazia na kutathmini jinsia ya kike, mitazamo, thamani na matakwa ya mwanamke sio tu katika fasihi bali nyanja zote za maisha (Mbatia, 2001). Utafiti huu utajikita katika nadharia hii kwa sababu watunzi wa nyimbo hizi za sifo za Wakamba ni wanajamii Waafrika na nyimbo zenyewe zimetungwa katika muktadha na mazingira ya Kiafrika.

#### 1.7.1.1 Mihimili ya Nadharia ya Ufeministi

Wafula na Njogu (2007) kwa kuzingatia matapo ya Kimaeneo na Kiitikadi wamefafanua mihimili ya nadharia ya ufeministi kama ifuatavyo:

i) Ni nadharia inayotumia fasihi kama jukwaa la kuelezea kwa uyakinifu hali aliyomo mwanamke ili kumsaidia mtu yeyote kuielewa hali hiyo.

ii) Nadharia hii inanuia kuwasawazisha wanadamu kwa upande wa utamaduni na uana. Inapigania jamii mpya yenye msingi katika amali za kibinaadamu.

iii) Ni nadharia inayokuza na kuendeleza hisia za umoja wa wanawake kama kundi linalodhulumiwa.

iv) Nadharia hii hunuia kuzidua mwamko kwa upande wa wanawake jinsi wanavyojiona na uhusiano wao na wa watu wengine.

v) Mtazamo huu vile vile unajaribu kuhamasisha utungaji wa kazi za sanaa zenye wahusika wa kike wanaoweza kuigwa, wanawake ambao hawawategemei wanaume ili wajitambulishe.

Katika utafiti wetu, tulijikita katika mrengo wa mtazamo wa Kiafrika kwani watunzi wa nyimbo hizi ni wanajamii ya Waafrika na zimetungwa katika muktadha na mazingira ya Kiafrika. Katika mtazamo wa Kiafrika wanawake wa Kiafrika wanasisitiza zaidi upinzani dhidi ya utamaduni unaomnyima mwanamke nafasi ya kutekeleza malengo yake. Miongoni mwa vitengo vya utamaduni huu ni; kutotambuliwa kwa mwanamke kama mzazi wa wanajamii, tohara na ukeketwaji wa mwanamke, kimya cha kulazimishwa, desturi na mila zinazomdhalilisha kama vile kuonewa kwa mwanamke tasa, ndoa za lazima, vita vya nyumbani miongoni mwa nyingine.

Kutokana na tahakiki mbalimbali zinazozidi kuongezeka kuhusu utafiti wa masuala ya uana, ni wazi kwamba ipo haja ya kuziendea tamaduni zetu na kuzitafakari dhidi ya nadharia zifaazo kushughulikia fasihi za Kiafrika. Tafiti mbalimbali zimeonyesha pia kwamba dhana za uana na ujinsia zinavyoeleweka na nchi za kimagharibi ni tofauti na jinsi hali ilivyo katika jamii nyingi za Kiafrika. Kama anavyoeleza Ogundipe-Leslie (1998), dhana ya ‘mwanamke’ katika muktadha

wa Kiafrika ina maana pana zaidi kuliko ule ufinyu wa kimagharibi wa kuyatazama maumbile yake.

Momanyi (2002) anaeleza kuwa, katika baadhi ya jamii zetu kama vile Igbo (Nigeria), Bemba (Zambia) na Taveta (Kenya), mwanamke anaweza kuchukuliwa kama 'mume' au 'baba' wa watoto kutokana na kadhia anazotimiza. Anaelezea kwamba, mwanamke anaweza 'kumwoa' mke, akalipa mahari. Kwa hivyo, ingawa jamii nyingi barani Afrika ni za kuumeni, dhana ya 'mwanamke' haikusimamiwa tu na umbo lake au hali yake ya kijinsia. Aliweza kutimiza majukumu mengi, yakiwemo yale yaliyofikiriwa kuwa ni ya kiume katika jamii.

### 1.7.2 Ufeministi wa Kiafrika

Mwasisi wa Ufeministi huu ni Filomena Steady (1981), anayefafanua kuchunguza hali ya jamii na tamaduni zinazorutubisha unyanyasaji wa mwanamke katika jamii. Steady (1981), anasema kwamba Ufeministi wa Kiafrika umejikita katika mwelekeo wa kuangalia majukumu tofauti ya kijinsia kama yanavyoegemea na kukamilishana. Anaendelea kusema kwamba majukumu haya yanaenda sambamba na jinsia na hata husababisha hali ya usawa. Mawazo mengine kuhusu Ufeministi wa Kiafrika yanabainika katika maoni ya Wamitila (2003:253) kwamba:

> Ufeministi ni istilahi inayotumiwa kueleza mojawapo ya nadharia ya uhakiki, imewekwa msingi na msukumo mkubwa, pamoja na nia ya kupigania ukombozi wa mwanamke kutokana na pingu za kitamanduni, kidini, kijamii, kisiasa na kiuchumi. Ufeministi huishambulia mitazamo ya kiume jinsi mwanamke anavyopaswa kuhisi, kufikiri na kuziitikia hali mbalimbali kimaisha.

Maoni haya ya Wamitila yanaonekana kukubali kwamba mwanamume ndiye kikwazo kikuu kwa ukombozi wa wanawake. Wanawake wa Kiafrika nao wanapinga utamanduni unaomnyima mwanamke nafasi ya kutekeleza malengo yake. Kwa maoni yao, utamaduni unaomfanya mwanamke kukosa uwezo wa kuchagua kuwa mke, ukeketaji, kuwa kimya na hata kudhalilishwa hasa wale wanawake walio tasa.

Katika kushughulikia nadharia ya Ufeministi, ni bora ifahamike kwamba kuna mihimili ambayo ni ya kimsingi. Kwanza, nadharia hii imetumia fasihi kama jukwaa ya kuelezea hali ya mwanamke katika jamii. Nyimbo za sifo kama fani mojawapo ya fasihi simulizi ni mwafaka katika kuchunguza na kuelezea hali ya mwanamke katika jamii. Pili, nadharia hii inanuia kuleta usawa wa kijinsia na kitamaduni kupitia kwa miundo misingi inayopatikana katika jamii. Inapigania jamii mpya inayoheshimu jinsia ya kike kupitia amali zake.

Mwasisi wa Ufeministi huu wa Kiafrika anafafanua matarajio ya nadharia yenyewe. Kwake, nadharia inafaa kuchunguza hali za kijamii na tamaduni zinazorutubisha unyanyasaji wa wanawake katika jamii. Nadharia yenyewe ina mitazamo ifuatayo:

i) Inadhihirisha nia na malengo mahususi yanayotokana na hali halisi katika jamii za Kiafrika.

ii) Inatambua historia ya jamii za Kiafrika, zilizokuwa na watawala na mashujaa wanawake.

iii) Inachunguza hali ya mwanamke katika jamii ambazo zimekuwa na harakati za ukombozi na ujenzi wa jamii mpya.

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika haina budi kuzama katika mila, desturi na kaida za kijamii ili ibainishe usawiri wa mwanamke na uwezo wake katika utendakazi sambamba na anavyofanya

mwanamume mbali na kuangalia dhuluma atendewazo mwanamke katika ufanisi wake kulingana na ulimwengu ulivyo.

Hata hivyo Ufeministi wa Kiafrika unaingiliana na unisai wa Kimagharibi pale ambapo mitazamo yote inatambua mwanamke. Popote pale, mwanamke ni mwananchi wa kiwango cha chini na ipo haja kuirekebisha hali hii. Utafiti huu utahakiki nyimbo za sifo za Wakamba kimaudhui kwa minajili ya kuonyesha jinsi kila mtunzi anavyomsawiri mwanamke kwa kuzingatia Ufeministi wa Kiafrika.

## 1.8 HITIMISHO

Sura hii imeeleza juu ya vipengele vifuatavyo: Utangulizi, Usuli wa mada, Suala la utafiti, Madhumuni ya utafiti, Maswali ya utafiti, Sababu za kuteua mada, Upeo wa utafiti na Misingi ya nadharia. Sura inayofuata inahusu yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti.

# SURA YA PILI

# YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA YA UTAFITI

## 2.1 UTANGULIZI

Sura hii inatathimini yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti. Imeonyesha mchango uliotokana na kazi hizo huku ikibainisha tofauti iliyopo kati ya tafiti hizo na utafiti huu. Masuala yanayohusu wanawake ni muhimu na huibua hisia tofauti katika jamii hasa wakati huu ambapo wanawake wameanza kujitambua na kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa jamii mpya nchini Kenya. Kazi nyingi zimetafitiwa kuhusu wanawake katika riwaya, tamthilia na ushairi. Hata hivyo, utafiti huu ulichunguza kazi hizo na kuangalia yale yaliyofaa kuchangia utafiti huu na kuyagawanya katika aina mbili:

(a.) Maandishi kuhusu utanzu wa nyimbo

(b.) Maandishi kuhusu suala la wanawake.

## 2.2 MAANDISHI KUHUSU UTANZU WA NYIMBO

Nyimbo ni kipera kikongwe miongoni mwa vipera vya fasihi simulizi ambacho hutekeleza majukumu muhimu katika jamii (Wamitila, 2002). Nyimbo zina dhima muhimu katika jamii hasa katika kuwasilisha maoni, mitazamo na mielekeo ya watu kuhusu masuala kadha yakiwemo ya kijamii (Mbarwa, 1989). Wamitila (aliyetajwa) anaendelea kueleza kuwa nyimbo ni ala muhimu za mawasiliano ambazo hutumia tamathali za usemi kupitisha ujumbe kwa walengwa wake.

### 2.2.1 Maana ya Nyimbo

Wataalamu mbalimbali wametoa maelezo anuwai kuhusu maana ya wimbo. Kwa mujibu wa *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004:645), wimbo ni maneno yanayotamkwa kwa sauti ya muziki.

Matteru (2003) katika makala yake, fasihi simulizi na andishi anasema kwamba nyimbo ni aina ya ushairi unaoimbwa pekee au kwa kuhusishwa na ngoma. Anadokeza kuwa nyimbo ni tungo za kishairi zenye kutumia mahadhi, melodia, mapigo na muwala. Wimbo unaweza kuimbwa na mtu mmoja pekee au na wazumi wake wakiitikia mikarara.

Wamitila (2003:104) anasisitiza kuwa, kazi ya kisanaa ya nyimbo hutokana na mazingira. Mazingira ndiyo yanayozalisha hisia na hatimaye kwa msanii. Hivyo basi katika wimbo panapaswa kuwa na wazo maalum ambalo linawasilishwa kwa hadhira husika kwa njia ya sauti. Nyimbo ni zao la shughuli za binadamu na hisia zake na hivyo huzingatia miktadha mbalimbali.

Kutokana na maelezo ya wataalamu hawa, nyimbo ni fani ya fasihi simulizi ambayo hutolewa katika muktadha fulani ili maana yake ieleweke. Maelezo haya yanaupa utafiti huu msingi thabiti wa kuchanganua nyimbo za sifo za Wakamba.

### 2.2.2 Nyimbo za Sifo

Wamitila, (2004) anaeleza kuwa sifo ni tungo za kusifu. Anaendelea kusema kuwa sifo huweza kumsifu mtu kutokana na matendo yake ya kishujaa au ya kijasiri. Anaelezea kuwa sio sifo zote ambazo hutoa sifa nzuri au chanya, zipo nyingine ambazo hukashifu au kutoa sifa kinyume, kuumbua, kumnyambua, kukosoa miongoni mwa nyingine.

Baadhi ya vitanzu vya sifo ni: majigambo, tondozi na pembezi. Majigambo ni maghani ambayo ni ya kujisifu. Kwa kawaida majigambo hughaniwa na mtunzi anayehusika. Tondozi ni tungo ambazo huwasifu watu, wanyama au vitu. Mtunzi anaweza kukisifu kitu chochote alichochagua na ambacho kwa maoni yake kinastahiki sifa hizo. Pembezi ni aina ya tondozi ambazo zimetengewa watu wa aina fulani. Aghalabu hawa huwa, kwa mfano, watu mashuhuri wanaosifika kutokana na matendo yao au nafasi walizo nazo katika jamii.

Sifo kwa hivyo huimbwa kwa lengo la kusifu wahusika kwa sababu ya ushujaa, cheo, kipawa cha pekee na mambo ambayo wameweza kuyatekeleza. Sifo huhimiza wanajamii kuiga matendo yanayosifiwa, kufunza maadili na amali za jamii. Baadhi ya sifo huwa zinakashifu au kukejeli**.** Tangu jadi jamii ya Wakamba ilikuwa na nyimbo za sifo. Mfano mzuri ni ule wimbo ulioimbiwa Kisoi wa Munyao alipoukwea Mlima Kenya (1963). Nyimbo hizi zingali zinaimbwa katika jamii ya Wakamba hadi sasa. Watunzi wa nyimbo hizi huweza kuimba kukisifu kitu au mtu katika jamii. Mtunzi anaweza kuimba kuusifu urembo wa mwanamke au kusifu tabia fulani. Vile vile mtumzi anaweza kukashifu tabia mbaya za watu katika jamii.

Nyimbo za sifo hutoa sifa mbalimbali ziwe chanya au hasi za wahusika ili kupitisha ujumbe kwa walengwa. Hubeba mawazo, fikra, falsafa na hutoa hisia. Nyimbo zina utendakazi muhimu katika shughuli za kijamii. Jamii ya Wakamba katika shughuli zao za kila siku husikiliza nyimbo. Wanajamii wanapofanya kazi mbalimbali kama vile ususi, kukarabati magurudumu, kuuza mboga, kulima miongoni mwa kazi nyingine wao huimba na pia kusikiliza muziki. Nyimbo za Kikamba pia huchezwa katika magari yao ya uchukuzi. Haya yote huwafanya wanaofanya kazi mbalimbali kupunguziwa na makali ya kazi zile

Mifumo ya kijamii kama vile elimu ya kisasa pamoja na dini imechangia kubadilika kwa mitindo ya nyimbo za jamii ya Wakamba. Ijapokuwa nyimbo hutumika katika matukio muhimu katika kuziumba dhamira mbalimbali za jamii mpya, taswira ya kuridhisha haijapewa wanawake. Baadhi ya mambo waliyotengewa na kuzungumziwa wanawake hayaridhishi. Kwa mfano, mtoto wa kiume akianguka anaambiwa aamke na asilie kwani wanaume hawalii (*Iyumisye aume mayiaa*), dhana kuwa wanaolia ni wanawake. Pia kuna kicheko mtu anachoweza kucheka na kuambiwa kuwa aache kucheka kama mwanamke (*Wing'ang'auka uu ko wi mundu muka*).

Dhana ya mwanamke kupewa sifa sizizofaa inaonekana katika jamii ya Wakamba. Matumizi ya lugha hukuza na kupalilia taasubi ya kiume katika jamii ya Wakamba kupitia matumizi ya lugha.

Wataalamu wengi wameshughulikia utanzu wa nyimbo. Miongoni mwao ni Finnegan (1970). Finnegan alijihusisha na aina za nyimbo hususan nyimbo za wawe, nyimbo za sifa za mashujaa vitani na za wasasi mawindoni huku akionyesha jinsi nyimbo zilivyotumika katika maisha ya kila siku. Amedhihirisha jinsi nyimbo zilivyotumika kutetea haki za wafanyakazi waliojikuta katika mazingira ya unyanyasaji hasa katika nchi zilizotawaliwa na wakoloni kama vile Afrika Kusini. Amebainisha kuwa, nyimbo zinaweza kutumiwa kama chombo cha kujitetea. Vile vile aliainisha umuhimu wa nyimbo katika jamii za Kiafrika na jinsi dhima ya nyimbo hizi inavyobainika. Anasema kuwa nyimbo ni chombo mwafaka cha fasihi simulizi kinachoongoza jamii kuyafikia malengo ya ufanisi. Anaendelea kueleza kuwa , nyimbo huchukua jukumu kubwa la kuelimisha, kutahadharisha na kuburudisha jamii inayohusika. Utafiti wa Finnegan uliweka wazi maoni kwamba, umuhimu wa nyimbo hupatikana katika maudhui na mtindo wa nyimbo hizo. Kazi yake ilifaa utafiti huu kupitia maudhui ya nyimbo aliyofafanua pamoja na maelezo aliyoyatoa kuhusu majukumu ya nyimbo katika jamii. Tofauti na utafiti huu, Finnegan alijikita katika nyimbo za jadi ilhali utafiti huu ulishughulikia nyimbo za sifo za kisasa za jamii ya Wakamba.

Akitafitia kuhusu umuhimu wa nyimbo katika jamii za Waembu na Wambeere, Chesaina (1991) alidhihirisha kuwa, nyimbo kama utanzu wa fasihi simulizi zinaweza kutumiwa kama chombo cha kuwazindua wanajamii waliokandamizwa na utamaduni wa kijadi. Chesaina alidai kuwa, wimbo kama utanzu wa fasihi simulizi ni chombo muhimu cha kueleza hisia wakati wa kuingia sherehe miongoni mwa wanawake. Aidha, alidhihirisha kuwa nyimbo huweza kutumiwa kama

jukwaa la kupinga udhalimu wowote unaoendelezwa na utamaduni. Aligundua haya kupitia utafiti wake kuhusu nyimbo kama chombo cha kuelezea umoja wa kijinsia miongoni mwa Waembu na Wambeere. Utafiti wa Chesaina ulikuwa muhimu katika kazi hii kupitia majukumu ya nyimbo aliyoyabainisha. Vilevile, jamii alizotafitia za Waembu na Wambeere zina utamaduni ulio na ukuruba na ule wa Wakamba ambao ndio watafitiwa katika utafiti huu. Hata hivyo, utafiti wa Chesaina unatofautiana na utafiti huu kwa sababu alijifunga katika nyimbo za sherehe ya unyago katika jamii za Waembu na Wambeere ilhali utafiti huu ulishughulikia nyimbo za sifo katika jamii ya Wakamba.

Mbiti (1991) anasema kwamba, nyimbo, methali na hekaya zinapatikana katika jamii nyingi za Kiafrika. Fani hizi huwa zinatokea katika kipindi maalumu na huwa na ujumbe unaobainika. Aidha, huwa na maudhui maalumu kuhusu nyanja fulani ya maisha. Maudhui ya nyimbo aliyoyashughulikia Mbiti, yalinufaisha utafiti huu kwani yanafafanua kuwa, nyimbo hutokea katika kipindi mahususi na huwa na maudhui maalumu kuhusu nyanja za maisha. Maudhui ya nyimbo kwa mujibu wa Mbiti, hubadilika mara kwa mara. Haya ni muhimu kwa sababu nyimbo zilizotafitiwa na utafiti huu zilitungwa katika vipindi tofauti vya maisha. Utafiti wa Mbiti ulijishughulisha na tanzu mbalimbali za fasihi simulizi tofauti na utafiti huu ambao ulijikita katika usawiri wa mwanamke katika nyimbo za sifo za jamii ya Wakamba.

Nao utafiti wa Yalwala (1991) ulishughulikia maudhui katika nyimbo za John Mwale ambapo alitathmini maudhui kwa mujibu wa muktadha uliyoyazalisha. Maudhui yaliyojadiliwa ni yale ya siasa, umoja, uzalendo na maadili katika jamii. Yalwala amechunguza namna maudhui ya nyimbo yanavyoweza kuathiri jamii na jinsi nyimbo hizo zinavyoleta ufahamu na umoja katika jamii yake. Utafiti wa Yalwala uliufaa utafiti huu kupitia kipengele cha maudhui

alichoshughulikia. Vilevile ulifafanua umuhimu wa muktadha katika utunzi wa nyimbo. Hata hivyo, kazi yake ni tofauti na hii kwa kuwa alijifunga katika nyimbo za msanii John Mwale ilhali utafiti huu ulijifunga katika nyimbo za sifo za jamii ya Wakamba za wasanii hawa: Wanginga, Kakai Kilonzo, Bosco Mulwa, John Muasa, Kijana Mumo, Dan Mutuku, Dicky Mulwa, Ancent Munyambu na Justus Myello.

Mwai (1997) katika utafiti wake kuhusu nguvu na uwezo wa nyimbo kwa wanawake Waswahili, amegundua kuwa ingawa wanaume wa jamii ya Waswahili wana uwezo uliokithiri katika ndoa, wanawake wamebuni njia zao za kuelezea hisia zao, maumivu yao na mateso wakitumia nyimbo na ngoma zilizotungwa na kuimbwa na wanawake. Hisia za wanawake Waswahili kulingana na Mwai, hudhihirika kupitia maudhui katika nyimbo. Mwai alilenga kubainisha kuwa, nyimbo zina utendakazi muhimu katika jamii ya Waswahili. Kupitia kwa nyimbo, wanawake wanapitisha hisia zao kwa wanaume ili mabadiliko yaweze kupatikana. Utafiti wa Mwai uliufaa wetu kupitia kipengele cha maudhui alichoshughulikia na pia utendakazi wa nyimbo alizochunguza. Utafiti wa Mwai ni tofauti na huu kupitia jamii aliyoshughulikia na pia utanzu wa nyimbo alioshughulikia.

Wambua (2001) alitafiti kuhusu mtindo na matumizi ya lugha katika nyimbo za Kakai Kilonzo. Kupitia kazi yake, mtafiti huyu alibainisha kuwa uteuzi wa lugha katika uwasilishaji wa ujumbe ni muhimu katika utunzi wa kazi ya fasihi. Aidha, Wambua alibainisha uhusiano kati ya uteuzi wa lugha na maudhui. Kazi ya Wambua ilichangia pakubwa kazi hii kwa kuipa mwelekeo wa kuchanganua nyimbo kimaudhui kwa kuangalia lugha inayomsifu mwanamke. Hata hivyo, utafiti wake ni tofauti na huu kwani yeye alitafitia nyimbo za Kakai Kilonzo akilenga kubainisha matumizi ya lugha katika nyimbo hizo na jinsi lugha inavyofafanua maudhui ilhali utafiti huu

ulichunguza usawiri wa mwanamke katika nyimbo za sifo za Wakamba za watunzi : Kakai Kilonzo, Bosco Mulwa, Dan Mutuku, Justus Myello, Kijana Mumo, Wanginga, Dickson Mulwa na John Muasa.

Kwa mujibu wa Wamitila (2003), nyimbo husheheni mawazo na huonyesha uhusiano wa kijamii. Aidha, nyimbo huchukua sehemu kubwa ya maisha ya binadamu. Anasema takribani shughuli zote za maisha ya binadamu kama kulima, kubembeleza mtoto, kupasha tohara na kuvuna huandamana na nyimbo. Vile vile ameeleza dhana ya nyimbo na kufafanua dhima ya utanzu huu wa fasihi simulizi katika jamii. Pia ameainisha nyimbo mbalimbali kwa mujibu wa dhima zake. Kuhusu nyimbo za sifo, anaeleza kuwa zinatumika kutoa sifa za mtu ziwe nzuri au mbaya. Kulingana naye, sifo huweza kumsifu mtu kutokana na matendo yake ya kishujaa au ya kijasiri. Kazi ya Wamitila ilifaa utafiti huu kupitia ufafanuzi wake wa dhima za nyimbo hasa nyimbo za sifo ambazo zilishughulikiwa na utafiti huu.

Kwa mujibu wa King'ei na Kisovi (2005), nyimbo zimeenea miongoni mwa jamii mbalimbali na huimbwa kuambatana na shughuli tofauti. Kulingana na King'ei na Kisovi nyimbo huwa katika makundi mawili makuu. Nyimbo za kimapokezi na zile za kisasa. Nyimbo za kimapokezi wanasema hupokezwa kizazi hadi kingine. Lengo kuu la nyimbo za kisasa kulingana nao ni kuchuma mali. Wanasema nyimbo za kisasa zina uwazi mwingi, maneno hayana adabu na midundo yao ina ucheshi mkubwa. Wanaeleza kwamba, mwimbaji huteua mambo kadha muhimu yanayoathiri jamii yake. Wanaongezea kwamba, si kila mtunzi wa kazi ya sanaa huchukua maudhui moja kwa moja kutokana na matukio ya kijamii bali huweza kutunga kwa kutaka kulifurahia tukio maalumu lililomsibu. Kipengele cha maudhui walichokishughulikia

pamoja na mambo yanayomsukuma mtunzi kutunga wimbo yaliufaa utafiti huu kwa kuchanganua mabadiliko katika nyimbo za sifo za Wakamba.

Utafiti mwingine uliokuwa na mchango kwa utafiti wetu ni wa Kilauni (2007) aliyetafitia athari za usasa katika maudhui na utendakazi wa *itheke*; "yaani, ngoma katika jamii ya Wakamba". Kilauni anaeleza kuwa, ujumbe wa ngoma ya *itheke* miongoni mwa jamii ya Wakamba hubadilika kulingana na wakati, tukio, mazingira na hadhira. Katika utafiti wake aligundua kuwa, usasa katika maudhui unajitokeza katika maswala ambayo hayalengi jamii ya Wakamba, bali yanalenga jamii pana ya Kenya na ulimwengu kwa jumla. Kulingana na Kilauni, usasa katika nyimbo ndio unaofanya nyimbo za *itheke* kutekeleza majukumu ya kijamii. Umuhimu wa utafiti wa Kilauni kwa huu ni kwamba, amefafanua chimbuko na historia ya jamii ya Wakamba iliyochunguzwa na utafiti huu. Vile vile alibainisha maudhui ya nyimbo ambayo yalikuwa na mchango katika utafiti huu. Tofauti na kazi ya Kilauni ni kuwa, Kilauni alijikita katika ngoma za jamii ya Wakamba ilhali utafiti huu ulishughulikia nyimbo za kisasa za sifo za Wakamba.

## 2.3 MASUALA KUHUSU WANAWAKE

Lugano (1989) ameshungulikia usawiri wa mwanamke kisiasa, kiuchumi na kijamii katika riwaya nne za Kezilahabi: *Rosa Mistika* (1971*) Kichwa Maji* (1974*), Dunia Uwanja wa Fujo* (1975) na *Gamba la Nyoka* (1979) katika tasnifu yake ya Uzamili. Katika kazi hii ameonyesha jinsi mwanamke alivyosawiriwa kama mtegemezi wa mwanamume, chombo chake na chanzo cha maovu yote. Anasema kuwa mwandishi ameendeleza falsafa za jamii yake kongwe kuhusu wanawake ambayo inamchukulia kama kiumbe duni. Kwa hivyo, anakatisha tamaa kuhusu ukombozi wa wanawake. Anaendelea kudai kuwa unyonge wa mwanamke umemfanya kuwa kisingizio cha kila jambo bovu linalotokea katika ndoa. Ikiwa mwanamke amezaa wasichana

pekee, kosa litakuwa lake, ikiwa hakuzaa kabisa pia kosa ni lake. Utafiti wake ulifaa utafiti huu kwani ulituchorea picha kuhusu mwanamke katika fasihi ya Kiswahili.

Momanyi (2002), katika utafiti wa “Kiswahili na Maswala ya Uana” anaeleza kuwa fasihi ya Kiswahili haina budi kutathimini upya swala la mwanamke kwa kuanza kushughulikia namna ambavyo mwanamke anaweza kuigwa kutokana na uwezo wake. Anaelezea kuwa wanawake halisi wanatekeleza majukumu mengi muhimu ambayo hubainisha vipawa vyao na hivyo ni lazima kudhihirisha sifa zao pasi kudidimizwa kwa ule uwezo wao wa kimaumbile. Katika kazi yake anajadili Nadharia ya Ufeministi kama nadharia badalia inayoweza kushughulikia fasihi za Kiafrika ikiwemo ya Kiswahili. Anaelezea lengo la nadharia hii ni kufufua na kurutubisha sauti ya mwanamke wa Kiafrika ambayo miaka mingi imekuwa imefukiwa na mamlaka ya kiume. Kazi hii ilikuwa na umuhimu mkubwa katika utafiti wetu kwani ilichangia kuweka bayana nafasi anayopewa mwanamke kupitia nyimbo za sifo za Wakamba, hivyo kutambua sifa za mwanamke mwenye uwezo na sifa za kuigwa. Tofauti iliyopo kati ya uchunguzi huu na wa Momanyi, ni kuwa Momanyi alishughulikia Fasihi andishi na maswala ya uana ilhali utafiti huu ulichunguza nafasi ya mwanamke katika nyimbo za sifo za Wakamba.

Maingi (2005) naye utafiti wake ulichunguza na kutathmini “Upembezwaji wa Mwanamke katika Udokezi wa Nafasi ya Mwanamke katika Utenzi wa Fatumah.” Anaonyesha namna mwanamke anapembezwa kwa kutoshirikishwa katika maamuzi muhimu ya kijamii ilhali anasifiwa kwa mchango wake wa kulea watoto nyumbani. Kazi hii ilikuwa na umuhimu kwetu kwani ilitupa mwanga zaidi juu ya asasi zinazomtweza mwanamke. Hata hivyo, tofauti ni kuwa mhakiki huyu aliangazia utenzi ilhali utafiti huu uliangazia nyimbo.

Katola (2006), amechunguza udhalimu dhidi ya wahusika wanawake katika tamthilia za Kiswahili nne. Tamthilia hizo ni za waandishi wa jinsia tofauti ambazo ni Muhando, *Hatia* (Muhando, 1972) na *Mama Ee (*Mwachofi, 1987). Hawa ni waandishi wa kike. Waandishi wa kiume waliandika *Buriani* (Yahya na Mulwa, 1983) na *Kitumbua Kimeingia Mchanga* (Mohamed, 2000). Katola anasema kuwa kwa kuzingatia Ufeministi wa Kiafrika, baadhi ya taasisi zinatumiwa kumdhulumu mwanamke na zafaa kuondolewa. Baadhi ya dhuluma alizotambua ni wanawake kuozwa bila hiari, kupigwa, kunyimwa haki na kukataliwa na jamii miongoni mwa nyingine. Matokeo yake ni mtazamo hasi kwa mwanamke katika jamii. Katika kazi yake hakuegemea upande wowote wa waandishi ila ameonyesha kuwa mwanamke anadhulumiwa na mifumo ya kiume katika taasisi ambazo zimejikita katika misingi ya ubabe-dume. Utafiti huu umekuwa wa manufaa katika utafiti wetu kwa sababu mtazamo wake kuhusu dhuluma umeupatia mwanga kutambua zile dhuluma na changamoto wanazopitia wanawake. Mawazo yake yalisaidia utafiti huu kuchunguza jinsi hali ilivyo kwa sasa karne ya ishirini na moja. Tofauti na utafiti wake ni kuwa, Katola alichunguza tamthilia lakini utafiti huu ulichunguza nyimbo za sifo za kisasa za Wakamba.

Mirikau (2011) alishughulikia taswira ya mwanamke katika tamthilia za Wamitila, ambazo ni: *Wingu la Kupita* (1999), *Pango* (2003) na *Seserumbe* (2009). Katika utafiti huo, Mirikau amejitahidi kufafanua istilahi “taswira” kwamba ni jinsi mtu anavyochorwa na kuweza kutoa picha kamili ya namna anavyoonekana. Anaendelea kueleza kuwa picha hii aghalabu hutokana na namna anavyofikiriwa kupitia mambo yanayopitia akilini mwa binadamu. Mambo haya huweza kudhihirika kupitia matendo halisi anayotendewa mwanamke. Mwanamke anatendewa na hata mwenyewe huweza kujitendea mambo ya kushangaza katika jamii husika. Anatamatisha kwa kusema kuwa taswira hii ni kuhusu ngazi katika jamii ambayo hujikuta amewekwa na

kukubali aidha atukuzwe au adhalilishwe. Vile vile kujidhalilisha mwenyewe. Mawazo ya Mirikau yalisaidia utafitii huu kwa kuyamulika matendo anayotendewa mwanamke na kubainisha changamoto zinazomkabili katika mfumo wa kijamii. Anadhihirisha namna ambavyo mwanamke ana utegemezi mkubwa wa kiuchumi na hata kifikra ilhali analimbikiziwa mzigo mzito katika jamii. Hii ni taswira mojawapo anayoangazia Mirikau. Tofauti na kazi hii ni kuwa Mirikau alijikita katika kuchunguza taswira ya mwanamke katika tamthilia ilhali utafiti huu ulishughulikia usawiri wa mwanamke katika nyimbo za sifo za Wakamba.

Yego (2013) katika tasnifu yake ya Uzamili alichunguza "Nafasi ya mwanamke na jinsi inavyotetewa katika nyimbo za Taarab za Zanzibar". Anasema kuwa nafasi ya mwanamke inayohusu juhudi za mwanamke za kupinga ukandamizwaji ni pamoja na kunyanyaswa kikazi na kiuchumi. Kulingana na Yego, mwanamke anaweza kujinasua katika hali hii kwa kupinga utamaduni usiomruhusu kujitengea nafasi yake katika jamii. Tofauti na utafiti wetu ni kuwa, Yego ameshughulikia nyimbo mbili za Taarab za Zanzibar zilizotungwa na mwanamume na mwanamke ilhali sisi tulishughulikia nyimbo za sifo za jamii ya Wakamba zenye watunzi wanaume pekee ambao wamewasawiri wanawake katika maoni chanya na hasi. Ni kupitia utafiti huu ambapo tulichunguza mchango wa mwanamume katika suala hili la kumpa mwanamke nafasi yake, hasa ikibainika kuwa mwanamume anachukuliwa kama kikwazo cha mwanamke kupata nafasi yake katika jamii.

Ruto (2015) katika tasnifu yake "Matatizo ya Mwanamke katika *Riwaya ya Kidagaa Kimemwozea* (Ken Walibora) na *Nyuso za Mwanamke* (Said A. Mohamed)" ameelezea madhila na dhuluma anazopitia mwanamke katika maisha ya kila siku. Madhila hayo ni kama vile: ndoa za lazima, kudharauliwa, kunyimwa haki za kuchuma mali na kurithi, dhuluma za kimapenzi

miongoni mwa mengine. Pamoja na hayo, mtafiti amebainisha athari zinazowakabili wanawake kutokana na dhuluma hizo. Miongoni mwa athari hizo ni kusambaratika kwa ndoa, kukosekana kwa uhusiano mwema wa kinyumba, kifo, woga na upweke. Utafiti huu ulifaa kazi hii kwa sababu umezungumzia kuhusu masuala yanayohusu wanawake ukibainisha matatizo wanayokabiliana nayo kila siku. Hivyo ulikuwa kama dira katika kuangazia nafasi ya mwanamke katika jamii na haswa katika jamii ya Wakamba.

Katika gazeti la *Daily Nation,* Agosti 1, 2016, kuliripotiwa kisa cha mwanamke aliyekatwa mikono na mume wake kutokana na utasa. Ripoti hii iliufaa utafiti huu sana kwa sababu iliupa mwanga juu ya uhusiano wa mume na mke hasa katika suala la watoto katika familia sana sana katika jamii ya Wakamba.

Fakih (2017) katika utafiti wake wa kutathmini mabadiliko ya " Usawiri wa Wanawake katika riwaya mbili za Said A. Mohamed ambazo ni *Utengano* na *Kamwe Si Mbali* " ameangazia uwezo mkubwa wa mwanamke wa kutenda matendo mbalimbali ambayo ameyagawanya katika sehemu mbili ambazo ni hasi na chanya kwani anaamini kuwa mwanamke ni binadamu. Amegundua kuwa kuna tofauti kati ya usawiri wa mwanamke katika maisha ya zamani na usawiri wa mwanamke katika maisha ya sasa kwa kubaini kuwa mwanamke wa sasa amebadilika na anajiamini kuliko wa zamani. Kazi hii ilikuwa na umuhimu mkubwa katika utafiti wetu kwani mtafiti huyu amebaini kuwa usawiri wa mwanamke umebadilika kiwakati. Hivyo ulikuwa kama mwongozo wa kusaidia kuchunguza sifa anazopewa mwanamke katika nyimbo hizi za sifo za Wakamba za watunzi wa kiume.

Katika gazeti la *Daily Nation*, Agosti 2, 2018 kuliripotiwa kisa cha mwanamke aliyechapwa na kuumizwa na mumewe kutokana na tetesi kwamba mke huyu hakuwa mwaminifu. Ripoti hii

iliufaa utafiti huu kwani ilionyesha mateso wanayopitia wanawake mikononi mwa waume wao na hasa ikibainika kuwa kisa hiki kilitokea katika jamii ya Wakamba ambao ndio watafitiwa. Ripoti hii ilisaidia kuchunguza iwapo kuna nyimbo ambazo zilimpa mwanamke wa Kikamba sifa za kukubalika na za kumuona mwanamke huyu katika macho mengine tofauti na yale ya ubaya tu.

## 2.4 HITIMISHO

Sura hii imekuwa na umuhimu mkubwa katika utafiti huu kama sura nyinginezo. Kwa muhtasari sura hii ilijikita kujadili kwa kina vipengela muhimu ambavyo vinatoa uhai wa utafiti huu. Mtafiti aliweza kutalii kazi mbalimbali zilizoandika na wataalamu tofauti ili kuthibitisha hoja na dhana mbalimbali zinazohusiana na mada ya utafiti huu. Sura inayofuata inahusu Mbinu za utafiti.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 UTANGULIZI

Sura hii inafafanua vipengele muhimu vifuatavyo: muundo wa utafiti, eneo la utafiti, walengwa wa utafiti, mbinu za usampulishaji na sampuli, vifaa vya utafiti, ukubalifu na utegemeo wa vifaa vya utafiti, mbinu za kukusanya data, uchanganuzi wa data na maadili ya utafiti. Kwa jumla sura hii inaeleza jinsi utafiti ulivyofanyika kuhusu mada husika ya utafiti.

Kothari (2004) anaeleza kuwa mbinu za utafiti ni jumla ya mbinu au taratibu zote stahiki zinazotumika wakati wa kufanya utafiti. Mbinu hizi zinajumuisha njia zote za uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data na uchanganuzi wa data.

## 3.2 MUUNDO WA UTAFITI

Utafiti huu ulitumia muundo wa kimaelezo na kitarakimu. Enon (1999) anaeleza kuwa muundo wa kimaelezo ni njia ya ukusanyaji na uchambuzi wa data kwa njia ya maelezo, ambapo nambari huwa hazitumiki. Aidha, muundo wa kitarakimu ni muundo ambao mtafiti huzikusanya data na kuzifanyia uchambuzi kwa kutumia tarakimu. Hivyo, data katika utafiti huu zilikusanywa na kuchambuliwa kwa njia ya maelezo na kitarakimu kwa pamoja.

## 3.3 ENEO LA UTAFITI

Enon (1998) anaeleza kwamba, eneo la utafiti la kijiografia ni mahali mahususi ambapo mtafiti amekwenda au amepatumia katika kukusanya data za utafiti wake. Hivyo, mtafiti alikusanya data yake katika mji wa Machakos. Alizuru maduka mbalimbali kama vile duka la Sokomoko, yanayouzwa kanda za video na santuri na kununua CD alizohitaji. Mji wa Machakos ndimo anamoishi mtafiti.

## 3.4 WALENGWA WA UTAFITI

Sampuli ni sehemu ya watu ama vitu vinavyotafitiwa ambavyo vinapatikana kutoka kundi kubwa la watu ama vitu hivyo. Watu hao huteuliwa na mtafiti kwa kuzingatia sifa na tabia zao ambazo zinaweza kukidhi katika kuwakilisha kundi pana la watu lililobakia (Kothari, 2004).

Sampuli katika utafiti huu ni nyimbo kumi za sifo zilizotungwa na watunzi wanaume pekee kutoka jamii ya Wakamba. Wanajamii ishirini vile vile walipewa hojaji. Wanajamii hawa waliolengwa walikuwa ni kuanzia miaka ishirini na zaidi kwani umri huu mtu huwa amekomaa kiasi cha kubainisha njema na mbaya. Walitoa maoni yao kuhusu usawiri wa mwanamke katika nyimbo teule kumi.

## 3.5 MBINU ZA USAMPULISHAJI NA SAMPULI

Utafiti huu ulitumia sampuli ya kimakusudi. Uteuzi wa sampuli kimakusudi uliegemezwa kwa kile kilichomwongoza mtafiti, yaani sababu fulani maalum za kitafiti na kiuchunguzi alizonazo. Kwa mujibu wa Mugenda na Mugenda (1999), uteuzi wa sampuli kimakusudi humruhusu mtafiti kuteua eneo na wahojiwa ambao wana habari kuhusu suala la utafiti. Utafiti huu ulijikita katika nyimbo kumi za sifo za Wakamba zilizotungwa na watunzi wa kiume pekee; tano zilizotungwa miaka ya themanini katika karne ya ishirini (karne 20) na tano za miaka ya hivi sasa karne ya ishirini na moja (karne 21) ambazo ziliteuliwa kimakusudi. Kigezo kilichotumika ni kuzungumzia mwanamke.

Ingawa zipo nyimbo nyingi za Wakamba zinazohusu masuala mbalimbali ya kijamii kama vile nyimbo za siasa, mapenzi miongoni mwa nyingine, tuliziteua nyimbo hizi kumi za sifo kwa sababu mwanamke amezungumziwa zaidi kama mhusika mkuu na tuliamini kuwa data tuliyoipata katika nyimbo hizi ilitimiza lengo letu na kufanikisha utafiti huu. Kwa mfano, Bosco Mulwa anazo nyimbo nyingi zinazohusu masuala mbalimbali ya kijamii, lakini zile tulizoteua

zinazungumzia masuala ya wanawake na tunaamini kuwa zilifaa utafiti huu. Mijadala mingi ya kijinsia huangazia nafasi duni ya mwanamke na udhaifu wake wala sio uwezo alionao. Kwa upande mwingine mwanamume amechorwa kuwa ndiye anayeendesha dhuluma hizi dhidi ya wanawake. Tulikusudia kutathimini kupitia nyimbo hizi za sifo za Wakamba nafasi mpya ya mwanamke katika jamii anayopewa na mwanamume kwa sababu kumekuwa na dhana kuwa vita vya ukombozi wa mwanamke ni vya mwanamke pekee.

## 3.6 VIFAA VYA UTAFITI

Utafiti huu ulitumia vifaa: kalamu, daftari, kipakatalishi, rununu, na CD. Vifaa hivi vilisaidia kunakili chochote kilichohusiana na mada ya utafiti wetu. Santuri na kanda za video zilitumika kwa ajili ya kutazama na kusikiliza nyimbo hizo. Rununu ilitumika katika kuwasiliana na baadhi ya watunzi na pia kuhifadhi nyimbo hizi za sifo. Kipakatalishi kilisaidia kutafitia kupitia mtandao na kuweka kumbukumbu za data yetu.

## 3.7 UKUBALIFU NA UTEGEMEO WA VIFAA VYA UTAFITI

Utafiti huu ulitumia vifaa mbalimbali katika ukusanyaji wa data. Kabla ya utafiti wenyewe, mtafiti alifanyia vifaa vya utafiti majaribio ili kuhakikisha uhalali na utegemeo. Umuhimu wa kuzingatia uhalali na utegemeo wa vifaa vya utafiti umesisitizwa na Mugenda na Mugenda (2003). Vifaa vya utafiti vilifanyiwa majaribio mwezi wa Agosti na Septemba mwaka 2018. Kila kifaa kiliufaa utafiti kama ifuatavyo:

### 3.7.1 Kalamu na Karatasi

Kalamu na karatasi zilitumika kuandika data mbalimbali zinazohusiana na mada ya utafiti. Aidha, mielekeo, maoni na falsafa za watafitiwa kuhusiana na mada ya utafiti zilinakiliwa

kupitia kalamu na karatasi. Vifaa hivi viliufaa utafiti huu kwa sababu ni vyepesi na hubebwa kwa urahisi na havihitaji utaalamu kuvihifadhi.

### 3.7.2 Rununu

Rununu ni kifaa cha mawasiliano ambacho hutumika katika ukusanyaji wa data wakati wa utafiti (Kothari, 2004). Rununu ina uwezo wa kunasa sauti, kupiga picha tuli za wahusika na mandhari ya utendaji na pia kuchukua video. Aidha ilitumiwa kurekodi maoni waliyoyatoa watafitiwa kuhusiana na mada ya utafiti. Kifaa hiki kiliufaa utafiti huu kwa sababu mtafiti alisikiliza nyimbo zilizorekodiwa mara nyingi iwezekanavyo kabla ya uchanganuzi wa data na pia kuwasiliana na watunzi.

### 3.7.3 Kipakatalishi na Wavuti /Tovuti

Kipatakalishi kilitumika kwa kiwango kikubwa kuchapa kazi hii ya utafiti kuanzia mwanzo hadi mwisho. Wavuti zilitumika kwa lengo la kutafitia machapisho, tasnifu na taarifa nyinginezo muhimu zilizohusiana na mada ya utafiti.

## 3.8 MBINU ZA KUKUSANYA DATA

Utafiti huu ulijumuisha kuzuru maeneo mbalimbali katika mji wa Machakos ambapo kuna maduka tofauti yanayouza santuri (CD) za nyimbo za sifo zilizorekodiwa katika maeneo mbalimbali na watunzi tofauti wa kiume na ambazo zinazungumzia wahusika wanawake pekee. Mtafiti alizinunua nyimbo hizi na kuzisikiliza na hatimaye kuzinakili katika daftari. Vile vile aliwahoji wanajamii ishirini (20) kupata maoni yao kuhusu swala hili.

Pili utafiti huu ulifanywa maktabani ambapo mtafiti alizisoma na kuzihakiki kazi mbalimbali juu ya masuala ya wanawake. Uchunguzi ulifanywa kuhusu suala la wanawake katika vitabu, majarida, tasnifu na machapisho mbalimbali katika maktaba.

Njia nyingine ya ukusanyaji data ilikuwa mtandao. Mtafiti aliyapitia yaliyoshughulikiwa kuhusu mada ya utafiti kwa minajili ya kukusanya na kunakili mambo yaliyo na manufaa katika kazi hii.

## 3.9 MAADILI YA UTAFITI

Ukusanyaji data kupitia mbinu yoyote ya utafiti huhitaji kuzingatia maadili kwa upande wa watafitiwa, mtafiti na mchakato wa utafiti (Mulokozi, 2003; Kothari, 2004; Kobia, 20008). Mtafiti alizingatia maadili kwa kuandika barua ya kujitambulisha na kuomba kibali cha kukusanya data kutoka kwa Halmashauri ya Kitaifa ya Sayansi na Teknolojia na Ubunifu na kupata kibali cha kukusanya data katika sehemu teule ya utafiti.

Mtafiti vilevile alizingatia maadili ya utafiti kwa kutowalazimisha wasailiwa kutoa maoni yao wala kuwachachawiza wakati wa kuyajibu maswali. Aliwaelezea watafitiwa sababu za kukusanya data yake na pia kutumia lugha iliyoelewaka na wasailiwa. Vile vile aliwaeleza kuwa, maoni yao yatahifadhiwa vyema na ni kwa kusudi la utafiti pekee. Utafiti huu ulizingatia maadili kwa kunukuu kazi za kitaaluma zinazohusiana na mada ya utafiti.

## 3.10 HITIMISHO

Sura hii imezingatia vipengele vifuatavyo: Muundo wa utafiti, Eneo la utafiti, Walengwa wa utafiti, Mbinu za Usampulishaji na Sampuli, Vifaa vya utafiti, Mbinu za kukusanya data na Maadili ya utafiti. Kwa jumla kila kipengele kina umuhimu wake katika kukamilisha kazi nzima ya utafiti huu. Sura inayofuata inahusu Uwasilishaji na Uchanganizi wa data.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA

## 4.1 UTANGULIZI

Sura hii inaeleza vipengele vya msingi vifuatavyo: muhutasari wa nyimbo za sifo, usuli wa watunzi, usawiri wa mwanamke katika nyimbo za sifo za jamii ya Wakamba na hitimisho. Data ilichanganuliwa kupitia uchanganuzi elezi na takwimu elezi. Baada ya kuzisikiliza na kuziandika nyimbo hizi, mtafiti alidondoa kauli, maandishi, misimamo na itikadi zinazodhihirisha nafasi ya mwanamke na jinsi anavyosawiriwa kwa mujibu wa watunzi hawa na kuhakiki thamani yake kwa mwanamke.

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Ufeministi na jinsi mihimili yake muhimu ilivyofanikisha kazi hii. Kauli zinazomtweza mwanamke na zile zinazomtetea na kumkinga kutokana na imani dunishi katika jamii zilidondolewa. Mtafiti aliziainisha kauli hizi mbili za watunzi hawa wanaume kisha kutathimini ikiwa zimempa thamani mwanamke au la kwa kiwango cha asilimia.

Maswala mbalimbali kuhusu usawiri wa mwanamke yaliorodheshwa ili kuchunguza jinsi kila mwimbaji alivyoyajadili kwa kutumia utokeaji, na kuyaweka katika viwango vya asilimia (%). Hii ilisaidia kupambanua ni masuala yepi ya watunzi hawa yanayoshughulikiwa katika nyimbo upi kwa kiwango gani.

Vile vile data ilichanganuliwa kupitia majedwali mbalimbali kudhihirisha kutukuzwa au kutwezwa kwa mwanamke katika nyimbo tulizozitafitia. Tulichunguza ni kwa kiwango gani (asilimia) kila wimbo unavyoonyesha jinsi mtunzi na jamii wanavyotetea nafasi ya mwanamke kwa mujibu wa maudhui yaliyojitokeza katika kila wimbo.

## 4.2 KUHUSU WATUNZI

Watunzi wa nyimbo hizi ni wanajamii kutoka kaunti tatu za Ukambani ambazo ni Kitui, Machakos na Makueni. Nyimbo walizoziimba zimerekodiwa katika studio mbalimbali katika maeneo tofauti ya nchi ya Kenya. Wameimba kuhusu masuala mbalimbali ya kijamii yakiwemo yanayohusu wanawake.

Kwa mfano mtunzi Kakai Kilonzo ambaye kwa sasa ni marehemu alizaliwa mwaka wa 1954 Kilimambogo, katika kaunti ya Machakos. Aliongoza kikundi cha wanamuziki cha Kilimambogo Brothers. Mwaka wa 1978 kikundi hiki kiligawanyika japo kuna nyimbo walizozitunga pamaja. Kakai Kilonzo aliziimba nyimbo zake kwa lugha asilia ya Kikamba na pia Kiswahili. Alikuwa miongoni mwa wanamuziki wa Ukambani waliobobea. Aliaga dunia mwaka wa 1987 baada ya kuugua kwa muda mfupi.

Ancent Munyambu ni mtunzi mwingine mkongwe wa nyimbo za Kikamba. Aliaga dunia mwaka wa 2017 kutokana na mshituko wa moyo. Alikuwa na miaka 77. Ancent ni mzaliwa wa kaunti ya Makueni. Aliishi mtaa wa Mathare jijini Nairobi. Musyoki Mumo pia alikuwa mwanamuziki mwingine wa nyimbo za Kikamba. Alizaliwa mwaka wa 1970 katika kijiji cha Kimangu kaunti ya Machakos. Aliaga dunia mwaka wa 2000 kutokana na ajali ya barabarani. Alijulikana kwa jina la muziki kama "Kijana Mumo".

Wanginga ni baadhi ya wanamuziki wakongwe wa Ukambani ambaye angali hai na ni mzaliwa wa kaunti ya Machakos. Yeye huimba nyimbo zake kwa lugha ya Kikamba. Bosco Mulwa ni mtunzi chipukizi anayeimba nyimbo zake akigusia masuala mbalimbali katika jamii. Anajulikana kwa jina la msimbo la *'One Man Guitar'*. Amezaliwa katika kaunti ya Makueni.

John Muasa pia ni mtunzi wa nyimbo za Kikamba ambaye anaonekana kunawiri sana katika nyimbo zake . Yeye huimba kwa lugha ya Kikamba. Huyu ni mzaliwa wa kaunti ya Machakos.

Justus Myello ni mzaliwa wa kaunti ya Machakos . Ni miongoni mwa waimbaji chipukizi. Alianza kuimba mwaka wa 2012. Nyimbo zake hugusia masuala mbalimbali ya kijamii. Dan Mutuku pia ni mtunzi wa siku hizi, amezaliwa katika kaunti ya Machakos.

## 4.3 USAWIRI WA MWANAMKE

Njia ambayo ilisaidia katika kutambua jinsi mwanamke alivyosawiriwa ni kupitia kwa watunzi wa nyimbo hizi za sifo za Wakamba ambao ni wanaume. Hapa mwanamume ametumika kufafanua mhusika wa kike. Watunzi hawa wameonyesha tabia za wahusika kutokana na jinsi wanavyoingiliana na wanajamii. Hivyo basi, kutambua jinsi wanaume wanavyomchukulia mwanamke.

Mtafiti amebaini kuwa, usawiri wa mwanamke umejitokeza katika hali mbalimbali zilizo chanya (njema) na hasi (mbaya). Mtafiti akitumia nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika amechambua usawiri wa mwanamke katika nyimbo kumi za sifo za jamii ya Wakamba kama alivyoongozwa na maswali ya msingi yafuatayo:

i) Mwanamke amepewa sifa za aina gani katika nyimbo za sifo za Wakamba?

ii) Mwanamke amesawiriwa vipi katika nyimbo za sifo za Wakamba zilizotungwa na watunzi wa kiume?

iii) Je, jamii ya Wakamba imebadili mawazo na kumsawiri mwanamke kama binadamu sawa na mwanamume kupitia maudhui ya nyimbo hizi?

Maswali haya ya msingi yameenda sambamba na malengo mahsusi, la kwanza na la pili la utafiti huu yasemayo: Kutathimini sifa anazopewa mwanamke katika nyimbo za sifo za Wakamba, kuchunguza jinsi ambavyo mwanamke amesawiriwa katika nyimbo za sifo za Wakamba na pia kuchunguza iwapo usawi wa mwanamke mkamba unaakisi hali halisi ya maisha ya hivi sasa karne hii ya ishirini na moja. Katika kuyajibu maswali haya ya msingi, mtafiti amefafanua sifa hasi zinazojitokeza katika usawiri wa mwanamke na sifa chanya za usawiri chanya wa mwanamke kama ulivyojitokeza katika nyimbo kumi teule za sifo za Wakamba.

## 4.4 USAWIRI CHANYA WA MWANAMKE

Wamitila (2002), anaeleza kuwa, usawiri mzuri wa wahusika unawafanya wasomaji wajitambulishe nao kwa kuhisi wanavyohisi na kuwaza wanavyowaza. Watunzi wa nyimbo hizi wameweza kuangazia nguvu na usawiri chanya wa mwanamke. Wameonyesha mchango wake muhimu katika jamii kupitia sifa mbalimbali.

### 4.4.1 Mwanamke Kama Anayewajibika

Uwajibikaji ni jambo muhimu katika kuijenga jamii imara na yenye kuhitaji mafanikio. Wanajamii wanapowajibika katika kazi mbalimbali husaidia sana maendeleo ya nchi. Nyimbo za sifo za Wakamba zimemsawiri mwanamke kama mwenye bidii katika kazi. Nyimbo mbili (2) zimedhihirisha haya ambazo ni sawa na asilimia ishirini (20%). Nyimbo hizi *Aka* wa Justus Myello na *Mother* ya Bosco Mulwa.

Wimbo wa Justus Myello *Aka* (Wanawake) umemsawiri mwanamke kama mwenye kuwajibika, anayefanya kazi kutimiza mahitaji ya familia. Haya yanabainika katika ubeti huu.

| | |
|---|---|
| *Masisye maithi nguni na mbisu yi iko,* | Wanawake hutekeleza majukumu, |

| | |
|---|---|
| *Usini kiwu nokuuta na indo nowe ukathasya,* | Kama kuchanja kuni, kupika, kuchota maji, |
| *Kitanda nowe ukalanya na kusuvia musee*. | Kuchunga mifugo pamoja na kutunza familia. |

Ubeti huu, unatubainishia ugumu wa kazi za nyumbani anazofanya mwanamke. Kazi hizi huchangia katika ujenzi wa familia na taifa kwa jumla. Maelezo ya Justus Myello yanaonyesha kazi anazofanya mwanamke wa jamii ya Wakamba. Katika hali halisi ya maisha kazi hizi ndizo hufanywa wa wanawake katika jamii hii. Msanii huyu ameibua taswira ya mwanamke mwenye kuwajibika. Kulingana na Wanaufeministi, mwanamke anastahili kupewa nafasi za kazi sawa na wanaume. Kule kuwajibikia kazi za pale nyumbani kwa mwanamke ni dhihirisho kuwa mwanamke ana uwezo wa kufanya kazi vizuri akipewa nafasi.

Kazi ya kupika, kuchanja kuni na kuchota maji huwa ya mwanamke katika jamii ya Wakamba. Wanawake katika jamii ya Wakamba huonekana na mitungi migongoni majira ya asubuhi wakitoka visimani. Wengine hutumia punda kubebea mitungi. Majira ya jioni wao huonekana wameeleka matita ya kuni huku wakiwaongoza mifugo wao kuelekea nyumbani. Wafikapo nyumbani wao huanza kazi ya mapishi. Hali hii hutokea katika hali halisi ya jamii ya Wakamba. Mtunzi Bosco Mulwa katika wimbo wa *Mother (*Mama) amemsawiri mwanamke kama mwenye kuwajibika. Mtunzi anaeleza namna mama yake alivyompeleka hospitalini alipokuwa mtoto mchanga na kumwepushia matatizo ya magonjwa sugu ya utotoni. Anayaeleza haya kupitia ubeti huu:

| | |
|---|---|
| *Mauau mathuku ta mukambi kana volio*<br>*Wandwaie nzanzoni na matyaangwata,*<br>*Liu ngua na kisomo wandeie nesa.* | Magonjwa sugu kama vile surua na polio<br>Ulinipeleka kuchanjwa na si kuugua.<br>Mahitaji ya kimsingi kama vile chakula,<br>Nguo na elimu ulinitimizia. |

Mama amesawiriwa kama mtu anayewajibikia majukumu yake. Kule kuwapeleka watoto wake kuchanjwa, kunaonyesha kuwa ni mtu anayejua majukumu yake. Kwa kutembelea vituo mbalimbali vya afya mjini Machakos na viunga vyake, kama vile Mitaboni, Masii, Wamunyu, Mwala na Kathiani, uchunguzi ulibaini kuwa asilimia kubwa ya wanawake katika jamii ya Wakamba ndio huwapeleka watoto wao kuchanjwa dhidi ya magonjwa mbalimbali. Idadi ya wanaume huwa ndogo na wengine huwa wameandamana na wake zao. Hali hii ni kweli kuwa wanawake wanashughulikia masuala ya malezi ya familia zao.

Suala la afya ni jambo ambalo limepewa kipaumbele katika jamii ya sasa. Jambo hili linatiliwa nguvu katika nchi ya Kenya ili kuzitimiza Ajenda Nne kuu ikiwemo masuala ya afya. Mama wa Taifa Bi. Margret Kenyatta ni mwanamke ambaye amejitolea kwa vyovyote vile kuhakikisha magonjwa yameangamizwa katika taifa la Kenya. Bi. Kenyatta ni mfano wa wanawake wa kuigwa.

### 4.4.2 Mwanamke Kama Mchumi

Mwanamke vile vile amesawiriwa akifanya biashara kama vile kuuza viazimbatata, mihogo na maparachichi. Haya yote wanafanya ndiposa walete mabadiliko katika jamii na kujiepusha na umaskini. Huku kujitegemea kibiashara na kikazi kunampa mwanamke uhuru wa kibinafsi unaoambatana na mwelekeo wa nadharia iliyotumiwa. Wanawake hawa hawategemei waume zao katika kugharamia kila kitu katika nyumba zao. Bidii ya mwanamke humwezesha kujikimu yeye mwenyewe pamoja na familia yake. Haya yameelezwa katika ubeti huu:

| | |
|---|---|
| *Aingi matatite maundu , tuviasala,* | Wengi wamejaribu mambo mbalimbali |
| *Vai kindu kivinya Ukamba ta kuea syana,* | Kama vile biashara, hakuna jambo ngumu |
| *Kuta maluu na manga na mavokando,* | Ukambani kukimu familia kwa kuuza viazi, |
| *Mekiite vitii kulungy'a ukya musyi.* | Mihogo na maparachichi. Wanawake hutia |

Bidii ili kumaliza umaskini katika familia.

Justus Myello anaonyesha kwamba, mama hufanya kazi kubwa sana ya kustahili kusifiwa. Wanawake katika jamii ya Wakamba hutekeleza majukumu haya. Kwa mfano mtafiti alitembelea gulio kuu la Machakos mjini na wengi wa wauzaji bidhaa zikiwemo nafaka, mboga na bidhaa nyingine walikuwa wanawake. Alitalii maeneo mbalimbali katika soko hili akapata wanawake wauza mboga walikuwa wengi. Wanawake wengi walikuwa wametandaza mboga zao kwenye magunia ardhini. Wengine walikuwa na vibanda, huku wengine wakizungusha bidhaa hizi kwa kuzibeba mikononi mwao ili kuwafikia wateja. Hii ni hali halisi katika jamii ya Wakamba.Kule kuchuma kwa mwanamke kunamwondolea utegemezi wake kwa mwanaume. Mwanamke anapofanya kazi, hujifaidi yeye mwenyewe pamoja na jamii nzima.

### 4.4.3 Mwanamke Kama Mshauri Mwema

Suala la kutoa ushauri mwema lina umuhimu mkubwa katika kuijenga familia na jamii kwa jumla. Ushauri mwema utawezesha kurutubisha jamii yoyote kwa ukamilifu. Katika nyimbo hizi imebainika kuwa mwanamke ana uwezo mkubwa wa kushauri juu ya msingi bora wa maisha na tahadhari kuhusu mambo ya ulimwengu yanayoweza kumletea mtu balaa baadaye. Nyimbo mbili (2) zimeangazia suala hili sawa na asilimia ishirini (20%).

Mtunzi Wanginga katika wimbo *Aka nima mithemba* (Aina mbalimbali za Wanawake) amemsawiri mwanamke kama mshauri mwema. Anaeleza vile nyanya alimtahadharisha kuhusu wanawake kwa kumwambia kuwa wanawake ni wa aina mbalimbali. Alimwelezea kuwa kuna wanawake ambao ni virukanjia na wengine wenye tabia ya umbeya. Mawaidha haya aliyopewa na bibi yake yalikuwa na umuhimu mkubwa katika kumwongoza mtunzi huyu hasa wakati wa kutafuta mchumba wa ndoa.

| | |
|---|---|
| *Natavawa ni susu ngamba kwona ta ithau,* | Nilipowosiwa na nyanya nilidhani ni utani, |
| *Natavawa ni susu ngamba kwona ta ithau,* | Kuna aina mbalimnali za wanawake, |
| *Aka ni ma mithemba, ve uko wa kilata,* | Wapo wanawake virukanjia na |
| *Ve uko wa usavi* | Wengine wambeya |

Nyanya anawakilisha wanawake wenye kutoa ushauri mwema kwa wajukuu. Hii sifa nzuri ya kushauri, inamjenga mwanamke na kumthaminisha. Katika jamii ya Wakamba kina babu na nyanya walikuwa wakiwashauri wajukuu wao. Mafunzo haya zamani yalitolewa nyakati za usiku baada ya kazi za mchana. Siku hizi kina nyanya na babu bado huwashauri wajukuu wao japo kutangamana kwao kumepungua kutokakana na mabadiliko ya maisha. Wakati mwingi wajukuu wao huwa shuleni na wengine wanaishi na wazazi wao mbali na kina babu na nyanya.

Bosco Mulwa katika wimbo wa *Mother* (mama) amemsawiri mwanamke kama mshauri mwema. Alimtahadharisha na dunia ambayo imejaa maovu na misukosuko. Alimwelezea umuhimu wa kuvumilia kwa kumwambia kuwa, mtu anapovumilia hatimaye hufanikiwa. Hii ni sifa nzuri anayopewa mama kuonyesha kuwa, wanawake wanajua wajibu wao. Haya yamejitokeza katika ubeti huu:

| | |
|---|---|
| *Wambiia Sheri, nthi yusuite ntina* | Ukanishauri Sheri dunia imejaa dhiki |
| *Iyuumisye sua umwe nukona nesa.* | Nivumilie siku moja nitafanikiwa |

Mara nyingi mama ndiye hukaa na watoto. Wakati huu yeye hupata fursa ya kuwaelewa vizuri. Ukambani kazi ya ulezi nyakati nyingi huwa ya mwanamke. Utampata akiwa na watoto wake katika shughuli nyingi anazozitekeleza pale nyumbani. Akiwa jikoni akipika, watoto huwa

wamemzingira huku wakiota moto. Anapokuwa shambani kufanya shughuli mbalimbali, watoto huandamana naye. Huu unakuwa wakati mwema wa mama kuwashauri watoto wake.

Ushauri huo hubaki kwenye akili ya mtoto na huwa na manufaa katika maisha yake ya baadaye. Jambo hili mtunzi analiweka wazi anapotumia wakati uliopita. Anamwambia mama alikuwa akimwambia kuwa, dunia imejaa maovu ajiepushe nayo. Mama pia alimuasa juu ya uvumilivu, alimwambia kuwa anayevumilia maishani hatimaye hufanikiwa. Kwa hakika mama amechorwa kama mshauri mwema.

Kupitia nukuu hizi imedhihirika kuwa mwanamke anahitajika katika maendeleo ya familia na jamii kwa jumla. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika imetilia mkazo zaidi katika kumpa mwanamke nafasi kwa kuzingatia uwezo wake ikiwa ni pamoja na uwezo mkubwa wa kushauri juu ya mambo na mipango ambayo inaweza kuleta mafanikio katika jamii.

### 4.4.4 Mwanamke Kama Mkombozi

Kutokana na uchanganuzi wa nyimbo hizi nafasi ya mwanamke kama mkombozi imejitokeza. Data hizi zinaonyesha kuwa wanawake wanaweza kujikomboa katika hali tofauti. Ukombozi huu unaweza kuwa ni wa kifikra, kiuchumi na hata ukombozi wa kiutamaduni. Nyimbo nne kwa nyimbo kumi zilizoteuliwa ambazo ni sawa na asilimia arubaini (40%) zimeonyesha kuwa mwanamke anaweza kujikomboa katika hali yoyote inayomtatiza katika maisha.

Nafasi ya ukombozi wa mwanamke imedhihirika kupitia kwa watunzi wa nyimbo hizi. Wimbo wa *Nyinya wa Ndetei* (Mama wa Ndetei), umemsawiri Mama Ndetei ambaye aliamua kujikomboa kutokana na minyororo ya ndoa na kuamua kupata talaka. Katika wimbo huu, msanii amemwonyesha mwanamke akifanya maamuzi yanayohusu maisha yake bila

kumtegemea mwanamume. Anafanya uamuzi mzito maishani mwake wa kuachana na mume wake wa ndoa. Ubeti huu unadhibitisha haya:

| | |
|---|---|
| *Nyinya wa  Ndetei, nyinya wa Nthiwa,*<br>*Mami wa Koreta,*<br>*Nyinya wa syana ni ivityo yau yu neekie,*<br>*Kuma wathi ona kavalua ndunandikia* | Mama Ndetei, mama Nthiwa,<br>Mama Koreta, Mama watoto ni kosa gani nililokukosea.<br>Tangu uende kwenu hata barua hunitumii. |
| *Nyinya wa Ndetei, nyinya wa Nthiwa, mami wa Koreta,*<br>*Kyeva kya ngoo na kimako nikyambingiviie,*<br>*Kethiwa wi tei ukambona yu wamba kuia,*<br>*Kethiwa wi tei ukambona ninamosie* | Mama Ndetei, mama Nthiwa, mama Koreta,<br>Ninahuzunika sana mwoyoni,<br>Ukiniona mama unaweza kunihurumia,<br>Hali yangu si hali nimekonda |

Ubeti huu unaeleza jinsi mama watoto alivyomtaliki mume wake. Tangu mama watoto alipoondoka alikatiza mawasiliano na mume wake. Mume wake anamrai  anamwuliza kosa alilomkosea. Mwanamke huyu ameamua kujikomboa kutoka katika ndoa iliyojaa dhuluma. Hii ndio sababu hataki kuwasiliana tena na mume wake. Mume wake anamwelezae hali yake, jambo ambalo linamfanya kuona kuwa mke wake si msamehevu.

Nyamweya (2018) anasema kuwa, katika kila hatua ya kumnusuru kiumbe yeyote, lazima utakutana na vikwazo fulani. Nyamweya anaendelea kueleza kuwa, vikwazo hivi huweza kutokana na anayenusuriwa au kutokanana njia inayotumika kumnusuru kiumbe huyo. Utafiti huu unakubaliana na mawazo ya mtafiti huu kwani kule kumrai mke kurudi kunaonyesha

changamoto alizokuwa akipitia mwanamume huyu. Dhana ya kuwa mke wake ndiye anayestahili kushughulika na yanayompata mume wake si sahihi. Wote wawili wanastahili kushughulika.

Yapo maswali ambayo mume wake anajiuliza katika wimbo wake huu: *Konakwikie ata mama?* (Kwani nilikufanyia nini mwanamke?), *Ko ve nai itaekeawa?* (Kuna kosa ambalo halisamehewi?). Maswali haya anayoyauliza yanaonyesha kuwa huyu mume ndiye aliyemkosea mke wake. Anajutia majuto ya mjukuu ambayo huja baadaye. Kule kumtaka mke wake amsamehe ni dhihirisho kuwa alikuwa amemkosea.

Wimbo wa *Syoka Mami* (Rudi Mama)  mama yake mtunzi aliamua kujinasua kutoka kwa ndoa na kwenda mjini kujitafutia maisha. Mtoto wake anamrai arudi nyumbani huku akimwuuliza ni kwa nini aliamua kuwaacha na ni yeye aliyewazaa. Mtumzi anayaonyesha haya kupitia ubeti huu:

| | |
|---|---|
| *Nayu ni myaka mingi,* | Umepita muda mrefu mama tangu uondoke, |
| *Twikalite twina kimako nue,* | Tumeishi kuuliza baba ulikoenda |
| *Tuikulya ndandi mami kula waendie* | Punde si punde, Tukapata habari |
| *Kalungu kalungu tukewa uvumi,* | Kuwa unaishi mtaa wa Kibera Nairobi, |
| *Wioneka Kibera kisaki Ilovi,* | Ukichuma mali na Mugikuyu anayeuza mabati |
| *Wikalite na Mwikuyu wa maleve.* | |

Ubeti huu unaeleza jinsi mama mzazi alivyoondoka nyumbani na kwenda mjini Nairobi kuchuma mali. Mtoto huyu anamtaka arudi nyumbani. Sababu za kuondoka kwake nyumbani hatujaelezwa. Masuala mengi katika ndoa wanayowapitia wazazi yanakuwa vigumu watoto kuyatambua. Mtoto huyu haelewi sababu za mama kuondoka. Hatua ya kwenda kujitafutia riziki mjini ni ukombozi wake kiuchumi.

Justus Myello na Bosco Mulwa katika nyimbo zao *Aka* (Wanawake) na *Mother* (Mama) wamemsawiri mwanamke kama mwenye uwezo wa kujikomboa kiuchumi. Mwanamke anaonekana kufanya biashara ndogo ndogo kuweza kuyakimu mahitaji ya nyumbani. Biashara hizi ni pamoja na kuuza viazi, mihogo na maparachichi. Katika jamii ya Wakamba wanawake ndio hufanya biashara hizi. Wengine wamefungua vibanda vya kuuza mboga na wengine hutandaza mboga zao kwenye magunia.

Biashara hizi zimewawezesha kujikimu kimaisha pamoja na kuwasomesha watoto wao. Kufanya biashara huku ni ukombozi wa mwanamke kiuchumi. Hivyo wanawake wanafanya majukumu ya kuchuma mali kama wanaume. Hii ni sifa chanya inayoonyesha wanawake wana uwezo kama ule wa wanaume katika kutafutia jamii na familia zao.

### 4.4.5 Mwanamke Kama Mlezi wa Familia

Suala la ulezi ni kazi nzito inayohitaji kujitolea ili kuimarisha familia bora. Uchunguzi umedhihirisha kuwa mwanamke anao uwezo wa kujitoa mhanga ili kuilea familia yake. Mwanamke katika jamii ya Kiafrika anahitajika kuijali familia yake kuhakikisha kuwa imepata lishe bora. Jamii huwa na matarajio maalum kwa mwanamke yeyote. Mwanamke anajitwika jukumu la kuwatayarisha na kuwafunza watoto jinsi ya kutayarisha chakula, kuwatunza watoto na waume na hata shughuli nyinginezo za nyumbani.

Utafiti huu unaonyesha kuwa nyimbo nne (4) zimegusia suala hili sawa na asilimia arubaini (40%) Mtunzi Bosco Mulwa katika wimbo wa *Mother* (Mama), amemsawiri mama kama aliye mlezi mwema wa watoto katika ubeti huu:

| | |
|---|---|
| *Wanzyaie ni munini sana Susana* | Ulinizaa nikiwa mchanga sana, Susana |
| *Wandea nginya neana.* | Ukanilea hadi nikakomaa. |
| *Wendo wa musyai Sheri mother ndwaambata* | Mapenzi ya mzazi hukuninyima |

*Mother ii mother ii nouwe mwendwa wakwa*.        Utasalia kuwa kipenzi changu mama

Ubeti huu unamuonyesha Mama kama aliye na uwezo wa kulea watoto na kuwakuza hadi wakakomaa. Mapenzi yake ya dhati kamwe hawanyimi watoto wake. Maelezo haya yanaonyesha mama kama mlezi mwema. Nafasi hii ndiyo anayozunguka nayo mwanamke kila anapokwenda. Kwa kuwa mwanamke ni mama, huwa ni mlezi, mwelekezi katika maisha ya watoto na jamii kwa jumla. Jamii ya Wakamba tangu jadi hadi sasa humtambua mwanamke kama mlezi wa familia na ndiyo maana alipewa jukumu la kulima shamba la ukoo lililojulikana kama shamba la *ng'undu*.

Shamba hili ni sehemu ya urithi wa mume wake kutoka kwa wazazi. Mwanamke haruhusiwi kuuza shamba hili. Yeye hukuza vyakula mbalimbali ili kulisha familia yake. Iwapo mume wake atafariki, mwanamke husalia katika kipande hiki cha shamba na kuendeleza kizazi cha mume wake.

Miongoni mwa jamii ya Wakamba, wanawake walitwikwa majukumu mengi kuliko wanaume. Wao ndio hugawiwa kazi nyingi. Wanaume hutekeleza majukumu kama ujenzi wa nyumba, kuchunga mifugo na majukumu mengine kama  kulima. Wanawake nao huezeka nyumba kwa nyasi, hupanda, huwinga ndege, huvuna na kuhifadhi mazao hayo. Vile vile wao ndio hukama ng'ombe. Kazi za nyumbani kama kupika, kulea watoto ni majukumu ya wanawake katika jamii ya Wakamba (King'ei, 1982). Kwa hivyo, ni wajibu wa wanajamii kutambua majukumu muhimu ya mwanamke na kumheshimu kama kiumbe ajiwezaye.

Mwanamke kama mama hupewa lugha ambayo inamsifia katika nafasi hiyo ambayo ni tofauti na jinsi ambavyo amechorwa katika nafasi nyingine. Mwanamke kuitwa mama kunampa sifa ya kipekee ambayo wanajamii wanaitambua. Jamii huwa na matarajio makubwa kwake. Ama kwa

hakika ‘ukipata radhi ya mama, uko katika salama.’ Mama kwa kuilea familia yake na jamii kwa jumla anakuwa dira ya kumwangazia mwanadamu maishani.Kwa kutumia misingi ya dini ya Kikristo, mwanamke anastahili kuwajibikia familia yake kama asemavyo Mfalme Solomoni katika kitabu cha Methali (31: 10-15);

> Ni nani anayeweza kumpata mke mwema? Thamani yake inazidi kabisa thamani ya majirani.Mume wake humwamini kutoka moyoni, na mume huyu hakosi chochote chenye thamani.Humthawabisha mume wake kwa wema, wala si kwa mabaya. Siku zote za maisha yake.Hujipatia sufu na kitani; hufurahia kufanya kazi kwa mikono yake.Yeye ni kama meli za mfanyabiashara, huleta chakula kutoka mbali. Yeye huamka kabla ya mapambazuko, na kuwaandalia chakula watu wa nyumbani mwake.

Dini inampa mwanamke sifa nzuri, amesawiriwa kama mchapa kazi kwa mikono yake, huamka kabla ya mapambazuko kwenda kutafutia familia yake. Mwanamke huyu amefananishwa na meli kwa sababu meli ya biashara hubeba bidhaa mbalimbali ndani yake. Mwanamke amebeba majukumu mengi sana katika maisha yake, kwa mfano ni mzazi, mlezi, mshauri miongoni mwa mengine. Kwa hivyo, mwanamke anao uwezo wa kutekeleza malezi ya familia yake.

Justus Myello katika wimbo wa *Aka* (wanawake) amemsawiri mwanamke kama mlezi mwema anapoelezea majukumu ya kimsingi ya mwanamke. Katika jamii tunaona kuwa mwanamke ndiye mwenye jukumu kubwa la ulezi. Katika malezi hayo mwanamke huweza kuelimisha watoto anaowalea, kutoa ushauri, kuadilisha, kuwa na upendo, kuonya na kuwa na mapenzi ya dhati kwa watoto hao. Mtunzi huyu anadhihirisha haya kupitia maelezo yafuatayo:

*Maisye makithi nguni na mbisu yi iko*
*Usini kiwu no kuuta na indo nowe ukuthasya,*
*Syana syetana mami nowe ikwenda,*
*Kitanda nowe ukalany'a na kusuvia musee.*
*Andu aa mukwona maithasya syana na yiia ya nondo.*

Wanawake hutekeleza majukumu mengi
Kuchanja kuni, kupika, kuchota maji
Kuchunga mifugo pamoja na kutunza familia.
Watu wawa hawa wanaowalea watoto kwa maziwa yao.

Katika ubeti huu, mwanamke amesawiriwa kama aliye na uwezo wa kulea watoto na jamii nzima kwa jumla. Anaonekana mwenye kushughulikia familia yake kupitia majukumu mengi, anachota maji na pia kutafuta kuni. Maelezo haya yanaonyesha kuwa mwanamke ndiye anahusika na mambo ya kuipikia familia yake. Watoto wanamlilia mama, dhihirisho tosha kuonyesha kuwa malezi ya watoto huegemezwa kwa mwanamke.

Msanii huyu anazidi kusifia malezi ya mama anapoelezea jinsi mama alivyovumilia uchungu wa uzazi. Akambeba tumboni mwake kwa muda wa miezi tisa tamima akiwa hajui ni kiumbe cha aina gani alichohimili. Hatimaye mama alimzaa na kumlea. Alimkinga dhidi ya magonjwa hatari ya utotoni kama vile, kupoonza na kuota kwa meno. Anayaeleza haya kupitia ubeti huu:

*Miei kenda ukangua utesi niilye ata,*
*Kwaunya na woo mwingi, kuzyaa na kundea.*
*Mauau me itai ta ini, kiumati, kung'ang'athuka*
*Othe ndesi wanzuvia wendo waku wi mwanya.*

Miezi tisa tamima ukanibeba tumboni
Hukujua mimi ni kiumbe za aina gani
Hatimaye ukanizaa,
Ulinikinga dhidi ya magonjwa ya utotoni,
Hakika mama mapenzi yako ni ya kiaina.

Ubeti huu umemsawiri mwanamke kama mwenye kuwanyonyesha watoto kwa maziwa yake mwenyewe. Hivyo yeye ni mhimili mkubwa wa familia kwa jumla. Kwa mfano, jukumu la kumtunza mume wake. Jamii ya Wakamba, kama zilivyo jamii nyingi za Kiafrika, ni jukumu la mwanamke kumtunza mume wake. Anastahili kumvisha, kumlisha na pia kumtimizia haja za

kimsingi katika ndoa. Majukumu haya humpa mwanamke thamani kubwa na kumfanya aheshimiwe na jamii.

Msanii Justus Myello anawasifia wanawake kwa jumla kutokana na mambo mengi wanayotekeleza katika jamii. Anasema wanawake hawa mnaowaona ni watu wa kuthaminiwa sana katika jamii. Anadhihirisha haya kupitia ubeti huu:

| | |
|---|---|
| *Adu aa mukwona meiyova suka na ikoi* | Watu hawa wanaojifunga lesa na vikoi, |
| *Nandu ma vata muno thayuni wa kila mundu,* | Ni muhimu katika maisha ya kila mtu, |
| *Aka me utonyi mwingi na vinya wa ika maundu manene,* | Wanawake wana uwezo mkubwa wa kufanya makuu, |
| *Keka maikwo nthi ino maundu makita kuema,* | Kama wasingekuwa katika dunia hii mambo mengi yasingewezekana, |
| *Tutonya kumane ki, tumakunie moko na ngemi,* | Tuwape nini ila kuwapongeza. Pongezi mama wewe ni mtu wa thamani kubwa katika dunia hii. |
| *Pongezi we mami mwaitu wi mundu wa vata nthi ino.* | |

Kupitia ubeti huu, Myello anasema kuwa, hawa wanawake wanaojifunga leso na vilemba ni watu wa thamani kuu katika maisha ya kila mtu. Wanawake wanaelezwa kama watu walio na uwezo wa kufanya mambo mengi. Kulingana na mtunzi wa wimbo huu, wanawake wasingekuwa, ingekuwa vigumu sana kutekeleza majukumu mengi katika dunia hii. Anajiuliza ni kipi cha kuwapa wanawake. Anawahimiza watu kuwathamini wanawake kwa kuwapongeza na kuwashangilia.

Msanii wa wimbo *Nyinya wa Ndetei* (Mamake Ndetei) amemsawiri mwanamke kama mlezi wa watoto, haya anayaonyesha kupitia mhusika mkuu ambaye ni mke wake aliyemtambua kama Mama Ndetei. Mama wa Ndetei alipomtaliki mume wake aliamua kwenda na watoto wake ambao ni Ndetei, Nthiwa na mtoto mwingine mchanga. Mwanamke huyu anawakilisha wanawake ambao wako tayari kuwalea watoto wao minghairi ya waume wao. Mume wake

anamrai arudi nyumbani, kwa kumweleza kuwa ni yeye tu anayemthamini. Maelezo haya yanaonyesha kuwa, mwanamume ameanza kutambua ule uwezo wa mwanamke kwani pindi tu anapoondoka anaacha pengo kubwa pale nyumbani. Anayasema hayo kupitia ubeti huu:

*Nyinya wa syana ni ivityo yau yu nyie nakwikie, kuma wathi ona kavalua ndunandikia, nakwikie ata mama, ko ve nai itaekeawa*.

Mama watoto ni kosa gani nililokukosea, tangu uende kwenu hata barua hunitumii, nilikufanyia nini, kwani kuna dhambi isiyosamehewa?

*Nyinya wa Ndetei, nyinya wa Nthiwa Mami wa Koreta,*
*Kethya Ndetei vamwe na Nthiwa na kana Kala kaitu kanini ka nondo,*
*Na nyinya wa syana uitata na vinya usyoke musyi*

Mama Ndetei, mama Nthiwa mama Koreta, Salimia Ndetei,
Nthiwa na yule mtoto wetu Mchanga.
Mama watoto jaribu uwezavyo urudi nyumbani.

Ubeti huu unaelezea kuwa jinsi mama watoto alivyokatiza mawasiliano yake na mume wake. Mume wake anataka kujua kosa alilomkosea. Kule kuachwa peke yake kunampa ukiwa ndiposa anamwambia mke wake awasalimie watoto wote. Anamrai arudi nyumbani. Taswira inayojitokeza hapa ni kuwa jamii huwa na matarajio maalum kwa mwanamke yeyote anayeolewa. Jambo hili ndilo linalosababisha mwanamume kuhisi lile pengo aliloacha mke wake. Bado anamtaka awe karibu naye.

Katika jamii ya Wakamba, mwanamke aliyetoka kwenye ndoa yake na kurudi kwao huitwa *mwinzioka*. Zamani suala la mwanamke kurudi kwa wazazi wake lilikuwa adimu. Hili lilisababishwa na aibu ambayo ilisemekana angeiletea familia yao kwa kuwa alilipiwa mahari. Siku hizi mambo yamebadilika, wanawake wengi wanapochoshwa na ndoa, wao hurudi kwao.

Wengine huenda kwenye miji mikubwa kujitafutia riziki angalau kuwatunza watoto wao. Mama Ndetei anawakilisha wale wanawake ambao wamekataa kufungwa na minyororo ya ndoa.

Suala hili la mwanamke kupewa talaka linastahili liwe na makubaliano kati ya mume na mke. Mara nyingi watoto wanapoondoka na mama yao na kurundi alikozaliwa, watoto hawa hukumbana na changamoto si haba. Hata kama anayeomba talaka anaweza kuwa na machungu ni vyema waelewane juu ya suala la watoto. Mtafiti ameona kuwa talaka sio suluhisho la migogoro inayotokea katika familia kwani watoto wakati mwingine hujipata katika njia panda. Kama wanandoa watakosa kabisa kukubaliana kuhusu yanayowakumba basi itakuwa ni vyema wakubaliane kutalikiana bila kumdhulumu yeyote.

Msanii John Muasa katika wimbo wa Syoka Mami (Rudi Mama) anamrai mama mzazi kurudi nyumbani. Anatambua pengo lililoachwa na mama pale nyumbani tangu aondoke.Anadhihirisha haya kupitia ubeti huu:

*Mami niki watwathukiie,*
*Mami niki watwathukiie,*
*Nengi noue watusyaie,*
*Niki watutiie na ndati wathi uendo,*
*Uka mami nitukumisi,*
*Ona ethiwa makosa wianya mavuti,*
*Uka tuyita ungi mwaitu,*

Mama kwa nini ulitutelekeza,
Mama ni wewe uliyetuzaa,
Mbona ukatuacha na baba ukaenda,
Rudi mama hata kama ulitukosea,
Hatuwezi kumwiita mwingine mama.

Maelezo ya mtunzi huyu yanaonyesha kuwa mama ni mlezi wa familia kwani anahisi kuna pengo kubwa katika familia yao hata kama wanaishi na baba mzazi. Anamwambia mama kuwa wanampenda huku akimrai arudi nyumbani. Anayofanya mama pale nyumbani yanakuwa mengi ijapokuwa hakuna anayetambua. Anapoyaondokea majukumu hayo, ndipo familia hutambua pengo analoliacha mwanamke.

Mwanamke amesawiriwa kama kiumbe muhimu katika malezi ya watoto na familia kwa jumla. Kwa kuzingatia Ufeministi wa Kiafrika, lengo ni kuwahamasisha wanawake wawe mstari wa mbele kuwajibikia majukumu yao. Hili linathibitisha nadharia hii inasisitiza kila mmoja awe mstari wa mbele kusimamia majukumu yake ipasavyo na asiwabebeshe mzigo wengine.

### 4.4.6 Mwanamke Kama Mwenye Mapenzi ya Dhati

Mapenzi ya dhati ni miongoni mwa raslimali adhimu na iliyotukuka katika kuijenga familia na jamii nzima kwa jumla. Mapenzi ya dhati hasa katika ndoa huimarisha masikilizano, uaminifu, heshima na uadilifu kwa wahusika. Katika uchunguzi huu, imebainika kuwa suala la mapenzi ya dhati linajitokeza katika nyimbo za sifo za Wakamba. Nyimbo tatu (3) zimegusia suala hili ambayo ni sawa na asilimia thelathini (30%).

Mtunzi Bosco Mulwa katika kulijadili suala hili kupitia kwa wimbo wa *Mother* (Mama) amemtumia mhusika mama. Mama anaonekana mwenye mapenzi ya dhati kwa mtoto wake. Anamzaa na kumlea mtoto tangu akiwa mchanga hadi akawa mkubwa. Anayaeleza haya kupitia ubeti huu:

| | |
|---|---|
| *Mother ii mother mwa ndikolya nue,* | Mama ewe mama sitawahi kukusahau, |
| *Mother ii mother ii wazyai,* | Mama ewe mama ulinizaa, |
| *Wanzyaie ni munini sana mother Susana,* | Ulinizaa nikiwa ndogo sana Susana, |
| *Wandea nginya neana,* | Ukanilea kikakomaa, |
| *Wendo wa musyai sweet mother twaambata,* | Mapenzi ya mzazi mpenzi mama hukuninyima, |
| *Mother ii Ngai akuathimae wi wakwa.* | Mama ewe mama Mungu akujalie mema, |

Ubeti huu anaeleza vile mama alivyomtunza mtoto wake tangu utotoni na kamwe hakumnyima mapenzi ya mzazi. Mtoto anamwambia mama kuwa, kamwe hatawahi kumsahau. Wanawake katika jamii ya Wakamba huonyesha mapenzi ya dhati kwa watoto wao kupitia njia mbalimbali, kwa mfano asubuhi na mapema wao huandamana na watoto wao kuhakikisha wamefika shuleni

salama. Mwendo wa adhuhuri wao ndio huonekana kuwaletea watoto chakula. Wengine huwaeleka watoto wao migongoni, ishara kuwa wanawajali.

Katika wimbo wa *Kana Nzula* (Mpenzi Nzula), msanii anamchora msichana Nzula kama aliyekuwa na mapenzi ya dhati kwa mchumba wake. Anaelezea kuwa baada ya Nzula kuhitimu masomo yake alienda ughaibuni kujiendeleza kimasomo. Baada ya masomo, alirudi nyumbani kwa mpenzi wake, hakubadili uamuzi wake. Mpenzi wake anamwambia Nzula kuwa alihofia kuwa angeolewa na mzungu. Nzula alikuwa ameamua kuolewa na mchumba wake, kwani alikuwa anampenda. Anayaeleza haya kupitia ubeti huu:

| | |
|---|---|
| *Niwikite nesa kunzyokea we Nzula,*<br>*Niwikite nesa kunzyokea we Nzula,*<br>*Nitwie thinani utaweteka Nzula,*<br>*Nitwie thinani utaweteka Mzula,*<br>*Ngw'eteele Nzula, umine masomo mwendwa,*<br>*Nge'eteele Nzula, umine masomo mwendwa* | Umefanya vyema kunirudia Nzula,<br>Umefanya vyema kunirudia Nzula,<br>Nilikuwa nikuhuzunika moyoni,<br>Huku nikusubiri urudi mpenzi,<br>Nikikusubiri ukamilishe masomo mpenzi, |
| *Ninai na wia niwisa utwawa ni musungu,*<br>*Ninai na wia ndukatwawe ni musungu*<br>*Uka Nzula kana nivata naku,*<br>*Uka Nzula mwiitu wa Musomba.* | Nilikuwa nikihofia ungeolewa na Mzungu,<br>Njoo mpenzi nakupenda.<br>Njoo Nzula binti Musomba |

Mpenzi wake anamwambia Nzula amefanya vizuri kumrudia. Anazidi kumweleza kuwa, alikuwa akiwaza juu yake huku akimsubiri arudi. Moyoni alikuwa na hofu kubwa Nzula angepata mchumba mwingine. Nzula ni kiwakilishi cha wanawake wenye mapenzi ya dhati kwani ni wengi hutengana na waume ama wachumba wao kwa sababu mbalimbali kama vile: kazi, masomo, magonjwa, kufungwa jela miomgoni mwa njia nyingine na wakirudi hupata wamebadili nia.

Justus Myello katika wimbo wa *Aka* (Wanawake) ameonyesha mapenzi ya dhati. Vile vile amemsawiri mwanamke kama kiumbe mwenye mapenzi ya dhati anapomwambia kuwa mapenzi yake ni ya kiaina. Anadhihirisha haya anaposema

| | |
|---|---|
| *Mowau me itai ta ini,* | Magonjwa sugu ya utotoni, |
| *Kiumati, kung'ang'athuka,* | Mama ulinikinga hata bila kujua, |
| *Monthe ndesi wanzuvia, wendo waku wi mwanya* | Hakika mapenzi yako ni ya Kiaina |

Msanii huyu anasema mapenzi ya mama ni ya kipekee, anayaona kuwa hayamithilishwi na kitu kingine. Anaelezea jinsi mama alivyomtunza akiwa mchanga pamoja na kumkinga dhidi ya magonjwa hatari ya utotoni. Jambo hili linaonyesha kuwa msanii huyu anayaegemeza maisha yake kwa mwanamke. Anamwambia mapenzi yake ni ya kweli.

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inatetea umuhimu wa kuwa na mapenzi ya dhati ili kuweza kujenga jamii iliyo bora na kuepukana na ubaguzi na udhalilishaji. Mapenzi ya dhati husaidia kujenga familia bora na yenye kushirikiana ili kuleta tija katika jamii. Jamii za Kiafrika, ikiwemo jamii ya Wakamba, huhimizwa kulizingatia suala la mapenzi ya dhati. Jambo hili husaidia kuleta uelewano katika maisha ya kila siku kwa kila mwanadamu.

**Jedwali (i):** Nyimbo zenye usawiri wenye sifa chanya

| **Namba** | **Usawiri wa sifa chanya** | **Wimbo** | **Jumla** | **Mtunzi** |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mwanamke kama mchumi | *Aka me vata* | *1* | *Justus Myelo* |
| 2 | Mwanamke kama | *Aka me vata* | *2* | *Justus Myelo* |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | muwajibikaji | *Mother* | | *Bosco Mulwa* |
| 3 | Mwanamke kama mshauri mwema | *Aka nima mithemba* | *2* | *Wanginga* |
| | | *Mother* | | *Bosco Mulwa* |
| 4 | Mwanamke kama mkombozi | *Nyinya wa Ndetei* | *4* | *Kijana Mumo* |
| | | *Syoka Mami* | | *John Muasa* |
| | | *Aka me vata* | | *Justus Myelo* |
| | | *Mother* | | *Bosco Mulwa* |
| 5 | Mwanamke kama mlezi wa familia | *Nyinya wa Ndetei* | *4* | *Kijana Mumo* |
| | | *Syoka Mami* | | *John Muasa* |
| | | *Aka me vata* | | *Justus Myelo* |
| | | *Mother* | | *Bosco Mulwa* |
| 6 | Mwanamke kama mwenye mapenzi ya dhati | *Kana Nzula* | *3* | *Bosco Mulwa* |
| | | *Aka me vata* | | *Justus Myelo* |
| | | *Mother* | | *Bosco Mulwa* |

Kulingana na jedwali hili, wasanii hawa wa nyimbo hizi za sifo za Wakamba wamemsawiri mwanamke vyema kwa kumpa sifa chanya. Wamemjenga na kumthaminisha. Kupitia sifa zote chanya walizompa, nafasi za mwanamke kama mkombozi na mlezi wa familia ndizo zimepewa kipaumbele na wasanii wengi. Mwanamke kama muwajibikaji imechangiwa na watunzi wawili tu. Msanii Bosco Mulwa amemsawiri mwanamke kwa kumpa sifa zote chanya. Mwanamke amepewa sifa ya mchuma mali, jambo ambalo linaonyesha jamii imeanza kutambua mchango

wa mwanamke katika jamii. Kulingana na usawiri huu ni kwamba kunao wanaume ambao hutambua mchango wa mwanamke katika jamii. Bosco Mulwa na Justus Myello wamemthaminisha mwanamke kwa kumpa sifa chanya kwa asilimia za juu.

Katika uhalisia wa maisha mwanamke ni kiumbe razini kama alivyo mwanamume. Kupitia usawiri mwema, mwanamke anaweza kufanya mengi katika jamii na kujijenga kimaisha pamoja na jamii nzima kwa jumla. Ni vyema kila mwanajamii kuwajibikia nafasi yake katika jamii pasi kudhalilisha jinsia yeyote. Hata kama kuna dhana kuwa, mwanamume ndiye huchangia katika kumdhalilisha mwanamke, kulingana na usawiri huu ni bayana kuwa kunao wanaume ambao hutambua mchango wa mwanamke katika jamii.

**Jedwali (ii):** Kuonyesha kiwango cha sifa chanya kwa mujibu wa watunzi

| **Mtunzi** | **Jumla** | **Sifa kwa asilimia** |
|---|---|---|
| Bosco Mulwa | 6 | 60% |
| Justus Myelo | 5 | 50% |
| Kijana Mumo | 2 | 20% |
| Wanginga | 1 | 10% |
| John Muasa | 2 | 20% |

Kulingana na jedwali hili msanii Bosco Mulwa amemsawili mwanamke kwa sifa chanya kwa kiwango cha juu cha asilimia sitini (60%) Wanginga na John Muasa wamemsawili kwa asilimia ya kiwango cha chini cha asilimia ishirini (20%). Justus Myello kiwango cha asilimia hamsini (50%) na Kijana Mumo asilimia ishirini (20%). Kulingana na kiwango hiki ambacho ni tofauti ni wazi kuwa, baadhi ya wanaume hutambua uwezo wa mwanamke wa kufanya mengi makuu ilhali

wengine wanatambua kwa kiwango cha chini. Kila mmoja anastahili kutambua uwezo alionao mwanamke katika jamii. Msanii Justus Myello ameeleza bayana kuwa, kama mwanamke asingekuwa duniani humu mambo mengi yangekuwa vigumu kuyatekeleza.

## 4.5 USAWIRI HASI WA MWANAMKE

Watunzi wa nyimbo hizi wamefaulu kubainisha sifa dhalilishi na ya kudunisha anamowekwa mwanamke na jamii inayomwenzi na kumkweza mwanamume. Haya yanatokana na yale yanayosemwa au anayotendewa mwanamke katika jamii. Mtafiti ameainisha usawiri hasi ifuatavyo:

### 4.5.1 Mwanamke Kama Mshirikina

Dhana ya uchawi imejitokeza katika data alizozikusanya mtafiti. Mtafiti amegudua kuwa nyimbo mbili zimeonyesha nafasi hii. Wimbo wa Kakai Kilonzo *Kiveti ngungu* (Mwanamke tasa), *Aka ma taoni* (Wanawake wa mjini) na Nyinya wa Ndetei (Mama Ndetei). Kiwango hiki ni sawa na asilimia thelathini (30%). Katika wimbo wa Mwanamke tasa, mwanamke tasa amemithilishwa na mchawi. Mchawi ameelezewa kama mtu asiyetakia wengine mazuri. Suala la utasa katika jamii ya Wakamba huchukuliwa kwa uzito sana.

Mchawi katika jamii ya Wakamba huogopwa kwa kuwa hudhaniwa huleta maafa katika jamii. Dhana ya uchawi katika jamii ya leo ya Wakamba si ngeni. Wote wanawake kwa wanaume wanaweza kuwa wachawi. Linaloingia masikioni mwa wanajamii sana, hasa katika jamii ya Wakamba ni kuwa mwanamke ndiye mchawi. Makali ya uchawi katika jamii ya Wakamba huaminiwa kupunguzwa kwa kushiriki aina ya kiapo kinachojulikana kama *ndundu*. Anayeshiriki kiapo hiki huwa hawezi kuwadhuru wanajamii kwa uchawi wake. Mtunzi Kakai Kilonzo ameonyesha haya kupitia maelezo yafuatayo:

| | |
|---|---|
| *Kiveti ngungu na muoi me nduu,*<br>*Na nundu nandu matendete umesye kindu,*<br>*Muoi ndendete kwona kindu kiseo,*<br>*Onetha ni alusi we okaa kwananga,*<br>*Onethiwa wina ngali euvoyea uvaluke*. | Mwanamke tasa na mchawi wana uwiano,<br>Ni watu wasiotakia wengine mema,<br>Mchawi ni mtu mwenye wivu,<br>Ukiwa na arusi anakutakia mabaya,<br>Ukinunua gari anakuombea ajali. |

Ubeti huu unaeleza kuwa, mwanamke tasa na mchawi wana uwiano, na ni watu wasiowatakia wengine mema. Unaendelea kueleza kuwa, mchawi hafurahii kuwaona wengine wakiendelea vyema, ukiwa na arusi, kusudi lake ni kuivuruga. Yeyote akinunua gari, yeye humwombea ajali.

Nafasi hii chukivu anamowekwa mwanamke ni baadhi ya dhana zinazomtweza na kumdhalilisha mwanamke. Kuwa tasa sio lazima uwe mchawi. Uchunguzi umebaini kwamba, suala la utasa limewaathiri wanawake wengi, ikibainika kuwa utasa ni jambo ambalo husababishwa na matukio mbalimbali ya kibayolojia. Kwa mujibu wa Sayansi, mwanamume anaweza kuwa na kasoro na kumfanya mwanamke asiwe na uwezo wa kuhimili mimba. Ni vyema wanajamii kuelimishwa kuhusu vinavyosababisha utasa, wasije kuwalimbikizia uchawi wanawake wasioweza kuzaa, kama vile alivyowasawiri wanawake katika wimbo huu. Wanajamii wengi wamepata madhara makubwa katika maisha yao kutokana na kukosa elimu ya kutosha. Ndoa nyingi zimevunjika kwa sababu ya kulimbikiziana lawama kuhusu suala la utasa kuchangiwa na uchawi. Pindi jambo hili linapotokea katika familia, mara nyingi mwanamke hulazimika kurudi kwao.

Dan Mutuku amegusia suala la ushirikina katika wimbo wa *Aka ma taoni* (Wanawake wa mjini). Anaelezea jinsi wanawake wa mjini wanavyothamini pesa kiasi cha kwenda kutazamia kwa waganga ili kupata pesa. Anadhihirisha haya kupitia ubeti huu:

| | |
|---|---|
| *Aka aa ukwona taoni,*<br>*Makua ndumba kali na maendaa kwa awe*<br>*Mayosa ndumba sya wendo.* | Wanawake hawa wa mjini ni washirikina<br>Wao huenda kutazamia kwa waganga,<br>Kuwapumbaza wanaume wasahau majukumu |

| | |
|---|---|
| *Ukunzwe ukethia ndwinuka* | yao |

Mtunzi katika ubeti huu amewasawiri wanawake wa mjini kama washirikina kwa sababu wao hubeba hirizi ndiposa waweze kuwapumbaza wanaume. Wanaume hawa ni wale pengine, utapata wana wake zao nyumbani. Wanapojihusisha na wananawake wa mjini wanaotumia ushirikina wanasahau majukumu yao. Wanatelekeza familia zao. Wanawake wamepewa sifa chukivu ya uchawi bila kuchunguza kuwa labda wale wanaume ndio huenda kupiga ramli kwa waganga ili waweze kupendwa na wanawake wale wa mjini. Maelezo ya msanii huyu yanaonyesha kuwa, mwanamume ndiye humpa mwanamke pesa. Kiuchumi mwanamke anaonekana kuwa katika nafasi ya pili kwani yeye anaonekana kutafuta pesa kupitia njia hii duni. Wanawake wakipewa nafasi sawa za kiuchumi kama wanaume, watafanya mambo yao bila kuwategemea wanamume kwa msaada. Baadhi ya vitendo hivi vyenye uozo kama vile ushirikina vitapungua katika jamii.

Uchawi pia unajitokeza katika wimbo wa Nyinya wa Ndetei (Mama Ndetei). Wimbo huu alipoondoka nyumbani mke wake, alidhani kuwa labda mapenzi yao yalikuwa yameingiliwa na mchawi. Anasema hivi katika ubeti huu:

| | |
|---|---|
| *Nyinya wa Ndetei, nyinya wa Nthiwa, mami wa Koreta, Nyinya wa Ndetei ,nyinya wa Nthiwa, ,*<br>*Wendo witu mwa kuwonekie ni amaitha*<br>*Na metho moo matunivite ta mwaki,*<br>*Ni vandu vooo Mwiai akasila,*<br>*Koti itesi mbesa kana kimanyanyo,* | Mama Ndetei, mama Thiwa, mama Koreta,<br>Mapenzi yetu kwani yaliharibiwa na wachawi ,<br>Na macho yao mekundu kama moto,<br>Shauri yao Mungu atawahukumu,<br>Katika mahakama isiyojua pesa ama uhusiano |

Msanii huyu anamini kuwa waliochochea talaka walikuwa wachawi. Anaeleza kuwa macho yao ni mekundu kama moto. Uchawi huu anauhusishwa na wale wanawake wenye kuvunja ndoa za

wengine. Ndio ndiyo sababu anasema Mungu ndiye atakaye wahukumu katika mahakama yake isiyojua pesa ama urafiki. Dhana hii ni potofu kwa sababu mwanamke anapokumbana na changamoto katika ndoa yake na kupanga kuondoka, si lazima kuondoka kwake kuchangiwe na uchawi.

Mtafiti kupitia kwa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika amegundua kuwa nadharia hii imeendeleza kutoa msisitizo kwamba matendo maovu si hazina. Haya ni kutokana na mhimili unaonuia kuzindua mwamko kwa upande wa wanawake jinsi wanavyojiona na uhusiano wao na wa watu wengine. Wanawake wana nafasi kubwa katika kuhamasisha kuhusu maendeleo yao na jamii kwa jumla ikiwa ni pamoja na kukemea na kuachana na tabia ya mambo ya ushirikina inayoweza kuleta madhara katika maisha yao na taifa kwa jumla. Nadharia hii inawataka wanawake wajitambue na wasiwe tayari kujiingiza katika dhambi kama hizi.

### 4.5.2 Mwanamke Kama Asherati

Uasherati unadhihirika kama ukosefu wa maadili miongoni mwa wanajamii na ambao unajadiliwa na watunzi wa nyimbo hizi za sifo za Wakamba. Katika hali ya kawaida ya jamii nyingi za Kiafrika, uasherati ni kitendo kinachoshusha hadhi ya mwanamke.

Tabia hii inaendelea kushika kasi katika jamii mbalimbali za Kiafrika na dunia nzima kwa jumla. Jambo hili linaweza kusababisha kuenea kwa maradhi mbalimbali hatari yakiwemo yale ya UKIMWI. Data alizozikusanya mtafiti, zimeonyesha kuwa nafasi hii ya uasherati imejitokeza katika nyimbo tatu (3) kwa kumi za watunzi wa nyimbo hizi za sifo za Wakamba ambazo ni sawa na asilimia thelathini (30%).

Wimbo wa *Aka ma taoni* (Wanawake wa mjini), wa Dan Mutuku unaonyesha msanii huyu akisikitishwa sana na wanawake wa mjini kufanya biashara ya ngono. Anaeleza vile wanawake wa mjini wanavyoshiriki kitendo hiki cha uasherati ndiposa wapate pesa. Wanawake hawa wamesawiriwa kama wenye tamaa ya pesa. Ubeti huu uaeleza haya:

| | |
|---|---|
| *Dan mwa ninguseng’a, ni aka ma taoni,* | Dan nashangazwa sana na wanawake wa mjini, |
| *Dan mwa ninguseng’wa ni aka mataoni,* | Dan nashangazwa sana na wanawake wa mjini, |
| *Mwa mendete muno mbesa yutia yila ya aume,* | Wao huthamini sana pesa, jasho la wanaume, |
| *Mwa mendete muno mbesa yutia yila ya aume* | Wao huthamini sana pesa, jasho la wanaume |

Wimbo huu umeonyesha kuwa baadhi ya wanawake huuza miili yao ili kukidhi mahitaji yao. Hali hii ya kukidhi mahitaji kwa sasa imekuwa kisingizio kikubwa kwa wanawake walio wengi (Fakih, 2017). Fakih anaelezea kwamba, biashara ya danguro na ukahaba ni tabia mbaya inayowafanya baadhi ya wanawake kujishughulisha katika kuuza miili yao kwa wanaume ili kukidhi mahitaji yao. Tabia hii kwa kawaida inaleta athari za kiafya, sio tu kwa mwanamke peke yake bali pia kwa mwanamume. Ni vyema kwa wanajamii kuachana na tabia za aina hii na mwanamke mwenyewe kutambua thamani yake na kutokuwa tayari kutumika kama bidhaa kwa wanaume.

Mwanamke anastahili kujua kuwa hata kama nyakati za maisha ni ngumu, kuna njia mbadala mbalimbali za kujikimu kimaisha kama vila ususi, ushoni, kilimo na hata mamantilie. Kujihusisha na kitendo cha ngono siyo suluhisho la hali ngumu ya maisha. Wakiona mwanamume na pesa, wao hutafuta mbinu zozote ili waweza kuzichukua na wanaume wakifilisika wao hutoroka. Mtunzi huyu anawatahadharisha wanaume kujiepusha na wanawake wa aina hii kupitia ubeti huu:

| | |
|---|---|
| *Woosana na Malaya, ndukalumya mbesa syaku* | Ukijihusisha na malaya, utafilisika |

| | |
|---|---|
| *Na kwikya mbesa neulu ni makosa ni kiumo.* | Na kufuja pesa ni hatia na ni laana. |

Maneno ya mtunzi huyu, yanaonekana kumpa mwanamke sifa ya umalaya. Anawaambia wanaume kuwa, wakijihusisha na malaya hawataweza kutunza pesa zao. Dhana ya kwamba mwanamke ni kiumbe malaya si ngeni katika ulimwengu wa fasihi na katika masikio ya watu katika ulimwengu halisi. Lazima ifike mahali jamii itambue kwamba, suala la umalaya si la mwanamke peke yake bali ni la watu wote, wakiwemo wanaume na wanawake. *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004:310) inaeleza ' malaya' kuwa ni mwanamke au mwanaume mwenye tabia ya uzinzi. Kulingana na maelezo haya, ni sahihi kusema kwamba, wanawake na wanaume wanashiriki ukahaba kwa kuwa kitendo hicho huhitaji ushirikiano wao wote. Wanawake kupitia wimbo huu wamepewa nafasi hii dhalilishi kwa kuitwa malaya.

Msanii huyu, hakuonyesha kuwa ukahaba anaosema hapa unaendeshwa na mwanamke pekee. Tukiangalia kwa ndani, uchochezi wa tendo la ngono linalosababisha umalaya si la mwanamke peke yake, bali wote wawili, yaani mwanamke na mwanaume. Kupitia ubeti huu anaeleza haya:

| | |
|---|---|
| *Mo masyaa ila ndia imbiie nikuka ingi,* | Wao husema yule mjinga aliniahidi kuwa |
| *Mo masyaa ila ndia imbie nikuka ingi,* | Atarudi tena, |
| *Vata wakwa ni mbesa yavika ningumywony'a.* | Haja yangu ni pesa akija nitamuonyesha. |

Kulingana na maelezo haya, mwanamume ndiye hugharamia tendo la ngono kwa kumlipa mwanamke. Mwanamke anasema haja yake ni pesa. Mwanamke ametumika katika tendo hili kwa lengo la kujipatia fedha na tamaa. Mwanamke anaonekana ni kiumbe mwenye kupata starehe kwa gharama za mwanamume. Katika hali halisi mwanamke ndiye ambaye hutajwa kuwa ni malaya hali ambayo si kweli. Hii ni elementi ya mfumo dume ambapo mambo mabaya husukumiwa mwanamke hata kama yanamhusu mwanamume (Lyatuu, 2011).

Siku hizi, tunaona jinsi serikali inavyojitahidi kupambana na wanawake malaya wanaojiuza katika miji mikubwa kama vile; Nairobi, Thika, Narok, Machakos na kwingineko, lakini haifanikiwi. Hili linatokana na ukweli kuwa mwanamke anayeonekana kuwa ndiye malaya hufadhiliwa na mwanamume. Inafaa jitihada hizo ziende mbali zaidi na kumhusisha mwanamume ambaye ndiye mdau mkuu katika suala la umalaya.

Wanaufeministi wanaamini kwamba, jitihada za kukomesha vitendo vya umalaya zitafanikiwa pale tu wanaume na wanawake watakapojitambua na kuamua kubadili tabia zao. Hii itasaidia katika harakati za kukomesha tendo hili katika jamii za Wakamba na pia ulimwengu mzima.

Wimbo wa John Muasa *Syoka mami* (Rudi mama) mwanamke amesawiriwa kama mwenye tabia ya uasherati pale ambapo mama mzazi, baada ya kumtaliki mume wake alienda mjini Nairobi mtaa wa Kibera alikoonekana akiwa na mwanamume mwingine wa kupanga. Kulingana na maelezo haya, ni bayana kuwa, baada ya wanawake kujinasua kutoka kwenye ndoa zao; wao hujiingiza katika vitendo vya uasherati. Jambo hili linaweza kuchangiwa na ule 'uhuru' mwanamke anajiona kumiliki baada ya kutoka katika ndoa. Mtunzi anaeleza haya kupitia ubeti huu:

| | |
|---|---|
| *Kalungu kalungu tukewa uvumi* | Baada ya kudadidisi tukasikia uvumi kuwa, |
| *Wioneka Ilovi Kivela Kisaki* | Unaishi mjini Nairobi mtaa wa Kibera |
| *Wikalitwe ni Mwikuyu wa Maleve*. | Na mwanaume mwingine mfanyabiashara |

Mwanamke huyu, amesawiriwa kama mwanamke mwasherati kwa sababu alipoondoka kwake alienda kuishi na mwanamume mwingine. Kule kujihusisha na mwanamume mwingine kunaweza kuchangiwa na kukosa utulivu pale nyumbani kwake. Nafasi hii anayopewa, inamdhalilisha kwa sababu kilichomfanya aondoke kinaweza kuwa kilichangiwa na mume wake. Mwanamume anapoonekana na mwanamke mwingine inakuwa kosa jepesi, lakini mwanamke

kuonekana na mwanaume mwingine ni kosa kubwa. Hii ni dhana iliyo kwenye fikra za wanajamii. Wanajamii wanastahili kuelewa kuwa kosa ni kosa liwe limefanywa na mwanamke au mwanamume.

Wanawake na wanaume wanastahili kuelewa kuwa, uhusiano mwema katika ndoa unaletwa na maelewano ya wote wawili. Ni kweli kuwa fasihi kwa jumla ni kipengele cha utamaduni kinachoathiriwa na hali halisi ya maisha ya jamii husika. Mabadiliko yanayoikumba jamii kwa njia moja au nyingine hujidhihirisha katika fasihi. Jambo hili limechangia msanii John Muasa kumchora mwanamke wa aina hii. Jamii ya Wakamba ilihusika katika kumwandaa mwanajamii kulingana na mfumo wa maisha na maadili ya jamii. Siku hizi, kwa sababu ya mabadiliko mengi ya kijamii na kiuchumi, wanajamii wanaonekana kupotoka na kuasi baadhi ya tamaduni zilizowajenga.

Katika utafiti wake, Chacha (1986) alidai kuwa jamii ya mhusika Rosa katika *Rosa Mistika* ilikuwa na matatizo ya mabadiliko ya wakati na baadhi ya watu wake kama vile Mzee Zakaria hawakuweza kujimudu katika hali hiyo. Mtafiti anakubaliana na mawazo ya Chacha kwani jamii yenyewe inahitaji mageuzi ya kimsingi ili iweze kuwiana na hali halisi ya wakati uliopo. Kabla ya kutoa hukumu kuwa mwanamke ndiye mwenye makosa, ni vyema kuchunguza kiini cha jambo linalosababisha kosa hilo.

Wanginga katika wimbo wa *Aka nima mithemba* (Aina mbalimbali za wanawake) anaelezea kuhusu mwanamke aliyeitwa Nzembi mzaliwa wa mji wa Emali. Anasema kuwa alimwoa mwanamke huyu bila kujua alikuwa ‘kirukanjia’. Alijitolea kuishi naye kama mke wa ndoa lakini akawa hatulii. Alimtaliki na kuolewa na wanaume wengine ambao pia walimtaliki

walipogundua kuwa alikuwa na tabia ya uasherati. Msanii huyu anaelezea haya kupitia kifungu hiki:

| | |
|---|---|
| *Onakwo akalunywa, nundu ni uko wa usavi,* | Ata huko akafukuzwa sababu ya mbeya |
| *Na ni uko wa kitimba,* | Ni aina ya makalio, |
| *Aka mailye ta indo.* | Wanawake ni wa aina mbalimbali kama mifugo. |

Ubeti huu unamwelezea Nzembi mwanamke asiyeweza kutulia katika ndoa. Alikoolewa alikuwa akitalakiwa kwa sababu ya umbeya na uasherati. Unazidi kueleza kuwa wanawake ni wa aina mbalimbali kama walivyo mifugo.  Mwanamke kumithilishwa na mifugo ni dhana isiyostahili kwani mwanamke ni binadamu kamili kama walivyo wanaume. Kwa mawazo yetu, sio vizuri na si sahihi kumchora mwanamke katika taswira chafu kama hii. Hali hii inaushusha utu na heshima ya uwanawake.

Hymes (1974) anasisitiza kuwa, ili kung'amua maana ya maneno ni muhimu kuzingatia suala la muktadha. Katika muktadha wa wimbo huu, maneno *'uko wa kitimba'* (aina ya makalio) lina maana ya uasherati. Maana yake inaeleweka kulingana na muktadha wa wimbo. Maudhui ya nafasi hii duni aliyotengewa mwanamke wa jamii ya Wakamba yanachukuwa nafasi muhimu katika wimbo huu.

Mila na tamaduni za Wakamba hazimruhusu mwanamke aliyeolewa kujihusisha katika kitendo cha ngono nje ya ndoa yake. Mwanamume anapoenda nje ya ndoa yake suala hili halichukuliwi kwa uzito. Hili linachangiwa na mfumo wa kijamii unaomthamini sana mwanamume. Wimbo huu umemchora mwanamke kama kiumbe dhaifu kimapenzi. Wimbo huu una lengo la kumkashifu mwanamke ambaye ana tabia ya kutotulia katika ndoa yake na unaonyesha mwelekeo wa jamii ya Wakamba kuhusu wanawake ambao walichukuliwa kama viumbe duni

wasio na akili. Wanawake wamesawiriwa kama makahaba ambao wanaweza kutenda lolote la aibu bila kujali fasili ya wanajamii. Jamii inafaa kuelewa kuwa, umalaya na ufuska ni suala linaloendeshwa na wahusika wa jinsia zote mbili.

### 4.5.3 Mwanamke Kama Mwenye Tamaa

Baadhi ya wanawake wametawaliwa na tamaa. Tabia hii huiendeleza katika maisha yao bila kujali maisha yao na ya wengine na pia athari za baadaye. Msingi mzuri wa maisha ni kuwa na tabia njema ambayo inaleta faida katika familia na jamii kwa jumla. Tabia mbovu huweza kumponza mwanadamu na kumuweka katika hasara au majanga makubwa.

Data zilizokusanywa kupitia kwa nyimbo hizi za sifo za Wakamba zimedhihirisha nafasi hii. Hali hii imeonekana kupitia kwa nyimbo nne (4) zilizozitafitiwa ambazo ni sawa na asilimia arubaini (40%). Wimbo wa *'Wanawake wa mjini'* umewasawiri wanawake kama wenye tamaa ya pesa. Wanawake hawa wako tayari kushiriki kitendo chochote kile ndiposa wapate pesa. Wanataka kula jasho la wanaume, jambo ambalo limesababisha kujiingiza katika mambo ya ushirikina. Msanii huyu anaonyesha haya kupitia ubeti ufuatao:

| | |
|---|---|
| *Dan mwa ningusenga ni aka ma taoni,* | Dan nashangazwa na wanawake wa mjini, |
| *Mwa mendete mbesa,* | Wao huthamini pesa sana, |
| *Yutia yila ya aume.* | Jasho la wanaume. |

Ubeti huu unaeleza vile mtunzi anavyoshangazwa na wanawake wa mjini ambao wanathamini pesa jasho la wanaume. Wanawake wamesawiriwa kama watu wasiofanya kazi ila kusubiri kupewa pesa na wanaume. Wanawake wamedhalilishwa kwa kupewa sifa hii. Iwapo kuna wanawake wanaoshiriki tendo hili, wanastahili kutoka usingizini na kujibidiisha katika kufanya kazi kwani wakati wa sasa ni wa kuzalisha mali ili kuipa jamii mahitaji ya kimsingi.

Msanii Ancent Munyambu katika wimbo *wa Kavola Kavola Kamengele* (Pole pole Kamengele) amemsawiri mwanamke kama mwenye tamaa ya mali kiasi cha kutaka kurithi mali ya alikozaliwa licha ya kuolewa. Anarauka mapema na kuingia ghalani ili kutoa mahindi ghalani. Msanii wa wimbo huu anaeleza haya kupitia ubeti huu:

| | |
|---|---|
| *Isu ni ng'ombe mukuthinza,*<br>*Mukiya ngathi na ing'eng'eto nakwa muinenga Mavindi,*<br>*Mwinenga mavindi ko ni ngiti.*<br>*Kavola kavola Kamengele kwa nau na mwaitu Nganengwa ki.* | Hao ni ng'ombe mnaochinja,<br>Mkila minofu na kunipa mifupa.<br>Mwanipa mifupa kwani mimi ni mbwa,<br>Polepole Kamengele kwa baba na mama<br>Nitarithi nini. |

Mwanaume huyu anauliza kama hao ni ng'ombe wanaowachinja, wakila minofu, huku wazazi wake na dada zake wakimpa mifupa. Anauliza kwa nini anapewa mifupa, kwani yeye ni mbwa. Lugha inayotumiwa katika wimbo huu ni ya kimafumbo. 'Ng'ombe' katika muktadha wa wimbo huu ni kuashiria mambo yaliyo mema. Nayo 'mifupa' inaonyesha vilivyo vibaya. Msanii wa wimbo huu anaonekana kumsawiri mwanamke kama mwenye kujitakia mazuri huku akuwaachaia wengine yale yaliyo mabaya.

Mwanamke anarudi kwao kuchuma mali. Msanii anaeleza kuwa dada yake huja nyumbani kubeba mahindi. Vile vile anasema wasichana wa wale kijijini pia wao huja kwa hitaji la mahindi. Haya anayaonyesha kupitia ubeti huu:

| | |
|---|---|
| *Weew'a kungulu makumbini, isu ti mbia ikuya mbemba*<br>*Onati ngulu kana nganga,*<br>*ni mwiitu wa mwaitu ukutua mbesa,*<br>*Kavola kavola kamengele kwa nau na mwaitu Nganengwa ki.* | Ukisikia kelele ghalni, usidhani ni panya wala mahindi,<br>Wala si fukusi ama kanga,<br>Ni dada yako anachuma mali,<br>Pola pole Kamengela kwa mama na baba<br>Nitarithi nini |

Ubeti huu unaeleza kuwa, ukisikia kelele ghalani, usifikiri ni panya walao mahindi, hata si fukusi wala kanga, ni dada yangu anachuma mali. Mwanamke amesawiriwa kama mwenye tamaa ya mali. Kaka yake anajiuliza atakachorithi kutoka kwa wazazi wake. Msanii katika wimbo huu anagusia suala la urithi. Wanaume wanashikilia msimamo kuwa wao ndio wanaostahili kurithi mali ya wazazi. Katiba ya Kenya 2010, inaeleza kuwa, wanawake na wanaume wana haki sawa katika masuala yote pamoja na kuwa na mali au kurithi. Kwa hivyo, jamii inastahili kubadili mtazamo wake kuhusu suala la urithi.

Imeonyesha kuwa tamaa vile vile inamfanya mwanamke kutotulia katika ndoa yake. Katika wimbo *Aka nima mithemba* (Aina mbalimbali za wanawake ) mtunzi amemsawiri mhusika Nzembi ambaye ni mke aliyemuoa kutoka eneo la Emali kama mwenye tamaa. Anamchora Nzembi kama mwanamke asiyetulia na mume mmoja. Uchumi wa pesa na hali ya kutaka kujikimu ni baadhi ya vitu ambavyo vimekuwa na athari kubwa katika jamii. Msanii anaeleza haya kupitia ubeti huu:

| | |
|---|---|
| *Ninye natwaie Nzembi kuma ngaluko sya Emali, avika kwakwa angeuka, kai ni uko wa Kilata, na ni uko wa usavi, ngamulungililya Itheka.* | .Nilioa Nzembi kutoka pande za Emali,<br>Tulipofika kwangu akabadilika,<br>Kumbe ni kirukanjia na mbeya, |
| *Auma vu kwakwa ngamwiwila Kajiado Atwaitwe ni Masai, onaku Akalungwa.* | Alipotoka Kwangu akahamia Kajado<br>Alikoolewa na Masai,hata huko akatalikiwa,<br>Kumbe ni kirukanjia |
| *Auma Kajiado ngamwiwila Kikuyu, atwaitwe ni Mwikuyu,*<br>*Onaku akalungililywa itheka, ni uko wa kilata na ni Uko wa kitimba,*<br>*Aka me uko ta indo.* | Alipotoka Kajiado alihamia Kikuyu,<br>Alikoolewa na Mgikuyu,<br>Hata huko Akapewa talaka ,<br>Kwa sababu ya umbeya na Uasherati,<br>wanawake ni wa aina mbalimbali kama mifugo |

Ubeti huu unamweleza Nzembi mwanamke asiyetulia. Nzembi ni jina la kimajazi lenya maana ya asiyetulia. Alipoolewa na mume wa kwanza hakutulia alimtaliki na kuolewa na mwingine. Mwanamke amesawiriwa kama mwenya tamaa kwa sababu anawatamani wanaume tofauti, mbona asitulie na mmoja? Nzembi anasemekana kuwa na tabia ya uasherati, tendo linaloonyesha kuwa alikuwa na tamaa ya pesa alizochuma kutoka kwa wanaume hawa kupitia tendo la ngono.

Wanawake wamesawiriwa kama wenye kupoteza mwelekeo. Wamekuwa wachuuzi wa miili yao. Pesa zimevuruga maadili ya kijamii jambo ambalo linamkera mtunzi huyu. Mtunzi huyu ananuia kuwatahadharisha baadhi ya wanawake ambao hawana mapenzi kwa mwanamume . Mapenzi yao yamo katika pesa *zao*. Sifa hii inamdhalilisha mwanamke kwani huenda kule kutotulia kulisababishwa na kasoro fulani ya wanaume aliokumbana nao katika pita pita zake.

Msanii katika wimbo wa *Nyinya wa syana* (Mama watoto) amemsawiri mwanamke kama mwenye tamaa ya pesa, wakati anaposema kuwa, akimpa mke wake pesa anadai zaidi. Anayaeleza haya kupitia ubeti huu:

| | |
|---|---|
| *Niuma wiani ngivika uimbitya mbesa,* | Nitokapo kazini wadai pesa, |
| *Nenga silingi mbongela kasumuni na* | Nipe shilingi niongezee zaidi, |
| *Nathelelwa kui mwiwano,* | Na nikifilisika amani inakosekana huku |
| *Ndineena ndyitwa katondomi.* | Ukigeuka mpyaro. |

Wimbo huu unamweleza mama watoto kama ambaye hatosheki. Anataka pesa kila mara na mume wake akifilisika hakuna amani katika nyumba. Anampa majina ya lakabu '*katondomi'* lenye maana ya 'mtu anayepayuka tu.' Kule kudai pesa kwa mama watoto kunamchora mwanamke kama ambaye anamtegemea mwanamume kwa kila jambo. Mama watoto anaweza kuwa alichopewa hakikuweza kutimiza haja za familia. Kwa hivyo, ni wajibu wa kila mmoja kuwajibikia majukumu yake pasi kulimbikiziana lawama. Mtafiti anawatahadharisha wanajamii

hususan wa Kiafrika kuwa tamaa si hazina katika maendeleo ya taifa lolote Afrika na dunia nzima kwa jumla. Wanajamii wanastahili kuepuka tabia kama hizi na kukumbatia tabia njema.

Tamaa ni tabia ambayo anaweza kuwa nayo mtu yeyote awe mwanamke au mwanamume. Wanawake wa jamii ya Wakamba wamesawiriwa na watunzi hawa kama wenye tamaa. Dhana kama hii haiungwi mkono na utafiti huu kwani mwanamke anayo haki ya kudai haki yake. Kama anataka pesa za mahitaji ya kimsingi asichukuliwe kuwa mwenye tamaa kwani ni haki yake. Tunakubaliana na wasanii hawa kuwa njia nyingine za kuchuma pesa hazifai lakini mwanamke akipewa nafasi yake ya kujiendeleza ataweza kujitimizia mahitaji yake pasi kumtegemea mwanamume. Lyatuu (2011), anasisitiza kwamba, mwanamke akipewa nafasi kutekeleza majukumi yake ataondokea mawazo potofu ya baadhi ya wanajamii kuwa, nafasi waliopewa wanawake ni kwa mapenzi ya Mungu.

### 4.5.4 Mwanamke Kama Mgomvi

Maisha yanategemea mno uhusiano mzuri baina ya mtu na mtu, mtu na watu na vile vile mtu na jamii yake. Kama ugomvi utakuwa baina ya wanajamii, basi uhusiano mwema utakosekana. Uhusiano mwema unawezekana tu pale ambapo nidhamu inadumishwa katika kuzingatia utu. Wimbo mmoja ndio uliogusia suala hili ambao ni sawa na asilimia kumi (10%). Kwa hivyo watunzi wengine nane (8) hawakumsawiri mwanamke kama mgomvi.

Wimbo wa *Nyinya wa syana* (Mama watoto), mwanamke amesawiriwa kama mgomvi na aliye na tabia ya kumgombeza mume wake.Kwa mfano kupitia mshororo huu; *ndivika uindavya ndeto veveve* (..nikifika unanitolea maneno ovyo ovyo). Msanii ametumia mbinu ya takriri ‘veveve’ ili kupitisha ujumbe kuwa mke wake anaongea sana na tabia hii ndiyo inayozua ugomvi baina yake na mumewe. Kupitia tabia hiyo, mume wake anatishia kumwoa mke mwingine ambaye anasema

atakuwa mrembo na mwenye tabia nzuri zaidi kuliko yule mwenye ugomvi. Mtunzi anaeleza haya kupitia ubeti huu:

| | |
|---|---|
| *Kai wingendwa nundu wa kwithiwa na Syana,* | Wanidharau kwa sababu ya watoto, hujui |
| *Kotesi aume me mavinduka maingi, No ndwae* | Wanaume wana mipango mingi, ninaweza |
| *Kakua mbunguo noitiwa Ungethetye kiveti.* | Kuoa mke mwingine mrembo zaidi na ubaki Ukiduwaa. |

Ubeti huu unaeleza kuwa, mama watoto anamdharau mume wake kwa sababu ya watoto, mume wake anamwambia kuwa wanaume wana mipango mingi anaweza kuoa mke mwingine. Mwanamke anapodai haki yake si eti anamdarau mume wake. Wanaume wanastahili kuelewa kuwa, watoto katika ndoa ni jukumu la wazazi wote wawili. Kuoa mwanamke mwingine sio suluhu, mwanamume anaonekana kumtishia mke wake kwa kusema kuwa ataoa mke mwingine. Ni vyema mwanamume atambue kuwa, mwanamke ana uwezo wa kufanya maamuzi sawa na mwanamume. Katika maamuzi ya ndoa yao ni vizuri wote wawili wakubaliane.

Wimbo huu utaeleweka vyema kupitia utamaduni wa jadi wa Wakamba. Jamii ya jadi ya Wakamba, mwanamke alipaswa kumwonyesha mume wake heshima, hata wakati wa mume wake kumkosea heshima. Alipaswa kutumia mavyaa wake kuongea na mumewe ili kusuluhisha matatizo baina yao (Watuma, 2001). Hakuna udamaduni wa jadi na wa kisasa. Utamaduni haubadiliki. Kwa hivyo maoni ya Watuma hatukubaliani nayo kwani jamii hukumbwa na mabadiliko kama vile ya kiuchumi, kijamii, kisiasa miongoni mwa mengine kadri wakati unavyosonga. Wakati wa sasa kuna wanawake ambao huwakosoa waume zao na kuchangia katika ujenzi wa familia. Kwa hivyo maoni ya mwanamke yasipuuzwe.

Mtunzi wa wimbo huu alikuwa na lengo la kukashifu hasira za mwanamke. Anaendelea kuwatahadharisha wanawake kuwa ni heri kunyamaza kuliko kutoa tamko kwa hasira kama afanyavyo mama watoto kwa sababu jambo hili husababisha ugomvi miongoni mwa wanajamii. Kulingana na wimbo huu, mwanamke anabaguliwa kwa sababu ugomvi huwa kati ya watu wawili wala si mtu mmoja.

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika imetusaidia kuweka wazi tabia ya baadhi ya wanawake kuendeleza suala zima la ugomvi; kwani nadharia hii hutumia fasihi kama jukwaa la kueleza kwa uyakinifu hali aliyomo mwanamke ili kumsaidia mtu yeyote kuielewa hali hiyo. Katika jamii zetu za Kiafrika tabia hii inaendelea kuchukuwa nafasi miongoni mwa wanawake. Mtafiti ameona kuwa masuala haya husababisha kufikia hatua ya usaliti, uhasama , uadui na vita baina ya mume na mke.

### 4.5.5 Mwanamke Kama Mtu wa Mipango ya Hadaa

Mipango ya hadaa ni miongoni mwa matendo yanayoendelea kuchukua nafasi katika maisha ya kila siku. Baadhi ya watu, wakiwemo wanawake, hubuni mipango ambayo baadaye huleta athari katika familia. Uchunguzi umebaini kuwa mipango ya hadaa huweza kuchangiwa na sababu mbalimbali zikiwemo kisasi kwa matendo aliyotendewa mtu binafsi au familia. Nyimbo ambazo zimegusia suala hili ni tatu (3) kwa kumi sawa na asilimia thelathini (30%).

Wimbo wa *Syoka Mami* (Rudi mama) mwanamke amesawiriwa kama mwenye mipango ya kuhadaa pale ambapo mke alimdanganya mume wake kuwa alikuwa anaenda sokoni kumbe alikuwa na mpango wa kutoroka. Mwanamke huyu baada ya kutoroka kwake, alienda mjini Nairobi alikoanza maisha mengine. Mtunzi ameelezea haya kupitia kifungu hiki

| | |
|---|---|
| *Lilikana uyuma kwaku watavisye ndati withi*<br>*Soko kumbe wainasyaku wavangite kutoloka.* | Kumbuka ulipotoka nyumbani ulimweleza<br>Baba kuwa ulikuwa unaenda sokoni kumbe<br>Ulikuwa na mpango wa kutoroka. |

Katika wimbo wa *Aka ni ma mithemba* (Aina mbalimbali za wanawake), mwanamke amesawiriwa kama mwenye mipango na hadaa. Mhusika Nzembi alikuwa na tabia ya kuwahadaa wanaume kuwa alikuwa anataka kuolewa kumbe alikuwa na nia tofauti. Jambo hili lilisababisha kutotulia kwake na mume mmoja akawa 'kirukanjia.' Nzembi hatimaye alipewa talaka na yule aliyemwoa. Mtunzi anadhihirisha haya kupitia ubeti huu:

| | |
|---|---|
| *Auma vu kwakwa ngamwiwila Kajiado,*<br>*Atwaitwe ni Masai, unaku akalungwa,*<br>*Ni uko wa kilata na ni uko wa usavi* | Nilipomtaliki, alihamia Kajiado<br>Alikoolewa na Mmasai, hata huko akatalakiwa<br>Alikuwa kirukanjia na mbeya. |

Ubeti huu unaelezea vile Nzembi alikuwa akiwahadaa wanaume tofauti, alipotoka kwa mume wake wa Emali, alimpata mwingine wa Kajiado ambaye hatimaye alimpa talaka kwani alikuwa kirukanjia. Sifa aliyopewa Nzembi ya kuhadaa wanaume inamdunisha na kumdhalilisha mwanamke.

Wanawake wamesawiriwa kama wenye mipango na hadaa pia katika wimbo wa *Aka ma taoni* (Wanawake wa mjini). Wanawake hawa huwahadaa wanaume mradi wapate pesa. Msanii anaeleza haya kupitia ubeti huu:

| | |
|---|---|
| *Makwona na mbesa, mo mewaa maile kwosa,*<br>*Syo siisawa muthekete na syathela*<br>*Mo maisemba.* | Wakimwona mwanamume akiwa na pesa,<br>Wao hupanga njama ya kuzichukua,<br>Wao huonyesha mapenzi ya uwogo,<br>Ukifilisika wanahepa |

Wanawake hawa wa mjini wanawataka wanaume wenye pesa. Wao huwapumbaza huku wakicheka nao, huwaonyesha mapenzi yasiyo ya kweli. Wanaume hawa wanapofilisika wao

hutokomea mbali. Wanawake wamesawiriwa katika hali ya kuendesha umalaya kama njia yao ya kukithi haja zao za kimaisha. Vitendo hivi vya ufuska vinatendwa na wahusika wote, wake kwa waume. Jambo hili husababisha aibu na pia linaweza kuchangia kuenea kwa maradhi mbalimbali yakiwemo yale ya zinaa.

Wanajamii wanastahili kuelewa kuwa mipango na hadaa ina madhara yake katika jamii. Wanawake wamesawiriwa kuwa ndio wenye mipango na hadaa lakini katika kule kuhadaiwa anatokea mwanamume. Jambo hili linadhihirisha kuwa watu wote wake kwa waume wanaweza kuwa wenye mipango na hadaa. Hata wanaume huwahadaa wake zao ili kwenda nje ya ndoa. Siyo tu kwamba haki sawa haitakuwa imetendwa kwa wote bali ni njia ya kufichua uovu unaoendelea katika jamii na kuuweka bayana.

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika imeendelea kutoa msisitizo kwamba matendo maovu si mtaji. Wanawake wana nafasi kubwa katika kuhamasisha kuhusu maendeleo yao na taifa zima. Wanastahili kukemea na kuachana na tabia za hadaa kwa watu wengine. Nadharia hii inawataka wanawake wajitambue na wasiwe tayari kujiingiza katika tabia za aina hii bali wawe tayari kujihusisha na miradi ambayo itawafaa wao na jamii kwa jumla.

**Jedwali (iii):** Nyimbo zenye sifa hasi

| **Namba** | **Usawiri wa sifa hasi** | **Wimbo** | **Jumla** | **Mtunzi** |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mwanamke kama mshirikina | *Kiveti ngungu* | *3* | *Kakai Kilonzo* |
| | | *Aka ma taoni* | | *Dan Mutuku* |
| | | *Nyinya wa Ndetei* | | *Kijana Mumo* |
| 2 | Mwanamke kama | *Aka ma taoni* | *3* | *Dan Mutuku* |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | muasherati | *Syoka Mami* | | *John Muasa* |
| | | *Aka nima mithemba* | | *Wanginga* |
| 3 | Mwanamke kama mwenye tamaa | *Aka ma taoni* | *4* | *Dan Mutuku* |
| | | *Kavola Kavola Kamengele* | | *Ancent Munyambu* |
| | | *Aka nima mithemba* | | *Wanginga* |
| | | *Nyinya wa Syana* | | *Dicky Mulwa* |
| 4 | Mwanamke kama mgomvi | *Nyinya wa Syana* | *1* | *Dicky Mulwa* |
| 5 | Mwanamke kama mtu wa mipango na hadaa | *Syoka Mami* | *3* | *John Muasa* |
| | | *Aka ma taoni* | | *Dan Mutuku* |
| | | *Aka nima mithemba* | | *Wanginga* |

Kulingana na jedwali hii, wasanii wa nyimbo hizi za sifo za Wakamba wamemsawiri mwanamke kwa kumpa sifa hasi tano (5). Kwa hivyo, wamemdhalilisha na kumtweza. Kupitia sifa tano zilizoibuka katika utafiti huu, sifa ya mwanamke kama mwenye tamaa imeangaziwa na wasanii wengi zaidi. Wasanii hawa ni Wanginga, Dicky Mulwa, Dan Mutuku na Ancent Munyambu. Mwanamke anapopigania ukombozi wake anaweza kuonekana kama mwenye tamaa kinyume na ari yake. Mwanamke kama mwenye mipango na hadaa ni sifa imeangaziwa na wasanii watatu. Wasanii hawa ni : John Muasa, Dan Mutuku na Wanginga.  Kakai Kilonzo, Dan Mutuku na Kijana Mumo wamemsawiri mwanamke kama mshirikina. Sifa ya mwanamke kama muasherati

imegusiwa na wasanii Dan Mutuku, John Muasa na Wanginga. Dan Mutuku amewasawiri wanawake kuwa wenye sifa hasi kwa kiwango cha juu.

**Jedwali (iv):** Jedwali kuonyesha kiwango cha sifa hasi kwa mujibu wa watunzi

| **Mtunzi** | **Jumla** | **Sifa kwa asilimia** |
|---|---|---|
| Dan Mutuku | 4 | 40% |
| Wanginga | 3 | 30% |
| John Muasa | 2 | 20% |
| Dicky Mulwa | 2 | 20% |
| Kijana Mumo | 1 | 10% |
| Kakai Kilonzo | 1 | 10% |
| Ancent Munyambu | 1 | 10% |

Kwa mujibu wa jedwali hii, wasanii wameonyeshwa jinsi walivyomsawiri mwanamke kwa kiwango cha asilimia. Dan Mutuku ndiye mwenye kiwango cha juu cha asilimia arobaini (40%), akifuatwa na Wanginga kwa kiwango cha thelathini (30%), John Muasa kiwango cha ishirini (20%) pamoja na Dicky Mulwa. Wasanii Kakai Kilonzo, Kijana Mumo na Ancent Munyambu wamechukuwa kiwango cha chini cha asilimia kumi (10%). Usawiri huu umejikita katika kuuchora ukweli na uhalisia wa mienendo ya wanawake kwa kutumia ulimwengu uliobuniwa na wasanii husika.

## 4.6 MAUDHUI KATIKA NYIMBO ZA SIFO ZA WAKAMBA YANAYOAKISI HALI HALISI YA MWANAMKE KATIKA JAMII YA WAKAMBA

Lengo mahsusi la tatu la utafiti huu; kutathimini kama hali halisi ya jamii ya Wakamba kwa sasa hivi, karne ya ishirini na moja, imebadili mawazo kwa kusawiriwa mwanamke kama binadamu ajiwezaye kupitia maudhui ya nyimbo hizi, limezingatiwa hapa.

Ndungo (1985) anasema kuwa fasihi ni hali halisi ya maisha. Kulingana naye, msanii kama mwanajamii huandika au kusimulia kutokana na tajriba anayoipata kutoka jamii anamoishi. Utafiti unaunga mkono maoni hayo ya Ndungo anaposhilikia kuwa, kazi nyingi za fasihi huweza kueleweka kupitia maudhui yake yanayohusu jamii na wakati maalumu.

Akiunga mkono kauli hiyo, Ngugi (1993) anasema kuwa fasihi haitoki katika ombwe tupu. Inapata mwelekeo, umbo na umuhimu wake kutoka jamii mahususi. Kwa mujibu wa Ngugi, masuala yanayoipa fasihi mwelekeo ni pamoja na uchumi, siasa, elimu, utamaduni, ndoa na mabadiliko mengine yanayotokea katika nyanja zozote za maisha ya jamii. Anaeleza kuwa tamaduni zinazobadilika ili kusawiri mabadiliko ndizo mwafaka zaidi.

Matukio makuu ya mwongo fulani yanaweza kutambulika kutokana na fasihi ya mwongo huo, kupitia kipengele cha maudhui. Maoni haya yanatiliwa mkazo na Njogu na Chimera (1999) wanaoshikilia msimamo kuwa, fasihi ni hai na hubadilika kadri jamii inavyozidi kubadilika. Kubadilika kwa maudhui ya nyimbo kulingana na wataalamu kama King'ei na Kisovi (2005) ni kwa sababu wimbo ni utanzu wa fasihi simulizi ulio hai, ambao hukua na kubadilika kulingana na mpito wa wakati na mabadiliko ya mfumo wa jamii.

Mabadiliko katika jamii yanawachochea watunzi kutunga nyimbo zinazolandana na wakati. Msukumo huu wa mabadiliko unaungwa mkono na Njogu na Chimera (1999) wanaposema kuwa

kuna uhusiano mkubwa kati ya sanaa na matukio ya kijamii; hivyo basi maudhui yanamsukuma mtunzi kwa kipindi alicho nacho. Maudhui yafuatayo yanalenga kutathimini kama jamii ya Wakamba imebadili mawazo na kumsawiri mwanamke kama binadamu ajiwezaye kupitia kwa nyimbo hizi za sifo za Wakamba.

Jamii ya Wakamba imeshuhudia mabadiliko kiwakati. Mabadiliko haya yamesababishwa na mfumo wa uongozi, msisimko wa teknolojia mpya, elimu ya Kimagharibi, kukua kwa miji na viwanda, maendeleo katika nyanja mbalimbali za kiuchumi, dini miongoni mwa mabadiliko mengine. Mabadiliko haya yameathiri kwa kiwango fulani fasihi simulizi yao. Nyimbo zimeathiriwa na mabadiliko haya. Kubadilika huku kunatokana na sababu kwamba, nyimbo ni kipengele cha utamaduni wa watu ambao kila siku unaendelea kuzaliwa, kuathiriwa na kubadilika jinsi maisha yanavyobadilika.

### 4.6.1 Elimu

Baada ya mjo wa wakoloni, jamii ya Wakamba sawa na jamii nyingine za Kiafrika ilipapia elimu ya Kimagharibi ambayo ilihusu usomaji wa darasani. Suala la elimu ya Kimagharibi ni nyeti katika jamii ya kisasa kwa sababu linahusishwa na nguvu na uwezo wa kiuchumi (Kaui, 2008). Kutokana na imani hii baadhi ya nyimbo za sifo za Wakamba zinasawiri maudhui ya umuhimu wa elimu mpya ya kisasa katika jamii.

Kama ilivyosisitizwa na waasisi wa Ufeministi, elimu ni kitu cha msingi katika harakati za kupigania ukombozi wa mwanamke. Mwanamke akipewa nafasi sawa ya elimu pamoja na mwanamume anaweza kustawi vizuri. Wanawake wengi wana uwezo wa kujiendeleza kielimu iwapo watapewa nafasi ya kufanya hivyo. Steady (1981) anaunga mkono maoni haya anaposema kuwa mwanamke wa Kiafrika anaweza kushiriki katika maendeleo ya jamii yake ilimradi

amepewa nafasi hiyo. Elimu ni nguzo maishani mwa binadamu yeyote yule kwani humtoa ujingani. Mwanamke anapopata elimu basi jamii nzima kwa jumla huweza kunufaika.

Katika kitabu chake *A Vindication of the Rights of Women* (1792) Mary Wallstonecraft alidai kwamba unyonge wa mwanamke husababishwa na mfumo wa kijamii na hali hii inaweza kurekebishwa kwa kusambaza kiwango sawa cha elimu kwa watoto wote wasichana kwa wavulana. Kulingana na Wollstonecraft, baada ya wasichana kupokea elimu bora watakuwa katika nafasi nzuri ya kuweza kupigania haki zao na pia kugombea nafasi mbalimbali katika jamii. Anazidi kueleza kuwa mwanamke hastahili tu kufanya kazi za nyumbani bali anastahili kupata elimu bora jinsi ilivyo na wanaume. Elimu ni silaha muhimu katika maisha ya binadamu.

Mwanamke akipokea elimu bora anaweza kuwa katika nafasi nzuri ya kujikomboa. Katika utafiti huu, data zilizokusanywa na mtafiti zimeweka wazi kuwa mwanamke kupitia maudhui ya nyimbo hizi anaonekana kama ambaye ameanza kujikomboa kielimu. Wimbo wa *Kana Nzula* (Mpenzi Nzula) msanii anaonekana kutambua elimu ya wanawake kupitia kwa mhusika Nzula. Nzula baada ya kuhitimu masomo ya shule ya upili, alienda ughaibuni kujiendeleza kielimu. Alienda kusomea udaktari ambako baada ya kusoma alirejea nyumbani kwa mchumba wake ili kuunda familia. Nzula ni mfano mwema wa wanawake ambao wanaonekana kujikomboa kielimu. Taaluma aliyoenda kusomea ya udaktari ni baadhi ya kazi zilizotambulika kufanywa na wanaume. Alielewa thamani ya elimu na ndio maana kwanza anasoma kabla ya kuolewa. Msanii anaeleze haya kupitia ubeti huu:

| | |
|---|---|
| *Niwikite nesa kunzyokea we Nzula,* | Ninafurahia kurudi kwako Nzula, |
| *Ngwetele Nzula umine masomo mwendwa,* | Nilikuwa nikihuzunika sana mpenzi, |
| *Ninai na wia nutonya kutwawa ni musungu,* | Nikikusubiri ukamilishe masomo, |
| *Uka Nzula kana ni vata naku.* | Nilikuwa nahofia utaolewa na mzungu. |

Ubeti huu unaeleza jinsi mchumba wake Nzula alivyomsubiri akamilishe masomo, anajawa na furaha kwa sababu ya kurudi kwake Nzula. Nzula kwanza aliyapa masomo yake kipaumbele. Kule kuthamini masomo kunaonyesha kuwa wanawake wameanza kuamka kutoka kwenye usingizi uliowalemaza wa kutosoma. Lyatuu, (2011); ameyaona waliyoyasema Mbilinyi na wanzake (1991) na akapendekeza kwamba, elimu ndiyo mkombozi wa mwanamke wa kumwezesha kujitoa katika mfumo kandamizi wa wanaume jambo ambalo linaungwa mkono na utafiti huu.

Umuhimu wa mwanamke kielimu unajitokeza tena pale ambapo mtunzi wa wimbo wa *Syoka Mami* (Rudi Mama) anapoeleza jinsi walivyotaabika, mama alipomtaliki baba yao. Hata kama mama hajulikani elimu yake ni ya kiwango gani , msanii huyu anasema kuwa elimu yao ilikuwa ya shida tangu mama alipoondoka nyumbani . Mfano ubeti huu:

| | |
|---|---|
| *Kusoma kwitu kwai na muisyo kitumi nundu* | Kusoma kwetu kulikumbwa na changamoto |
| *Mami niwaendie,* | Kwa sababu mama ulituacha. |
| *Indi kalivu syoka musyi musyi kwaku uthumue.* | Karibu nyumbani upumzike. |

Maelezo haya yanaweka bayana kuwa mwanamke anachangia katika elimu ya watoto. Watoto wake wanamchukulia kuwa kiungo muhimu katika elimu yao. Mtafiti anaamini kwamba msanii huyu mwanamume anamwona mama mzazi kama mtu anayeshikilia elimu ya watoto wake. Haya yanajitokeza anaposema kuwa elimu yao iliingia doa kwa sababu mama yao aliwaacha. Uchunguzi huu umebaini kuwa, ijapokuwa mwanamke haonekani akijikomboa kupitia elimu, anajua kuwa kupitia elimu binadamu anaweza kuwa na maisha mema ya baadaye.

Bosco Mulwa ni msanii mwingine anayegusia suala la elimu. Mwanamke katika wimbo wa *Mother* (Mama), msanii anaeleza kwamba mama alimpa malezi ya kimsingi ambayo ni chakula,

mavazi na elimu. Maelezo haya yanaonyesha kuwa mwanamke hujua kuwa elimu ni suala la kimsingi. Mama anaonekana kujali elimu ya mtoto wake kwani maishani elimu hii itamwangazia. Mwanamke akipewa nafasi anaweza kujielimisha na pia jamii kwa jumla. Anadhihirisha haya kupitia maelezo haya:

| | |
|---|---|
| *Liu ngua na kisomo* | Mahitaji ya kimsingi ulitimiza, |
| *Wandeie nesa,* | Chakula, nguo na masomo, |
| *Mother ii mother ii ngai akuathimae wi wakwa* | Ulinilea vyema mama mpenzi, |
| | Mungu akubariki mama. |

Wasanii hawa wawili wameonyesha mwanamke kama mzazi anayeshughulikia elimu ya watoto wake. Japo hawajaonyesha bayana ule ukombozi wao, lakini wanaonekana kuchukulia elimu kama chombo cha kuwawezesha watoto wao kujiendeleza. Mwanamke anastahili kujua kuwa elimu ni njia mwafaka ya kujikomboa yeye mwenyewe pamoja na jamii nzima.

Justus Myello anamtambua mwanamke kama mwenye uwezo kielimu. Anaeleza kuwa mwanamke huzaliwa na akili tambuzi na hata masomo huwa nayo. Kulingana na mtafiti, msanii huyu anaonekana kuunga mkono elimu ya mwanamke. Tafsiri ya tabia ya mwanamke mara nyingi hutolewa na namna mwanamke anavyotazamwa na jamii. Mara nyingine ni jinsi wanaume wanavyomtazama au kuelezewa katika sekta tofauti za jamii. Sehemu hii inaonyesha jinsi msanii huyu anavyomtazama mwanamke:

| | |
|---|---|
| *Yuyu nooka nasye aka ithyi twikwo na* | Nawasifia wanawake nikisema, |
| *Tunengetwe utonyi ni mumbi witu,* | Wamepewa uwezo na mwenyezi Mungu, |
| *Akili na kisomo tutuie nasyo,* | Akili tambuzi pia masomo wanamiliki. |
| *Ona maovisi manene tutua namo.* | |

Ukosefu wa elimu bora miongoni mwa wanawake wengi, umesababisha hali ya kutojielewa kwao na hata pia kujua malengo yao. Elimu ni silaha muhimu katika maisha ya binadamu.

Mwanamke akipokea elimu bora, anaweza kujikomboa. Matatizo mengi yanayowakabili wanawake yanatokana na kutojielewa na pia kutoelewa chanzo cha matatizo yao. Mwanamke anatajwa kuwa mwenye akili tambuzi. Kwa hivyo mwanamke akipewa nafasi kujiendeleza kielimu ana uwezo wa kufanya mengi. Jambo hili linadhihirika kupitia maelezo ya msanii huyu anaposema kuwa hata ofisi kubwa wanawake wana uwezo wa kunyakua mamlaka. Anadhihirisha haya kupitia ubeti huu:

| | |
|---|---|
| *Andu aya nienda masuviwe muno, ndaia nene manengwe.* | Watu hawa naomba watunzwe sana, heshima zote wapewe, |
| *Ooh itui sya kwaka musyi.* | Ooh nguzo na mhimili wa familia, |
| *Yuyu nooka nasye aka ithyi twikwo na* | Sasa nasema wanawake tupo, |
| *Tunengetwe utonyi ni mumbi witu,* | Tumepewa mamlaka na uwezo na Mungu, |
| *Akili na kisomo tutuite nasyo,* | Akili tambuzi na elimu tunaishi nazo, |
| *Ona maovisi manene tutua kw'o.* | Hata nyadhifa kubwa tunaongoza. |

Msanii anasema kuwa, wanawake wanahitaji kutunzwa, waheshimiwe kwani ni nguzo za kujenga familia. Anazidi kueleza vile wanawake wamepewa uwezo na Mwenyezi Mungu kufanya mambo mbalimbali. Katika jamii ya Wakamba kuna wanawake wenye nyadhifa mbalimbali katika nchi ya Kenya, kwa mfano Charity Kaluki Ngilu ambaye sasa ni Gavana wa Kaunti ya Kitui, Wavinya Ndeti aliyekuwa mbunge wa Kathiani mwaka wa 2007-2012, Dorcas Mwilu ambaye sasa ni Naibu Jaji Mkuu, Dkt. Monica Juma ambaye hii leo ni waziri wa Mambo ya Kigeni miongoni mwa wengine. Nchini Kenya na ulimwenguni kote wapo wanawake ambao wana uwezo wa kuongoza, mfano Marehemu Profesa Wangari Mathai alionyesha ushujaa wake kwa kuwa mstari wa mbele kupinga uchafuzi wa mazingira. Alituzwa tuzo ya Nobeli mwaka wa 2005. Bi. Margaret Thatcher aliyekuwa Waziri Mkuu nchini Uingereza miaka ya tisini, aliongoza vyema nchi hiyo na kupata umaarufu. Kwa sasa hivi Uingereza kuna Theresa Mayer kama Waziri Mkuu Ujerumani, Ellen Johnson Sirleaf alikuwa rais wa Liberia kutoka 2006

mpaka 2018. Alikuwa mwanamke wa kwanza kuchaguliwa kama rais barani Afrika. Kwa hivyo kasumba ya kumdunisha mwanamke ni jambo lisilo na mashiko yoyote na linafaa kutupiliwa mbali katika ulimwengu wa leo.

Kwa msaada wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, mtafiti amegundua kuwa wanawake wanaendela kuamka na kutoa msukumo mkubwa katika kutafuta elimu. Elimu tangu zamani hadi sasa imeonekana kama silaha yakinifu ya kumkomboa mwanamke kutokana na ujinga na utegemezi mkubwa kwa mwanaume miongoni mwa mengine. Wanawake kwa kiwango fulani wamebadilika na kuwa wasomi pamoja na kuthamini elimu. Jambo hili limewawezesha kujiamini na kuwa viongozi bora katika nyanja tofauti.

### 4.6.2 Ndoa

Jamii ya Wakamba kama zilivyo jamii nyingine za Kiafrika kutoka zamani ilitambua ndoa kama asasi muhimu ya kuendeleza kizazi. Mwanaume katika jamii ya Wakamba akifikia umri wa kuoa, alikuwa akipewa mawaidha juu ya suala la ndoa. Baadaye alipewa nafasi ya kujitafutia mke. Akimpata alikuwa anawaambia wazazi wake ama wazee. Kulikuwa na kipindi kilichojulikana kama '*kuowa'* hiki ni kipindi cha kuangali mienendo na tabia za msichani aliyemtaja. Msichana akikubaklika na jamii mipango ya ndoa ilianza kushughulikiwa (Watuma, 2011). Mambo siku hizi yamebadilika kutokana na yanayokumba jamii ya sasa kama vile mfumo wa teknolojia, elimu, dini miongoni mwa mengine. Wachumba wanapatana katika maeneo tofauti wanachumbiana na kuoana hata bila kuwaarifu wazazi au wazee.

Ndoa ni miongoni mwa asasi za kijamii ambazo baadhi ya wafuasi wa Ufeministi wanapigania ziondolewe. Wafuasi wa ufeministi wanadai kwamba ndoa ni moja ya kati ya asasi nyingi za kijamii ambazo hutumiwa katika kuwadhulumu wanawake. Madai ya Ufeministi kuhusu ndoa ni

kwamba mwanamke anapoolewa na kulipiwa mahari, mwanamke huchukuliwa kuwa mali ya mume. Hali hii kulingana na ufeministi husababisha kuonewa na kudhulumiwa kwa wanawake. Utafiti huu unapinga maoni ya wafuasi wa Ufeministi kwa sababu ndoa ikiondolewa katika jamii, utambulisho wa jamii utafifia. Ndoa ni asasi muhimu katika jamii yoyote ile kwa kuwa msingi wa uzazi unaendelezwa kupitia watoto. Mbiti (1991) anaeleza kuwa, suala la ndoa ni kipengele kinachotambuliwa duniani kote kama suala nyeti lenye kuathiri maendeleo ya kijamii. Ni vyema kila mwanajamii awe na mtazamo mwema kuhusu suala la ndao pasi kumwona mwanamke kama mtumwa.

Ogundipe – Lesile (1984) anamwona mwanamke wa Kiafrika kama aliye na mizigo ya ziada inayomlemea. Kuna unyanyasaji kutoka nje na ule urithi mila na desturi za Kiafrika. Mwanamke wa Kiafrika ndiye anayeweza kuufasili uhuru wake yeye mwenyewe. Anafungwa na mielekeo hasi juu yake mwenyewe na kutawaliwa na itikadi za mifumo ya kuumeni na taasubi za kiume.

Kwa kuwa mwanamke ana uwezo wa kufasili uhuru wake, ni muhimu kuzingatia uamuzi atakaochukuwa katika maisha yake. Iwapo utakuwa wenye manufaa katika maisha yake, basi hana budi kuchukuwa uamuzi huo. Mwanamke anayedhulumiwa katika ndoa anastahili kupima dhuluma hizo na hali yake ya maisha. Akiona kupata talaka kutakuwa na suluhu, anapaswa kuiacha ndoa yake na kutafuta njia nyingine za kujikimu.

Mwanamke katika jamii ya Wakamba hatarajiwi kuonyesha ujasiri ama uwezo wowote na nguvu za kukabiliana na mume wake. Anapaswa kuonyesha unyenyekevu, uvumilivu, subira na utiifu kwa wanaume wote (King'ei, 1982; Nzioki, 1982). Mwanamke wa Kiafrika anashauriwa awe na nidhamu katika lugha yake. Mawazo ya King'ei na Nzioki hatukubaliani nayo kwani mwanamke anastahiki haki yake katika ndoa. Ni mhimili mkubwa anayestahili kuheshimiwa sawa na mwanamume. Ni vyema apewe uhuru wa kutoa maoni yake katika ndoa. Kuna

wanawake wanaoendeleza familia zao bila wanaume  na wanafanya vyema hata zaidi ya familia zilizo na wanaume.

Katika jamii ya sasa ya Wakamba, wanawake wengi wamekaidi kimya cha kulazimishwa. Baadhi yao hujibizana na waume panapotokea haja. Jambo hili japo linaweza kutazamwa na jamii kama ni kuasi mila na tamaduni za jadi za Wakamba, jamii inatakikana kuelewa kuwa hata wanawake wanao uwezo wa kutoa hoja zikafuatwa na kufaidi familia na jamii kwa jumla. Watunzi wa nyimbo hizi wamelivalia junga suala hili la ndoa kupitia maudhui ya nyimbo hizi. Wameonyesha mwanamke kama ambaye ameanza kujikomboa kutokana na minyororo ya dhuluma katika ndoa zao.

Msanii katika wimbo wa *Nyinya wa Ndetei* (Mama Ndetei) anamsawiri Mwanamke akimtaliki mume wake na kwenda kwao na watoto na pia kukatiza mawasiliano naye. Haya yanaonyesha vile wanawake wameanza kuasi mila na tamaduni za jadi zilizoshikilia kuwa mwanamke ni mali ya mume wake. Mwanamke kuchukua hatua kama hii, inaonyesha kuwa yaliyomsibu yalimwumiza. Mama Ndetei alidhihirisha jukumu lake kama mzazi alipoamua kwenda kwao na watoto wake. Japo Mama Ndetei aliondoka, mume wake anaonekana kuhisi pengo katika ndoa yao. Anaelezea haya kupitia ubeti huu:

| | |
|---|---|
| *Nyinya wa Ndetei, nyinya wa Nthiwa ,* | Mama Ndetei, mama Nthiwa , |
| *Mami wa Koreta, kyeva cha ngoo na kimako nikyambingiviie,* | Mama wa Koreta, nahuzunika na kusononeka moyoni, |
| *Ketha wi tei na ukambona yu wamba kuia,* | Kama ungekuwa mwenye huruma, |
| *Kethiwa wi tei ukambona yu ninamosie* | Ungenihurumia kwani hali yangu si hali nimekonda |

Mume wake kupitia ujumbe huu anamweleza vile anahuzunika moyoni. Anazidi kumwambia kuwa hali yake si hali, amekonda na hata kama angemwona angelia. Mwanamume huyu

anaonekana kujawa na mawazo. Ametambua kuwa mwanamke ni kiungo muhimu katika ndoa. Kusema kuwa afya yake imedhoofika kunaonyesha kuwa, labda hapati chakula vizuri kwa kuwa wa kumpikia hayuko au mtafuta riziki alikuwa ni huyo mke wake. Ni wazi kuwa, mwanamke anao uwezo wa kukimu mahitaji ya kimsingi jinsi walivyo wanaume. Kwa hivyo, ni mhimili mkubwa katika jamii kwani anaweza kutegemewa sawa na mwanamume.

Mwanamke na mwanamume wote wawili wanastahili kukubaliana kuhusu changamoto zinazotokea katika ndoa yao. Ikiwa itafikia wakati mama watoto kurudi kwao, basi wakubaliane wataishi namna gani, si mwanamke akirudi na ameanza maisha yake, mume wake anaanza kumsumbua kwa kumweleza mambo mbalimbali yanayomhusu. Ni vyema kama ni talaka iwe na makubaliano. Mwanamke akimtaliki mume wake, asisumbuliwe kwa sababu amefikia uamuzi wake.

Katika wimbo wa *Syoka Mami* (Rudi Mama) mtunzi huyu amemchora mwanamke ambaye ni mama yake? Baada ya kuchoshwa na maisha ya ndoa aliamua kumwacha mume wake kwa kutumia hila kuwa alikuwa anaenda sokoni. Haya anayaelezwa kupitia ubeti huu:

| | |
|---|---|
| *Mami niki watwathukiie,* | Mama kwa nini ulitutelekeza, |
| *Mami niki watwathukiie,* | Mama kwa nini ulitutelekeza, |
| *Na nengi noue wa tusyaie,* | Ni wewe uliyetuzaa, |
| *Niki watutii na ndandi wathi uendo,* | Mbona ukatuacha na baba na kwenda kwenu. |
| *Lilikana uyuma kwaku,* | Kumbuka ulipoondoka, |
| *Watavisye ndandi wathi soko* | Ulimdanganya baba unaenda sokoni, |
| *Kumbe wai na muvango wavangite kutoloka* | Kumbe ulikuwa na mpango wa kumtaliki. |

Mtoto wake mama huyu ana maswali yanayomtatiza, anamwuliza mama yake mbona akawaacha na ni yeye ndiye aliyewazaa. Kusudi la mwanamke huyu lilikuwa kumtaliki mume wake.

Alipotoka kwa mume wake aliguria mjini Nairobi alikoenda kuanzisha maisha mapya. Alipofika mjini Nairobi, alianzisha biashara ya kuuza mabati kujitafutia riziki.

Kulingana na tabia za mwanamke huyu, tunaweza kumhukumu kama mwenye tabia ambazo hazikubaliki katika jamii. Lakini kabla ya kumtolea hukumu tunastahili kujiuliza; kwa nini alimwacha mume wake wa awali na kwenda kuishi na mwanamume mwingine mfanyabiashara? Mwanamke huyu alikuwa amemwacha mume wake pasi na kufanyiwa lolote. Mtunzi aneleza kuwa alimdanganya muwe wake kuwa alikuwa anaenda sokoni. Hatujaelezwa kuhusu ugomvi wowote kati yake na mume wake. Alipoenda sokoni hakurudi bali alienda mjini Nairobi alikoonekana na mwanamume mwingine waliokuwa wakiuza mabati.

Mwanamke huyu alikuwa amejikomboa kiuchumi kutoka kwenye ndoa ambayo hatujaelezwa ilikuwa na kasoro gani. Kule kuondoka kwa mama watoto bila kuaga kunaonyesha uwezekano wa upungufu wa jambo fulani katika ndoa yao ama kutoka kwa mwanamke au mwanamume.

Ni vyema wanajamii waelewe kuwa, kuna majanga mengi yanayoweza kumkumba mwanadamu yeyoye atakayekiuka maadili ya jamii. Kule kwenda kuishi na mwanamume mwingine kunaweza kumsababishia majanga katika maisha yake yakiwemo maradhi kama vile UKIMWI. Wanandoa wanastahili kujadiliana kuhusu mambo mbalimbali yanayoikumba ndoa yao bila kunyamazia. Kule kufanya uamuzi wa kwenda mjini bila hata watoto kujua, kumeleta ukiwa katika familia. Mwanamke anapojinasua anastahili kuishi maisha yatakayomfaidi yeye mwenyewe na jamii nzima kwa jumla.

Kupitia wimbo wa *Aka ni ma mithemba* (Aina mbalimbali za wanawake) kuna wanawake wanaoweza kudumu katika ndoa na wengine ni 'virukanjia.' Mtunzi anawapa tahadhari

wanaume wanaotafuta wachumba wawe waangalifu kwani kuna wanawake wasioweza kutulia katika ndoa. Mawaidha ya nyanya yake yanawatahadharisha wanaume kupitia sehemu hii:

| | |
|---|---|
| *Natavawa ni Susu ngambakwona ta ithau,* | Nilipowosiwa na nyanya nilidhani kuwa ni mzaha, |
| *Aka ni ma mithemba, kwi uko wa nzuku,* | Kuna aina mbalimbali za wanawake, |
| *Kwi uko wa kilata ,* | Kuna wanawake virukanjia na wengine wambeya. |
| *Aka ni mamithemba mingi,* | |

Ubeti huu unaeleza vile nyanya alivyokuwa akimuasa mwanaume huyu, naye anachukulia kuwa mzaha. Nyanya alimwambia kuwa kuna aina mbalimbali za wanawake, wapo wenye tabia ya umbeya, virukanjia, asherati miongoani mwa tabia nyingine. Kulingana na msanii huyu tabia ya mwanamke ni muhimu sana kwani wanajamii wanaamini kuwa ili ndoa iweze kudumu, mwanamke anastahili kutulia katika ndoa yake. Utafiti huu unakashifu maoni ya mtunzi huyu kwani kila mtu awe mume au mke anastahili kutulia katika ndoa. Dhima moja inayotekelezwa na nyimbo za sifo ni kumpa mtu au kitu sifa, ziwe nzuri au mbaya.

Katika jamii ya Wakamba mtu mwenye sifa nzuri ni yule mwenye maadili mema. Ikumbukwe kuwa kuna wanaume wasiotulia na mwanamke kwenye ndao. Akioa mwanamke, baada ya siku kadhaa anamtaliki na kuoa mwingine. Hata hivyo, inapokuwa ni mwanamke kutoka kwenye ndoa moja na kuanzisha nyingine, jamii inachukulia kuwa kosa nyepesi. kwa jicho. Masaibu yanayoweza kumpata mwanamume akawa akimwoa mke huyu na kumwacha yanaweza pia kumpata mwanamke. Kule kutotulia kwa Nzembi, msanii anakuona kuwa ni tabia ya uasherati. Anathibitisha haya anaposema;

| | |
|---|---|
| *Auma Kajiado ngamwiwila Kikuyu,* | Alipotoka Kajiado alitorokea Kikuyu, |
| *Atwaitwe ni mwikuyu,* | Aliolewa na Mgikuyu, |
| *Onakwo akalunjwa,* | Hata huku akatalikiwa, |
| *Nundu ni wa usavi, ni uko wa kitimba,* | Kwa sababu ya uasherati, |

| | |
|---|---|
| *Aka mailye ta indo* | Wanawake ni aina mbalimbali kama mifugo. |

Msanii huyu anasema kuwa, Nzembi alipoolewa Kikuyu, alipewa talaka kwa sababu alikuwa asherati na mbeya. Anazidi kuelezea kuwa wanawake ni wa aina mbalimbali kama mifugo. Wakati mwanamke anapojikomboa kutokana na dhuluma katika ndoa, anaonekana kuasi mila na tamaduni. Kwa nini naye mwanamume anapomtaliki mwanamke mmoja na kumwuoa mwingine asitazamwe hivyo? Kule kusema wanawake ni wa aina mbalimbali kama mifugo kunaonyesha dhana ya kudhalilishwa kwa mwanamke. Mwanamke anapojikomboa, hawezi kuwa sawa na mifugo. Yeye ni kiumbe razini si hayawani. Mwanamke ana uwezo wa kutoa maamuzi yoyote na kuyatekeleza.

Msanii huyu anaelezea tabia za Nzembi kuwa za kutotulia kwake. Alikuwa akiolewa na mwanamume anamtaliki na kwenda kwa mwingine. Anadhihirisha haya kupitia ubeti huu:

| | |
|---|---|
| *Ninye natwai Nzembi kuma ngaliko sya Emali,*<br>*Twavika kwakwa angeuka,*<br>*Twavika kwakwa angeuka,*<br>*Kai ni uko wa kilata na ni uko wa usavi,* | Nilimuoa Nzembi kutoka pande za Emali,<br>Tulipofika kwangu akabadili nia,<br>Kumbe alikuwa ni kirukanjia na mbeya. |
| *Auma vu kwakwa ngamwiwila Kajiado,*<br>*Atwaitwe ni Masai ii, una ku akalungililwa*<br>*Aka nima mithemba mingi,* | Alipotoka kwangu akahamia Kajiado.<br>Hata huko akatalikiwa kwani<br>Alikuwa kirukanjia, aina ya umbeya,<br>Wanawake na aina mbalimbali |
| *Auma Kajiado ngamwiwila Kikuyu*<br>*Atwaitwe ni mwikuyu, onakwo akalunjwa,*<br>*Nundu ni wa usavi, ni uko wa kitimba,*<br>*Aka mailye ta indo* | Alipotoka Kajiado alitorokea Kikuyu<br>Akaolewa na Mgikuyu,<br>Hata huku akapewa talaka,<br>Alikuwa muasherati,<br>Aina ya umbeya asiyetulia,<br>Wanawake ni aina mbalimbali kama mifugo |

Nzembi anawakilisha wanawake wa kisasa ambao wameasi mila na tamaduni zao kwani wametambua haki zao. Unawamulikia wanaume kuhusu hatari za kuoa wanawake wasiotulia kwani huenda ukawaletea majuto katika maisha ya baadaye.

Mwanamke kulingana na tamaduni za Wakamba anapaswa kushikilia majukumu yake ya kiuana hususan kuzaa, kulea watoto na kumtunza mume wake miongoni mwa majukumu mengine. Majukuma ambayo yamejaa taasubi ya kiume kwa sababu kwa mwanamke sio nyumbani peke yake hata ofisini anafaa. Msanii amemchora Nzembi kama mwenye tabia ya kutotulia. Kumsawiri huku kunamdalilisha mwanamke. Mwanamke anaweza kukosa utulivu kutokana na vikwazo vya mwanamume. Mwanamke anaonekana kujikomboa kutoka kwenye ndoa tofauti ambazo hatujaelezwa zilikuwa na hitilafu gani. Nzembi ni mhusika aliyepewa jina la kimajazi, neno '*nzembi'* humaanisha asiyetulia. Msanii huyu amemsawiri mwanamke kama asiyetulia. Kunao wanaume wasio tulia katika ndoa zao. Si wanawake tu wasiotulia, kwa hivyo matatizo yanayowafanya wanawake wasitulie yanaweza pia kuwakumba wanaume. Mwanamke asiyetulia asilaumiwe kabla ya kujua chanzo cha kutotulia kwake.

Uchunguzi huu umebaini kuwa, baadhi ya tabia za wanajamii zinakiuka maadili katika jamii husika. Wanajamii wanastahili kukumbatia yaliyo mema na kuachana na yaliyo maovu. Ni vyema iwapo wasanii watayaeleza yaliyo bayana ndiposa wanajamii waweze kuyaelewa. Katika ndoa yoyote ile panapotokea talaka panakuwa na sababu fulani. Mwanamke asiwe ndiwe wa kulaumiwa na kusawiriwa akiwa na mienendo isiyofaa jinsi alivyosawiriwa Nzembi. Ukombozi wa mwanamke unastahili kuwa ule unaomuauni shida zinazomkabili. Wanawake wanastahili kuelewa kuwa wakati wa sasa ni wa kuzalisha mali ili kuipa jamii mahitaji ya

kimsingi.Mwanamke akijikomboa anastahili kujihusisha na mambo yatakayomletea tija katika maisha yake.

Ugomvi ni mvurugano unaotokea baina ya watu kwa kutoelewana. Katika wimbo wa *Nyinya wa Syana* (Mama watoto), msanii anaonyesha ndoa iliyosheheni ugomvi baina ya mume na mke. Mama watoto ana tabia ya tamaa ya pesa na pia kumtukana mume wake asipomtimizia mahitaji ya kifedha. Kujibizana huku ni baadhi ya sababu ambazo zinasababisha mvurugano katika ndoa. Kwa hivyo msanii anahimiza uvumilivu katika ndoa. Mwanamke awe mvumilivu. Anaeleza haya kupitia ubeti huu:

| | |
|---|---|
| *Nyinya wa syana niki ndwikwiwa nthoni,* | Mama watoto mbona huna haya , |
| *Uingunuia maletho ngutwaite,* | Mama watoto mbona huna haya, |
| *Ndukinyange mbuleki,* | Ukinitolea ukali na nimekuoa, |
| *Noituvya kamunuka,kilomo* | Punguza mwendo, na uachane na kupayuka |

Mama watoto anaambiwa apunguze mwendo. Mume wake anamwuliza hata haya hana kwa kumtolea ukali akiwa mumewe. Mwanamke anaonekana kupewa nafasi ya pili katika jamii kwani mume huyu anamkumbusha kuwa ni yeye amemwoa. Mwanamke kupitia mawazo ya msanii huyu anahitajika kunyamaza kwani ameolewa. Mawazo ya msanii huyu hatukubaliani nayo kwa sababu mwanamke ni mwanajamii mwenye akili razini na ana haja ya kujinyakulia ukombozi wake. Suala la usawa katika jamii ni la kimsingi kwani wote wake kwa waume wanastahili kujitahidi kwa ushirikiano katika kupiga vita ubabedume. Mwanamke anaweza kutoa maoni ya maana ambayo yanaweza kusaidia katika ujenzi wa familia. Wote wawili mke na mume wanastahili kusikizana ili kufikia uamuzi.

Kutokana na tabia ya mama watoto kutotosheka na kile anachopewa na mume wake, mumewe anamtishia kuoa mke mwingine. Anamweleza haya kupitia ubeti huu

| | |
|---|---|
| *Kai wingenda nundu wa kwithiwa wina syana,* | Wanidharau kwa sababu ya watoto, |
| *Kotesi aume me mavinduka maingi,* | Hujui wanaume wana mipango mingi, |
| *No ndwae kakua mbunguo,* | Naweza kuoa mke mwingine |
| *Noitiwa ungethetye kiveti.* | Nikuache ukiduwaa mwanamke |

Ubeti huu unaeleza vile mwanamume huyu anamtishia mke wake kwa kumwambia anaweza kuoa mke mwingine. Kuoa mke wa pila sio suluhisho la shida zinazowakumba wanandoa, cha msingi ni wanandoa kutambua makosa yoa na kuyarekebisha.Wimbo huu unaonyesha baadhi ya wanawake wa kisasa ambao wamekataa kimya cha kulazimishwa na wanaume katika maisha yao. Kwa kiwango fulani, mtunzi amejaribu kujenga maudhui ya ndoa kuonyesha kuwa wanawake wako tayari kuchangia katika kustawisha ndoa zao. Mwanamke anajikomboa kutokana na kimya cha kulazimishwa katika kutoa maoni kuhusu masuala ya ndoa zao.

Ufeministi wa Kiafrika unapendelea ushirikiano kati ya wanawake na wanaume ili kuweza kuondoa mbali dhuluma za kijinsia. Hata hivyo, itambidi mwanamke mwenyewe kuwa mstari wa mbele kutetea haki zake. Msanii huyu anazidi kuelezea vile wanaume huwatishia wanawake wanapowaona wakiwa tayari kujikomboa. Maneno anayomwambia yanaashiria vitisho.

Mwanamume huyu anaona kuwa mama watoto amekuwa na kiburi kwa sababu ya watoto. Watoto hawa ni wao, kwa hivyo mwanamume huyu anastahili kujua kuwa ni jukumu lake kuwatunza watoto wale. Kumtishia mama watoto kuwa anaweza kuoa mke mwingine kunajenga taswira ya wanaume kudhani mke wa pili ni suluhu katika ndoa. Mume wake anamtaka awe mnyenyekevu. Utumwa huu wa mwanamke katika jamii ya Wakamba unamnyima uhuru wa kujiamulia. Taasubi ya kiume katika jamii nyingi za Kiafrika ilizua tafsiri na sifa ambazo zilimtazama mwanamke kwa namna iliyopotoka (Masinde, 2003). Mkabala wa kuumeni ulitawala jamii nyingi za Kiafrika na kuchangia kudunishwa na kupuuzwa kwa mwanamke.

Mwanamke anastahili kuwa mnyenyekevu iwapo mahitaji yake yote yatatimizwa. Mama watoto amesawiriwa katika ubeti huu kama mwanamke asiyetosheka na kile ambacho alipewa na mume wake. Mume huyu anawezakuwa alikuwa akimpa kidogo na ndio maana anadai zaidi. Isiwe wakati mwanamke anadai mahitaji yake, atasemekana ni kisirani. Msanii anazidi kumchora mama watoto kama ambaye hawezi kujiamulia mambo. Ubetu huu unaeleza hayo:

| | |
|---|---|
| *Ninguukulya na tei wambe kwisilya,*<br>*Kitumi nundu wilikywa kithekani,*<br>*Na itina nukuia we kiveti,*<br>*Na wathauka uyivyika matani.* | Ninokusihi kwa heshima ufikirie,<br>Kwa sababu unadanganywa na ni wewe<br>utapata shida |

Mwanamume huyu anadhani kuwa, kuna watu wanaomwingiza mke wake mashakani. Hii ndio maana anamrai kwanza afikirie kabla ya kufanya lolote. Anaona kule kudai mahitaji yake kumesababishwa na kufuata ushauri wa watu wengine. Ni lazima wanaume watambue kuwa wanawake wana fikra kama wanaume na wanaweza kutoa maoni yao binafsi na kuyafuata. Suala ibuka ambalo limekuwa nyeti katika maisha ya kisasa ni kuwa asasi ya ndoa imekumbwa na misukosuko mathalan ugomvi, vita, talaka na hata mauaji. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inamtaka mwanamke aikomboe nafsi yake kwa kujitegemea na kuweza kujiamulia mambo. Mwanamke mwenyewe anastahili kuwa mstari wa mbele ili kuikomboa nafsi yake mwenyewe.

Ndoa inawezesha mfumo wa ubabedume kukita mizizi katika jamii kwa kuwa inapelekea kuwepo kwa familia ambapo mwanamume ndiye kiongozi. Mwanamke anapoolewa hujipata chini ya uongozi wa mwanaume. Mambo yote anayofanya lazima yaidhinishwe na mume wake. Ili mfumo wa ubabedume uimarike vizuri, ni lazima kuwe na mtawala na mtawaliwa. Kwa kutokuwa na ndoa, mwanamume asingekuwa mtu wa kutawala, huenda mtazamo wake kuhusu mwanamke ungebadilika. Wanawake wanapoolewa wanajikuta katika familia zinazotawalwa na wanaume.

### 4.6.3 Uchumi

Virginia Woolf katika kitabu chake, *A Room of One's Own* (1928), analipa uzito suala la uchumi katika ukombozi wa mwanamke. Kulingana na Woolf, mwanamke hawezi kupata ukombozi wa aina yoyote kama hajakombolewa kiuchumi. Maisha ya mwanamke au mwanamume yanategemea hali ya uchumi. Hali ya uchumi ikiwa mbaya, maisha nayo yanakuwa mabaya.

Wafuasi wa Ufeministi wanawahimiza wanawake watafute njia za kuwawezesha kujitegemea kiuchumi. Mbinu wanazozipendekeza ni pamoja na kujiunga katika vikundi mbalimbali vya akina mama ili waweze kusaidiana na kuhimizana kiuchumi. Mwanamke anafaa asimame na kupinga ukandamizaji wa kiuchumi. Millet (1969:157) anaeleza kuwa mabadiliko ya kiuchumi yanawezekana kupitia kujiimarisha kwa mwanamke kijamii na kiuchumi.

#### 4.6.3.1 Mwanamke Mkamba Katika Biashara

Justus Myello katika wimbo wa *Aka* (Wanawake), anampa mwanamke nguvu za kiuchumi anapoeleza kuwa wanawake wanafanya biashara ndogo ndogo. Wanawake wengi katika jamii ya Wakamba hukimu mahitaji yao pamoja na ya jamii zao kupitia kufanya biashara ndogo ndogo. Mwanamke kwa mikono yake hufanya kazi kwa bidii ili asiwe mzigo kwa familia yake.

| | |
|---|---|
| *Aingi matatite maundu tuviasala ,*<br>*Vai kindu kivinya Ukamba ta kuea syana na*<br>*Kuta maluu na manga, mavokoto,*<br>*Mekiite vitii nongi kulungya ukya musyi,* | Baadhi ya wanawake huanzisha biashara ndogondogo,<br>Kama kuuza viazimbatata ndiposa waweze<br>Kuangamiza umaskini katika familia.<br>Jambo hili si rahisi katika jamii ya Wakamba |

Ubeti huu unamwonyesha mwanamke kama mchumi. Mwanamke ana uwezo wa kutafuta riziki ili aweze kuumaliza umaskini katika familia yake na jamii nzima. Kulingana na msanii huyu, wanawake wa jamii ya Wakamba wanaojaribu kujikomboa kiuchumi kwa kuuza viazimbatata,

mihogo na maparachichi. Kulingana na mtafiti ni kuwa hata kama biashara hii haina faida kubwa itamwezesha mwanamke kujitegemea pasi kumtegemea mwanamume kumkidhia mahitaji yake.

Wao husafiri mbali kutafuta bidhaa za kuuza. Kwa mfano katika masoko mengi kaunti ya Machakos likiwemo soko kuu la mji wa Machakos, wanawake wengi huwa wamebeba bidhaa zao kwa magunia. Wengine hutumia punda kubebea bidhaa hizo. Miongoni mwa bidhaa hizi ni zile ambazo ametaja msanii. Amesema wengine huuza maparachichi, mihogo, viazimbatata ili kukabiliana na hali ya umaskini. Hii ni hali halisi katika jamii ya Wakamba. Msanii anaeleza haya kupitia ubeti huu:

Jambo hili linaonyesha kuwa mwanamke anaweza kushiriki katika suala la uchumi. Msanii anaonyesha kuwa mwanamke habweteki tu, anaweza kujipatia riziki yake pasi kumtegemea mwanamume. Haya yanaibua taswira kuwa mwanamke si mtu wa kukaa nyumbani bali ana uwezo wa kuzalisha mali kwa ajili ya familia yake na taifa kwa jumla. Mali hii itamsaidia mumewe katika kugharamia baadhi ya mahitaji. Hivyo mke na mumewe watasaidiana katika uchumi wao.

Ukizuru soko kuu la Machakos mjini, kaunti ya Machakos, asilimia themanii (80%) ya wachuuzi hapa ni wanawake. Mtafiti alizuru soko hili akahesabu wachuuzi mia mbili na hamsini (250). Miongoni mwa hawa, wanaume walikuwa hamsini pekee (50) kwa asilimia, wanawake ni 80% na wanaume ni 20%. Kwa hivyo ni dhahiri kuwa sifa ya mwanamke wa Mkamba ni mchumi ni kweli. Jambo hili lilirejelewa katika masoko mbalimbali kama soko la Masii, Mutitini, Mitaboni, Wamunyu, Tala miongoni mwa masoko mengine katika kaunti ya Machakos. Katika kaunti nyingine za Ukambani kama Makueni na Kitui ilibainika kuwa wengi wa wachuuzi ni wanawake Wakamba.

Mifumo ya kiuchumi ya kikoloni iliwafanya Waafrika kushindwa kukidhi mahitaji yao na ya familia zao (Masinde, 2003). Hii ndiyo sababu baadhi ya wanawake wanashawishika kuuza miili yao ili wapate pesa. Hiki ndicho chanzo cha taasubi za kiume ambapo wanaume wanawachukulia wanawake kama vifaa vya kuwastarehesha, mradi wametoa pesa. Ukoloni kwa kiwango kikubwa ulikengeusha jamii za Kiafrika kwa kutoa uchumi wa pesa na kazi za kuajiriwa. Kutokana na mabadiliko ya kimaisha mapenzi yakaegemezwa kwa upande wa pesa.

Katika wimbo wa *Aka ma taoni* (Wanawake wa mjini) wanawake hawa wanaonekana kuthamini pesa za mapenzi kusudi lao kuu ni kupata pesa kutoka kwa wanaume. Haya yanadhihirika katika ubeti huu:

| | |
|---|---|
| *Mo masyaa ila ndia imbiie nikuka ingi ,* | Wao usema yule mjinga alinambia atarudi, |
| *Vata wakwa ni mbesa* | Haja yangu ni pesa |
| *Yafika ningumwnya* | Akifika nitamwonyesha. |

Katika ubeti huu, wanawake wamesawiriwa kama wapenzi wa pesa, wanasema haja yao ni pesa. Mwanamume anaonekana kuweka ahadi kuwa angerudi tena. Jambo ambalo linaonekana kutendeka mara kwa mara. Mwanamke anasawiriwa kuwa ndiye anayelipwa. Hata hivyo, tukiangalia kwa undani uhusika huu wa kufanya ngono huzishirikisha na kuzifurahisha jinsia za kike na za kiume. Kwa ushirikiano huo, tungeliunga mkono suala hili endapo jinsia zote zingeshirikiana kulipia starehe hiyo gharama. Hapa panazuka kudhalilishwa kwa mwanamke kwani mwanamume ndiye mlipa pesa kwa tendo walilolifanya pamoja kuashiria kuwa mwanamke ametumika kama chombo cha kumstarehesha mwanamume.

Msanii anaelezea kuwa wanawake hawa wa mjini wakiwaona wanaume na pesa, wanatafuta mbinu zozote za kuwapokonya. Wimbo huu unasheheni maudhui ya mapenzi ya siku hizi ambayo yanaelekea kuwa ya kununuliwa kwa pesa. Kazi hii wanayoifanya wanawake wa mjini

ni uchumi. Baadhi ya wanawake wamejijenga kiuchumi kupitia njia hii. Msanii anaeleza kuwa wanawake hawa husema haja yao ni pesa. Ubeti huu unadhihirisha haya:

| | |
|---|---|
| *Manya thina ni kwaku ,* | Fahamu shida ni kwako, |
| *Mwa mbee wa maisha maku,* | Kuhusu maisha yako, |
| *Elewa maiukulya,* | Wanawake hawa hawajali haja yao ni pesa |
| *Mo mesi tu kuya mbesa* | |

Wanawake hawa wanasemekana kutojali maisha ya yule anayewapatia pesa. Wao haja yao ni pesa. Pesa hizi wao huzitumia kukimu mahitaji yao. Katika hali halisi wanawake wengi wamejiendeleza kupitia biashara hii. Wengine wamejenga nyumba zao, wengine wamesomesha watoto na hata kununua mashamba miongoni mwa mambo mengine. Wanawake huiona tabia hii ya wanaume kuwa ya kijinga na ndio maana wao huwaita wajinga. Msanii anaeleza haya katika ubeti huu:

| | |
|---|---|
| *Mo masyaa ila ndia , imbiie nikuka ingi,* | Wao husema tule mjinga alisema atarudi tena, |
| *Vata wakwa ni mbesa, yavika ningumwyony'a* | Haja yangu ni pesa, akifika nitaonana naye |

Wanawake hawa kupitia ubeti huu, huwaona wanaume wakiwa wajinga. Wanasema yule mjinga alisema atarudi tena, akifika atakabiliana naye kwani haja yake ni pesa. Wanawake hawa si eti wao hufurahia kile kitendo bali wao huwa wanachuma mali. Wanaume ambao hurudi tena na tena huwafaidi. Hali hii ya kutafuta pesa kulingana na mtafiti ni duni kwanza huzusha hadhi ya mtu na pia inaweza kuchangia kuenea kwa magonjwa ya zinaa. Japo hii ni njia ya kuchuma mali, ni vyema wote wanawake na wanaume waelewe kuwa, ni vizuri kufuata maadili mema yatakayowawezesha kuishi maisha mema, kwani njia nyingine za kuchuma mali zinaweza kusababisha maafa katika jamii kama vile kuvunjia kwa ndoa, kifo, talaka na pia magonjwa ya zinaa ukiwemo ugonjwa wa UKIMWI. Utamaduni wa Wakamba hauruhusu tabia na mienendo ya aina hii. Zamani mwanamume aliruhusiwa kuoa wanawake wengi lakini si kwenda kufanya

mambo ya ukahaba na wanawake wengine. Siku hizi haya yameathiriwa na dini, teknolojia, siasa na mifumo mingine katika jamii.

Tabia za ufuska hazikubaliki katika jamii ya sasa kulingana na sheria za dini za Kikristo na Kiislamu. Dini ya Kiislamu ina msimamo mkali kuhusu ukahaba, jambo ambalo adhabu yake ni kifo (Quran, Sura 2:282). Katika Biblia Takatifu kitabu cha Matayo 19:9 inasema:

> Nami nawaambieni, mtu yeyote anayemwacha mkewe, isipokuwa kwa sababu ya uasherati, akaoa mke mwingine anazini.

Dini inakashifu vitendo vya uzinzi. Wanajamii wanastahili kujikomboa kutokana na vitendo viovu vinavyozusha hadhi na utu wa mtu. Japo wanawake hawa huwa wanatafuta mali ni vyema wakipata mtaji wakome kabisa kujihusisha na tabia hii na wachume mali kwa njia nyingine zilizo njema.

### 4.6.4 Ukombozi wa Mwanamke Katika Utamaduni

*Kamusi ya Kiswahili Sanifi* (2004), inaeleza kuwa, utamaduni ni mila, asili, jadi na desturi za kundi la jamii fulani. Makoti (2005) akimnukuu Mbiti (1969) anasema kuwa, utamaduni unapigwa vita na dini ya Kikristo na Kiislamu kuhakikisha umefifia. Makoti anahimiza tuudumishe na kuuthamini utamaduni wetu. Jamii ya Wakamba ina utamaduni wao unaowaongoza wanajamii. Maoni ya Makoti ya kudumisha utamaduni yanaungwa mkono na utafiti huu, kwa kuwa utamaduni mwema unadhibiti maadili katika jamii. Katika jamii zinazoshikilia mila na desturi, ni vigumu msanii kujinasua katika makucha ya mila hizi. Hawezi kusema yuko huru kuweza kuwa yakinifu akaihakiki jamii iliyomlea na kumkuza kwani msanii ni sehemu ya tabaka fulani.

Yule (1996) anaeleza kwamba utamaduni ni maarifa anayopata mtu kutoka kwa jamii. Kwa hivyo kila jamii ina mwonoulimwengu wake. Utamaduni ni muhimu katika kumfunza mtu itikadi za jamii na hutenga nafasi ya kila mmoja. Ni bayana kuwa kila binadamu hutoka katika utamaduni fulani ulio na miundo mbalimbali inayotumiwa kuwagawanya watu kwa misingi mbalimbali kama vile kijinsia na usawa. Kwa mfano, kulikuwa na majukumu yaliyotekelezwa na wanaume na pia ya wanawake.

Ndungo (1999) anaeleza kuwa utamaduni na malezi huchukua nafasi muhimu katika kuunda na kuimarisha itikadi na mielekeo ya jamii kuhusu wanawake, kwa hivyo utamaduni ndicho kitovu cha maisha ya binadamu. Twaona kuwa tamaduni nyingi humtaka mwanamke awe mnyenyekevu, myamavu, mpole na mtiifu wala asiwe na hiari katika maisha yake yote ya kujichagulia au kujiamulia lolote lile (Somba, 2000).

Siku hizi kutokana na mabadiliko ya maisha na kukengeuka kwa wanajamii, kutokana na utamaduni wa Kimagharibi, wanawake wameanza kujikomboa kutoka minyororo ya tamaduni zilizowafunga na zinazowapa nafasi ya pili katika jamii. Mwanamke kulingana na utamaduni wa Wakamba, anapaswa kushikilia majukumu yake ya kiuana kama vile kuzaa, kulea watoto na kumtunza mume miongoni mwa majukumu mengine. Wanawake wa jamii ya Wakamba wanaonekana kujikomboa kutoka tamaduni hizo. Wameanza kukataa kimya cha kulazimishwa na pia kufungwa kwenye ndoa zinazowadhulumu. Hali hii imewawezesha wanawake wa Wakamba kuwa na uwezo wa kujiamulia mambo na pia maisha pasi kumtegemea mwanamume.

Mwanamke kupitia wimbo wa *Syoka Mami* (Rudi Mama) anaonekana kuasi utamaduni wa kufungwa kwenye ndoa na badala yake kuamua kuanzisha maisha mapya. Msanii wa wimbo huu anaeleza haya.

*Mami niki watwathukiie na nengi noue watusyaie,*
*Niki watutie na ndadi wathi uendo,*
*Lilikana uyuma kwaku watavisye ndadi withi soko kumbe waina syaku wavangite utoloka*

Mama kwa nini ulitutelekeza na ni wewe ulituzaa,
Mbona ukatuacha na baba ukaenda kwenu,
Ulimdanganya baba kuwa unaenda sokoni,
Kumbe ulikuwa na mpango wa kutuacha.

Taswira hii imetumiwa katika wimbo huu ili kuibua uzito wa matatizo wanayoyapitia watoto, mwanamke anapouasi utamaduni. Watoto wanataka kujua ni kwa nini mama aliwaacha na kuwaachia shida na ni yeye aliyewazaa. Japo ni uamuzi mzito wa mwanamke kuwaacha watoto wake, inafikia wakati mwingine hana budi. Katika jamii ya Wakamba mwanamke anaporudi kwao ana hiari ya kwenda na watoto wake ama kuwaacha kwa mume wake.

Mama watoto katika wimbo huu aliwaacha watoto wake chini ya ulinzi wa mume wake. Kwenda kwake mjini ilikuwa ni njia ya kwenda kuchuma mali. Alienda kuishi na mfanyabiashara wa kuuza mabati. Mtoto wake anamrai arudi nyumbani. Ni muhimu kwa wanawake kujikomboa kiutamaduni lakini pia ni vyema kuweka kwenye mizani madhara ya ule ukombozi. Kwa mfano, kama mwanamke ataondoka kwenye ndoa yake na watoto wake waanze kuteseka, ni vyema kuondoka nao. Malezi ni jukumu la wazazi wote wawili. Mwanamke kuonekana kama mlezi pekee wa watoto ni kosa. Mwanamke pia ana haki ya kwenda kuchuma mali. Kwa hivyo, mwanamume anapoachiwa watoto anastahili kuwalea na kuwatunza vyema.

Vilevile wanawake wanaonyesha kujikomboa kutokana na tamaduni zilizowafunga kwa kuwataliki waume zao kurudi kwao.. Wimbo wa *Nyinya wa Ndetei* (Mama Ndetei) mwanamke anaonekana kujikomboa kutoka katika ndoa na kufanya hiari na kwenda kwao. Msanii anaeleza haya kupitia ubeti huu:

*Nyinya wa Ndetei, nyinya wa Nthiwa mami wa Koreta, nyinya wa syana ni ivityo yau yu nekie,*

Mama wa Ndetei, mama Nthiwa, mama wa Koreta, nakuuliza ni kosa gani nililokukosea,

| | |
|---|---|
| *Kuma wathi ona kavalua ndunandikia, Nakwikie ata mama, ko ve nai itaekeawa* | Tangu urudi kwenu hata barua hunitumii, Nilikufanya nini, hakuna dhambi isiyosamehewa |

Mwanamke huyu alimtaliki mume wake na akaondoka na watoto wake. Mume wake anamwuliza ni kosa gani alilomkosea. Mwanamume huyu anamtaka mke wake arudi nyumbani, naye Mama Ndetei ameamua kujikomboa kutokana na tamaduni zilizomfunga za kijadi kuwa mwanamke anastahili kuvumilia kwa mume wake hata hali ikiwa ngumu vipi.

Wanawake katika jamii nyingi za Kiafrika hawapewi haki ya kurithi kwani hawamiliki chochote. Anapoolewa anafanywa kuwa sehemu ya mali ya mumewe. Hali hii inasababishwa na ulipaji mahari kabla ya ndoa. Ingawa wanawake wengi waliteseka katika ndoa iliwabidi kuvumilia kwani kama sivyo mahari yao ingerudishwa kwa mume. Hata baada ya kifo cha mume, mke alihitajika kubaki katika familia ya mumewe. Urithi uliachiwa watoto wa kiume kwani waliaminiwa kuwa wao ndio sehemu ya ukoo. Mambo yanaonekana kubadilika siku hizi kwani wanawake wanaonekana kurithi mali ya wazazi. Kulingana na *Katiba ya Kenya* 2010, sura ya pili, ibara ya ishirini na saba inasema kuwa, wanawake na wanaume wana haki sawa ya kushughulikiwa kwa usawa ikiwemo haki ya kupata nafasi sawa katika shughuli za kisiasa, kiuchumi, kitamaduni na kijamii katika masuala yote pamoja na kuwa na mali au urithi.

Hakuna sheria, utamaduni au mila itakayokuwa halali ikiwa inawanyima wanawake au wanaume haki zao. Kwa hivyo, wanawake na wanaume wana haki ya kushughulikiwa kwa usawa ikiwemo haki ya kupata nafasi sawa katika shughuli za kisiasa, kiuchumi, kitamaduni na kijamii.

Katika wimbo wa *Kavola kavola Kamengele* (Polepole Kamengele) dada yake msanii anaonekana kurithi mali ya wazazi, kaka yake anaonekana kujisahili atakachorithi kutoka kwa

wazazi wake. Kwa mujibu wa wimbo huu, mwanamke anaonekana kuchukuwa hatua ya kujikomboa. Kule kurithi mali ya alikozaliwa ni jambo ambalo siku hizi limekuwa likijadiliwa kwani jamii imeanza kutambua kuwa mtoto ni mtoto awe wa kike au kiume. Msanii anaeleza haya kupitia ubeti huu*:*

| | |
|---|---|
| *Kavola kavola Kamengele, kwa nau na mwaitu nganengwa ki?* | Polepole Kamengele, kwa wazazi wangu nitarithi nini? |
| *Isu ni ng'ombe mukuthinza,* | Hao ni ng'ombe mnaochinja, |
| *Mukiya ngathi na ingengeto nakwa muinenga mavindi,* | Mkila minofu name mwanipa mifupa, |
| *Mwinenga mavindi ko ni ngiti.* | Mwanipa mifupa kwani mimi ni mbwa? |

Lugano (1989) anasema kuwa jamii nyingi za Kiafrika hupendelea wanawake wanaozaa watoto wa kiume. Anaendelea kudai kuwa unyonge wa mwanamke umemfanya kuwa kisingizio cha kila jambo bovu linalotokea katika ndoa. Wimbo wa *Kiveti Ngungu* (Mwanamke tasa) mwanamke tasa anafananishwa na mchawi, mchawi anapewa sifa ambazo hazikubaliki katika jamii. Jambo hili linaonekana kuota mizizi ambayo itachukuwa muda kuing'oa. Hata wanawake wenyewe wameikubali hali hii jinsi ilivyo. Kwa mujibu wa Wamitila (2002:160);

> Utamaduni umeundwa au kujengwa kwa namna inayomkandamiza mwanamke katika nyanja zote za maisha. Wanawake wanapokulia katika jamii zao wanayachukua mawazo yanayoendeleza itikadi hii hasi na kwa njia hii kuidharau jinsia yao wenyewe.

Utamaduni anamokulia mwanamke unaonekana kuchangia katika kumdidimiza na kumfanya kuwa mnyonge zaidi. Wanawake wanastahili kuwa mstari wa mbele kutetea nafasi zao.

Wanapaswa kupiga vita tamaduni zinazowakandamiza na kukumbatia tamaduni zinazowajenga. Jamii ikiwemo jamii ya Wakamba, inastahili kufahamu kuwa, mwanamke ana uwezo wa kujiamulia mambo. Asiwe tu kila wakati anatakikana awe mnyamavu, mpole na mtiifu na asiwe na hiari katika maisha yake.

Hivyo basi, Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika haina budi kuzama katika mila, desturi na kaida za kijamii ili ibainishe usawiri wa mwanamke na uwezo wake katika utendakazi sambamba na anavyofanya mwanaume. Pia kuangalia dhuluma atendewazo mwanamke katika ufanisi wake kulingana na jinsi ulimwengu ulivyo.

**4.6.5 Uongozi**

Mfumo dume umetawala katika vyama vya siasa na jamii kwa jumla kumuona mwanamke kama kiumbe asiye na uwezo wa kuwa kiongozi, na mwenye mamlaka hayo ni mwanamume pekee. Baadhi ya wanawake wana karama ya kutoa maoni yao yakasikizwa, mitazamo yao ikazingatiwa na maoni yao kufikiriwa na kufanyiwa kazi. Hofu ya mwanamke kuwa nyuma katika kugombea nafasi kwenye majimbo dhidi ya waume inazidi kutanda, huku baadhi ya wadau wa maendeleo ya demokrasia, zikiwemo asasi za kiraia na jumuiya za kimataifa, zikiwataka wanawake kuamka ili kupambana na wanaume katika ngazi za juu kabisa za uongozi. Wanawake ndio wadau muhimu katika shughuli nyingi zikiwemo za kisiasa na maendeleo, kutokana na idadi yao kama wapiga kura.

Katika miaka ya nyuma wanawake wengi nchini Kenya walikuwa wanaogopa kujiingiza katika masuala ya siasa na badala yake wakageuka kuwa wapiga kura tu. Nchini Kenya tunaweza kusema kuwa japo wanawake wamebaki nyuma katika kuwania viti mbalimbali, dalili za mwamko mpya zinaendelea kuonekana polepole. Katika Bunge la kumi na moja

wanawake walijitokeza na kunyakuwa nafasi za ugavana, ikilinganishwa na Bunge zilizotangulia.

Kenya imepiga hatua kuhakikisha kuwa wanawake wamepata hatamu za uongozi katika nyanja za kisiasa. Katika uchaguzi wa 2017 idadi ya viongozi wanawake waliochaguliwa iliongezeka. Wanawake watatu walichaguliwa kama magavana. Wanawake hawa magavana ni: Joyce Laboso, Gavana Bomet, Ann Waiguru, Gavana Kirinyaga na Charity Ngilu, Gavana Kitui. Vile vile wapo wanawake waliochaguliwa kama maseneta ambao ni Margaret Kamar, Seneta Uasin Gishu, Dullo Fatuma, Seneta Isiolo na Susan Kihika, Seneta Nakuru. Viti vya ubunge vya wanawake pia viliongezeka ikilinganishwa na uchaguzi wa 2013. Hata hivyo, wanawake na uongozi ungali chini lakini haya yanaonyesha kuwa wanawake wamepiga hatua.

Umoja wa Afrika (AU), kwenye tamko la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) la jinsia na maendeleo la mwaka 2008 pamoja na mkataba wa nyongeza wa haki za wanawake wa mwaka 1995, ilidhihirika kuwa wanawake wana uwezo wa kushiriki katika uchaguzi kama wapiga kura na wagombee nafasi mbalimbali za uongozi. Ni jukumu la mwanamke kujitolea kugombea nyadhifa za kisiasa na uongozi badala ya kutarajia kuonewa imani na wanaume. Kwa sababu wanawake wanaunda asilimia kubwa ya wapiga kura nchini Kenya, wanastahili kuungana na kuchagua viongozi wanawake.


Watunzi wa nyimbo hizi hawajagusia suala hili kwa kina. Justus Myello katika wimbo wa *Aka* (Wanawake) anaeleza kuwa wanawake wanazo nyadhifa kubwa lakini hajafafanua ni nyadhifa za aina gani. Anaeleza haya kupitia ubeti huu:

*Yuyu nooka nine nasye aka ithi twi kw'o,*
*Na tunengetwe utonyi ni mumbi witu,*
*Akili na kisomo tutuite nasyo,*
*Ona maovisi manene tutua kw'o*

Naimba nikisema kuwa, wanawake
tumepewa uwezo na Mwenyezi Mungu,
Akili tambuzi , masomo tunayo na vyeo
vikubwa

Utafiti huu umetambua kuwa, wanawake bado wanahitaji kujiamini ndiposa waweze kunyakuwa nyadhifa za kisiasa hapa Kenya na kote ulimwenguni. Msanii huyu anasema wanawake wamepewa uwezo na karama kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Mwanamke anastahili kutumia kipawa chake kunyakuwa uongozi katika nyadhifa mbalimbali za uongozi.

**Grafu (i):** Maudhui yanayotathimini hali halisi ya mwanamke katika jamii ya Wakamba




Nyimbo zote tulizozichunguza, zimedhihirisha maudhui ya elimu, ndoa, uchumi, utamaduni na uongozi. Katika maudhui haya, elimu na ndoa zimegusiwa zaidi (40%), ikifuatwa na utamaduni (30%). Uchumi umegusiwa katika kiwango cha asilimia ishirini (20%) . Uongozi ndio umechukua kiwango cha chini kabisa (10%). Kulingana na grafu hii nafasi ya mwanamke bado ni finyu. Masuala yanayomthamini mwanamke ili aweze kujikomboa hayajafikia asilimia hamsini. Eimu na ndoa ni miongoni mwa masuala yanayopewa uzito kulingana na maudhui ya nyimbo za sifo za Wakamba zilizotafitiwa. Mwanamke ameonyesha kupiga hatua kielimu, katika nchi ya Kenya. Serikali imetangaza elimu ya bure kwa kila mwanafunzi. Kwa hivyo mwanamke anao uwezo wa kujiendeleza kupitia elimu. Baadhi ya wanawake kulingana na wasanii hawa wanatambua elimu ya watoto wao na pia wao wenyewe wameweza kupata elimu kama alivyoeleza msanii Bosco Mulwa. Kulingana na msanii Justus Myello wanawake wana akili tambuzi waliotunukiwa na Mwenyezi Mungu.

Masuala ya uchumi na uongozi yanaonyesha kuwa mwanamke bado hajapiga hatua kubwa. Kenya imepiga hatua kuhakikisha kuwa wanawake wamepata hatamu za uongozi katika nyanja za siasa. Wanawake wanastahili kutambua kuwa ni jukumu lao kujitokeza kugombea nyadhifa za siasa na uongozi badala ya kutarajia kuonewa imani na wanaume.

## 4.7 HITIMISHO

Sura hii imejikita katika Uwasilishaji na Uchanganuzi wa data ambao ulifanywa kwa mujibu wa madhumuni mahususi yaliyobainishwa katika utafiti huu. Imebainika kuwa mwanamke ni mwanadamu mwenye uwezo mkubwa wa kutenda matendo mbalimbali ambayo hugawanywa katika sehemu mbili kuu. Matendo mema (chanya) na matendo maovu (hasi). Mtafiti ametambua kuwa mwanamke ameanza kujikomboa kutokana na hali mbalimbali za kijamii, kiuchumi ,kisiasa na kitamaduni. Hii inamaanisha kuwa mwanamke ni mhusika anayekwenda sambamba na mabadiliko ya wakati. Sura inayofuata inahusu Hitimisho na Mapendekezo.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 UTANGULIZI

Utafiti huu ulilenga kuchunguza usawiri wa mwanamke katika nyimbo za sifo za Wakamba. Kwa kuongozwa na nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, ulijikita katika eneo la Afrika, katika jamii ya Wakamba nchini Kenya. Hii ni kwa sababu nyimbo zenyewe zimetungwa katika mandhari ya Kiafrika. Sura hii imeshughulikia muhtasari wa hitimisho ya sura zilizojadiliwa katika tasnifu na mapendekezo ya mtafiti. Matokeo ya utafiti huu kulingana na malengo pia yanashughulikiwa. Yale yaliyobainika kutokana na uchanganuzi wa nyimbo za sifo za Wakamba yameshughulikiwa. Katika sura hii mapendekezo yametolewa ya kuwafaidi watafiti wa baadaye.

## 5.2 HITIMISHO

Kwa jumla watunzi wa nyimbo hizi za sifo za Wakamba wamejadili suala la ukandamizaji wa mwanamke na pia uwezo wake katika jamii. Mwanamke ni binadamu kama walivyo wanaume. Ni mwenye uwezo mkubwa wa kutenda matendo mbalimbali ambayo hugawanywa katika sehemu mbili kuu, matendo mema (chanya) na matendo maovu (hasi).

Nyimbo hizi kumi zinaakisi maisha ya sasa na kuhusisha matendo ya jamii ya leo na kumfanya mwanamke aonekane amebadilika zaidi tofauti na zamani. Hii inamaanisha kuwa, mwanamke ni binadamu anayekwenda sambamba na mabadiliko ya wakati, historia, kisiasa, kiuchumi na kijamii. Hali hii inamfanya aonekane mwenye thamani. Wasanii wa nyimbo hizi za sifo za Wakamba wameangalia taswira ya mwanamke katika nyanja zote za maisha, yaani kiuchumi, kijamii, kisiasa na kitamaduni. Kila msanii ameichora taswira ya mwanamke

katika mtazamo wa mwonekano anaopenda na kuamini. Usawiri chanya umepewa uzito na watunzi wengi. Kwa hivyo, jambo hili linaonyesha kuwa wanaume katika jamii ya Wakamba wameanza kuelewa mchango wa mwanamke katika jamii.

Mwanamke anafaa apewe nafasi anayostahili katika jamii lakini ikumbukwe kuwa anapopewa nafasi hiyo, bado anabakia kuwa mwanamke na hawezi kuwa mwanamume. Pia, mwanamke akipewa nafasi katika jamii, hafai kumdunisha mwanamume kwani wanafaa kufanya kazi pamoja ili kuiendeleza jamii kwa jumla. Usawa kati ya wanawake na wanaume ni suala la haki za kijamii na ni jambo la msingi katika kuleta amani na maendeleo katika jamii.

Katika karne hii ya ishirini na moja (21), wanawake watahitajika kutafsiri kwa usahihi jinsi gani maisha mema ya kibinadamu yanavyostahili kuwa na kupiga hatua kimaendeleo. Utafiti umebaini kuwa, wanawake wana uwezo wa kuchuma mali, wameelimika, wana uwezo wa kuongoza na pia wameanza kujinasua kutoka kwa dhuluma nyingi zilizowafunga. Kwa hivyo, ili wanawake waweze kutimiza wajibu wao ipasavyo popote pale walipo, hawana budi kujitahidi kushiriki kadri wanavyoweza katika masuala ya kijamii.

Kwa mujibu wa nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, mwanamke ana mchango mkubwa katika maendeleo ya mataifa ya Kiafrika na dunia nzima kwa jumla. Hivyo basi mwanamke ana uwezo mkubwa wa kushika nafasi mbalimbali ndani na nje ya nchi husika. Uchunguzi huu kupitia data zilizokusanywa umebaini kuwa, thamani mojawapo kubwa ya wanawake ni kujitambua na kuweza kuwa na msimamo thabiti juu ya haki zake na familia na pia katika nafasi ya uongozi. Jambo hili litamjenga kufikia malengo makubwa ya maendeleo kwa jamii zetu za Kiafrika na ulimwengu kwa jumla.

### 5.2.1 Matokeo ya Utafiti

Baada ya hatua za uchambuzi kukamilika, matokeo ya utafiti huu yalipatikana na kuelezwa kwa mujibu wa madhumuni mahsusi ya utafiti huu. Katika madhumuni mahsusi ya kwanza nay a pili, uchunguzi umebaini kuwa, nyimbo hizi za sifo za Wakamba zimemsawiri mwanamke katika hali mbili, hali chanya na hasi. Katika usawiri chanya, mwanamke ameonyeshwa ni muwajibikaji, mlezi wa familia, mwenye mapenzi ya dhati, mkombozi na mshauri mwema.

Kwa kiasi kikubwa, utafiti umegundua kwamba, nafasi ya mwanamke kama mlezi wa familia imepewa kipaumbele. Ulezi ni ngome na mhimili wa mwanamke na hauepukiki hata akiwa na cheo gani. Hii ndiyo nafasi yake adhimu. Katika hali zilizo hasi, mwanamke amesawiriwa kama: mshirikina, muasherati, mwenye tamaa, mgomvi na mtu wa mipango na hadaa. Hali hizi zote, chanya na hasi zinahakisi hali halisi ya mwanamke katika jamii ya Wakamba karne hii ya ishirini na moja.

Madhumuni ya tatu ni kutathimini kama jamii ya Wakamba imebadili mawazo na kumsawiri mwanamke kama binadamu sawa na mwanamume kupitia maudhui ya nyimbo za sifo za Wakamba. Kupitia utafiti huu, ilibainika kuwa, kuwepo kwa mfumo rasmi wa elimu, mifumo mipya ya uzalishaji mali, dini, maswala ya kiuchumi na kijamii miongoni mwa mengine, kumeathiri maudhui ya nyimbo za sifo za Wakamba. Hii ni kutokana na sababu kwamba, msanii huongozwa na matukio na historia ili kuteua maudhui.

Maudhui yaliyoshughulikiwa katika utafiti huu ni pamoja na elimu, ndoa, utamaduni, uongozi na uchumi. Utafiti huu umegundua kuwa nafasi ya ukombozi wa mwanamke katika maswala haya imepiga hatua japo kidogo. Mwanamke amekuwa mchumi anayetafuta njia

mbalimbali za kujikimu pamoja na familia yake. Vile vile mwanamke amepiga hatua ya kujikomboa kutokana na ndoa zenye dhuluma. Katika uongozi, nafasi ya mwanamke ni finyu. Ni msanii mmoja aliyeonyesha nafasi ya mwanamke kama kiongozi. Hata hivyo katika hali halisi nchini Kenya, bado nafasi ya mwanamke uongozini ni finyu. Lengo la nadharia ya Ufeministi lilikuwa ni kuondoa unyanyasaji wa kijinsia hasa kwa wanawake. Hivyo basi, malengo ya Ufeministi yalijikita katika kumnasua mwanamke kutoka pingu za kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kijamii. Malengo haya ndiyo yanayoleta ukinzani wa maisha halisi ya mwanamke wa Kiafrika. Mfumo wa uzalishaji mali haumpi nafasi mwanamke katika kuzalisha na kugawa mapato sawa na mwanaume. Kwa upande mwingine wanaume ndio wamiliki wakuu wa mapato yatokanayo na uzalishaji mali.

Mtafiti amegundua kuwa, mwanamke ni binadamu kama walivyo wanadamu wengine kwa hivyo ana uwezo wa kutenda matendo ambayo hugawanywa katika sehemu mbili kuu. Matendo mema (chanya) na matendo maovu (hasi). Baadhi ya sifa chanya alizopewa mwanamke ni pamoja na kuwa muwajibikaji, mlezi wa familia, mshauri mwema, mchumi, mwenye mapenzi ya dhati na mkombozi. Uchunguzi umebaini kuwa masuala ya mwanamke kama mkombozi na mlezi wa familia yamepewa uzito. Mwanamke vile vile ametazamwa kwa upande hasi, baadhi ya sifa hasi alizopewa mwanamke ni; muasherati, mgomvi, mwenye mipango na hadaa, mwenye tamaa na mshirikina. Suala la tamaa limejitokeza kwa kiwango kikubwa katika usawiri hasi.

Maudhui yaliyojadiliwa yameonyesha kuwa, kwa kiwango fulani mwanamke ameanza kujikomboa japo polepole. Jambo hili limeonyesha kuwa mwanamke katika jamii ya Wakamba ameanza kujikomboa na kwenda sambamba na mabadiliko ya wakati. Utafiti

umebaini kuwa, nafasi ya uongozi bado ni finyu. Kwa upande wa utamaduni, mwanamke ameonekana kukandamizwa kwa kuonekana hana mamlaka ya kurithi mali ya wazazi na pia ya mume wake. Mwanamke anaonekana kujikomboa kutokana na ndoa zinazomdhulumu.

## 5.3 MAPENDEKEZO YA UTAFITI

Kutokana na utafiti huu, kuna haja ya kufanya utafiti zaidi. Tukinzingatia kuwa wanawake wengi wa karne ya sasa wamekengeuka na kuathiriwa na kasumba ya kimagharibi katika viwango vyote vya maisha kwa sababu ya masomo na utandawazi. Mtafiti anaamini kwamba, ametoa mchango kupitia utafiti kuhusu usawiri wa wanawake katika nyimbo za sifo za Wakamba. Hata hivyo, kwa upande mwingine anaamini kuwa, hakuna utafiti unaoweza kukamilisha kila jambo. Kutokana na hali hiyo, anapendekeza yafuatayo:

i) Mjadala unaoibuliwa na tasnifu hii si wa mwisho. Kuna maswala ambayo hayakushughulikiwa katika tasnifu hii na ni muhimu yashughulikiwe na watafiti wengine. Usawiri wa nyimbo za sifo ni swala ambalo litahitajika kufanyiwa utafiti zaidi katika jamii nyingine. Utafiti huu umeshughulikia nyimbo kumi za sifo za Wakamba zilizotungwa na watunzi wa kiume pekee. Mtafiti mwingine ashughulikie nyimbo za watunzi wengine ili kufikia uamuzi faafu wa mjadala wa watunzi wa kiume. Pia, mtafiti mwingine anaweza kuangalia usawiri wa wanawake katika nyimbo za sifo zilizotungwa na watunzi wa kike pekee au utafiti linganishi.

ii)Mtafiti anapendekeza utafiti kufanywa katika jamii nyingine utakaoangazia watunzi wa kiume wa nyimbo za sifo jinsi wanavyowasawiri wanawake ili kuona kama kuna mabadiliko yoyote katika usawiri wa mwanamke katika jamii nyingine kando na Wakamba. Utafiti

linganifu wa nyimbo za sifo za Wakamba unaweza kufanywa katika miaka ya 1970 au kabla ya karne ya ishirini na moja na ya sasa.

iii) Mtafiti anapendekeza wanaharakati wa masuala ya haki za wanawake wawe mstari wa mbele kuwapa elimu wanawake juu ya ukombozi wao. Elimu hii itasaidia wanajamii kuondokana na mawazo potofu ya kusema kuwa nafasi aliyopewa mwanamke ni mapenzi ya Mungu na ndivyo stahili yake. Elimu itawawezesha wanawake kufahamu jinsi ya kukabiliana na changamoto zinazowakumba hasa baada ya kujikomboa.

Elimu itawawezesha wasanii na wanajamii kujenga mawazo mapya na kutoa fursa sawa kwa wote na kufanya mwanamke aondokane na unyonge unaosababishwa na utamaduni wenye kubeba mila potofu. Mwanamke atakapohamazishwa vizuri, ataelewa kuwa tatizo kubwa sio kushindana na wanaume tu, bali pia ni jinsi gani ya kujenga fikra mpya na kusaidia kujenga upya mfumo wa jamii ambao umewafunga watu wote, wanawake kwa wanaume.

## 5.4 MCHANGO WA UTAFITI

Utafiti huu utakuwa na mchango mkubwa katika fasihi simulizi ya ulimwengu na Kiafrika kwani utachangia kuhifadhi kipera cha nyimbo za sifo katika maandishi kwa faida ya vizazi vya kesho. Mtafiti anayefanya utafiti wa nyimbo za sifo katika jamii yoyote ile atanufaika na utafiti huu. Kwa wasomi utawapa mwelekeo wa uelewa jinsi ya kuchanganua masuala ya kijinsia kitaaluma. Jamii ya Wakamba wanaposoma utafiti huu watapata maoni ya mwanamke wa Kikamba anavyosawiriwa na kumpa maono tofauti na alivyosawiriwa hapo zamani. Pengine anaweza kuwa na mtazamo mpya juu ya mwanamke wa kikamba katika karne hii ya 21. Vilevile, utakuwa wa umuhimu kwa wanawake ili kuwatia hamasa kubadili hali zinazowapata.

## MAREJELEO


Andrew, F.& Salvadori, S. (1980). *Peoples and Culture of Kenya*. Naorobi: Primrose Sundries

Beauvoir, S. (1949). *The Second Sex*, London: Pan Book Publishers.Chesaina, C. (1991*)* *Oral Literature of Kalenjin.* Nairobi: Printing Industries.

Chacha, N. C. (1986), "Mazingira ya Mwanamke Katika Fasihi ya Kiswahili: Rosa Mistika wa E. Kezilahabi", Katika Mwamko, Na. 3.

*Daily Nation*, August 1, 2016 "Heavy price for childless marriage" uk 8.

*Daily Nation*, August 2, 2018 "Assaulted woman in viral video to get aid" uk 3.

Eagleaton, M. (1986). *Feminist Literary Theory. A Reader*. Malden: Blackwell Publishing *Encyclopeadia Americana Volume 6*

Enon, J. C. (1998). *Education Research Statistics and Measurement*. Kampala: Makerere University Press.

Fakih, S. J (2017). "Kutathimini Mabadiliko ya Usawiri wa Wanawake katika Riwaya ya Utengano na Kamwe Si Mbali". Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (Haijachapishwa)

Finnegan, R. (1970*). Oral Lterature in Africa*. London: Oxford University Press.

Hymes, D. (1974). *Foundations in Social Linguistics: An Ethnographic Approach*. Philadelphia: University of Pennsylvania Press.

Katola, E. (2006) "Udhalimu dhidi ya Wahusika wa kike katika Tamthilia za Kiswahili". Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Kaui, M. (2008). "Usawiri wa Vijana katika Tamthilia teule za Kiswahili." Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haichachapishwa)

Kieti, M. (1999). Myali Songs. Social Critique among the Kamba. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. *(* Haijachapishwa)

Kieti, M. na Coughlin, P. (1990). *Barking. U wili Be Eaten! The Wisdom of Kamba Oral Literature,* Nairobi: Phoenix Publishers.

Kilauni, N.M. (2007). "Usasa katika nyimbo za Itheke". Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Kimilu, D. (1962). *Mukamba wa w'o*. Nairobi: East Africa Literature Bureau

King'ei, K. (1982). Uhakiki wa *Nthimo* (methali) za Kikamba kwa kufuatisha misingi ya Methali za Kiswahili. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

King'ei, K. na Kisovi, C. (2005). *Msingi Wa Fasihi Simulizi.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Kitavi H.M. (1992). "A Comparative Study, the Kitui North and Machakos Dialects of Kikamba." UoN: MA thesis. (Haijachapishwa)

Kothar, C. R. (2004). *Research Methodology; Methods and Techniques*, New Delhi: Wisha Prakashan.

Lugano, R. (1989). Mwanamke katika Riwaya za Kezilahabi. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Lyatuu, J. (2011). "Usawiri wa Wanawake katika Fasihi ya Kiswahili; Ulinganifu wa Waandishi wa Kike na wa Kiume, Uchunguzi katika Riwaya Teule." Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Maingi, H. (2007). "Upembezwaji wa Mwanamke katika Utenzi wa Fatumah." Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Makoti, V. S. (2005). *Across Borders; Benefiting from Cultural Differences. Digo Death and Funeral Songs*. Naorobi: DAAD.

Masinde, E. W. (2003). "Usahairi wa Kiswahili: Maendeleo na Mabadiliko ya Maudhui."Tasnifu ya Uzamifu Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Massamba, D. (2009). *Kamusi ya Isimu na Lugha, Falsafa ya Lugha.* Dar es Salaam: TUKI.

Matteru, L. B. (1981). *Fasihi Simulizi na Uandishi. Makala ya Semina ya Waandishi wa Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Mathooko, P.M (2004). "An Intergrated Perspective of Language Accomodation; A Case Study of Kikamba and Kitharaka". PhD Thesis Kenyatta University. (Haijachapishwa)

Mbatia, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*, Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishing.

Mbarwa, H. (1989). *Your Oral Literature*. Nairobi: Kijabe Printing Press.

Mbiti, J.S. (1991). *African Religion and Philosophy*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Millet, K. (1969). *Sexual Politics*, London: Virago.

Mirikau, S. (2011). "Taswira ya Mwanamke katika Tamthilia za Wamitila." Tasnifu ya Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Momanyi C. (2002*). "*Utafiti wa Kiswahili na Maswala ya Kiuana" Katika toleo la Inyani Simala- *Utafiti wa Kiswahili* Moi University, Eldoret: Moi University Press.

Msokile, M. (1993*). Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: EAEP Ltd.

Morris, P. (1997*). Literature and Feminism*. USA: Blackwell Publishers Ltd.

Mugenda, O. and Mugenda A. (1999). *Research Methods, Quantitative and Qualit*ative *Approaches*, Nairobi: Act Press.

Mwai, K. W. (1997). "The Power of Songs for Swahili Woman. Contesting social Death." Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Musyimi, D. M. (2011). "Maana za majina ya watu katika jamii ya Wakamba." Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Nandwa, J. & Bukenya, A. (1983). *African Oral Literature for Schools*. Nairobi: Longman.

Naomi, N. M. (2016). "Mabadiliko ya Maudhui katika Nyimbo za Jando Mfano Kutoka Jamii ya Wakamba. Tasnifu ya uzamifu Chuo Kikuu Cha Mount Kenya. (Haijachapishwa)

Ndeti, K. (1972*). Elements of Akamba Life*, Nairobi: East African Publishing House.

Ndungo, C. (1985). "Wanawake na mabadiliko ya Kihistoria Katika Fasihi ya Kiswahili." Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Ngugi Wa Thiong'o (1993). *Moving the Centre. The Struggle for Cultural Freedoms*. London: James Currey.

Njogu, K. na Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi. Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nurse, D. & Spear, J. (1984). *The Swahili Reconstructing*: *The History and Languages of African Societies*. 1800-1850. Philadelphia, University of Pennysylvania.

Nyangweso, S. M. (2017). "Nafasi na Athari ya Kiongozi wa Kike katika Tamthilia Teule." Tasnifu ya Chuo Kikuu cha Masai Mara. (Haijachapishwa)

Nzioki, S. (1982). *People of Kenya.The Akamba*. Nairobi: Evans Brothers.

Ogundipe-Leslie, O. (1994). *"African Women, and Critical Transformations;* Trenton, African World Press.

Ruto, M. C. (2015). "Matatizo ya Wanawake katika Kidagaa Kimemwozea na Nyuso za Mwanamke". Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Senkoro, F. M. (1989). *Fasihi na Jamii*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Shitemi, L. N. na wenzake (2008*). Nadharia katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika,* Eldoret: Moi University Press.

Simiyu, F.W. (2007*). "*Nyiso za Wabukusu". Maudhui na Lugha.Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Somba, J. N. (2000). *Ndeto sya Thome*. Kangundo: Somba Publications

Steady F. C (1981*). The Black Women Cross-Culturally*, Cambridge: Schenkam Publishing Co. Inc.

The Bible Societies (1971). *The Holy Bible*. New York: Collins Bible

TUKI, (2004*). Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.

Wafula R. M na Njogu K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*, Nairobi: Jomo Kenyattta Foundation.

Wambua, S. (2001). "Mtindo namatumizi ya Lugha katika nyimbo za Kakai Kilonzo." Tasnifu ya Uzamili Chuo K ikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Wamitila, K. (2002). *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers

Wamitila, K. W. (2003*). Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia*, Nairobi: Focus Publishers.

Wathome, R. (2009). "Mtindo Katika Nyimbo za Jamii ya Wakamba wa Masaku ya Kati." Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Watuma, B. W. (2011). *Mukamba na Syithio Syake*. Naorobi: Sengani Publishers.

Wollstonecraft, M. (1792*). A Vindication of the Rights of Women*, London: Forgotten Books.

Woolf V. (1929*). A vindication, A Room of One's Own*, London: Hogarth.

Yalwala, P. (1991). "Maudhui katika nyimbo za John Mwale." Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Nairobi. (Haijachapishwa)

Yego, E. (2003). "Nafasi ya Mwanamke na Jinsi Inavyotetewa Katika Nyimbo za Taarab za Zanzibar". Tasnifu ya Uzamifu Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Yule, G. (1991). *Pragmatics.* Oxford University Press

**KIAMBATISHO I**

HOJAJI YA WANAJAMII

Jina langu ni Kimondiu Dorcas Kasiva. Ninafanya utafiti ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili wa Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Machakos juu ya Nafasi ya Mwanamke na Jinsi Anavyosawiriwa katika Nyimbo za Sifo za Wakamba. Naomba uchukue fursa hii kuijaza hojaji hii.Toa habari za kweli bila woga wowote.Usiandike jina lako. Habari zote zitashughulikiwa kama siri na kwa sababu za kiusomi pekee.

**Sehemu ya kwanza**

1. Umri wako (age)

   a) 20-30 ( )

   b) 31-35 ( )

   c) 36-40 ( )

   d) 40 na zaidi

2. Jinsia yako (gender)

   a) Mwanamume ( )

   b) Mwanamke ( )

3. Kiwango cha elimu

   a) Elimu ya msingi ( )

   b) Elimu ya sekondari ( )

c) Elimu ya chuo cha anuwai (  )

d) Chuo kikuu (  )

**Sehemu ya pili**

1. Je, ni sifa gani anazopewa mwanamke kupitia nyimbo za sifo za Wakamba zilizotungwa na wanaume kama vile Wanginga, Bosco Mulwa miongoni mwa wengine?

___________________________________________

___________________________________________

___________________________________________

2. Mwanamke amasawiriwa namna gani kupitia nyimbo za sifo zilizotungwa na watunzi wanaume kama vile John Muasa, Bosco Mulwa na wengine?

___________________________________________

___________________________________________

___________________________________________

**Sehemu ya tatu**

1. Unafikiri jamii ya Wakamba imebadili mawazo na kumpa mwanamke nafasi yake kama binadamu ajiwezaye kupitia maudhui ya nyimbo hizi.Toa maoni yako ____________

___________________________________________

___________________________________________

___________________________________________

**KIAMBATISHO II:**
**Wimbo wa Bosco Mulwa (Mama)**

| KIKAMBA | KISWAHILI |
| --- | --- |
| *Mother ii mother mwa ndikolwa nue,*<br>*Mother ii mother ii noue mwendwa wakwa,*<br>*Niwaa muyo nalilikana mathina ala woonie yila nai kana,*<br>*Wanzyaie ni munii mother Susana,*<br>*Wandea nginya neana* | Mama ewe mama sitakusahau,<br>Mama ewe mama ni wewe mpenzi wangu,<br>Mimi hufurahi ninapokumbuka shida Ulizokumbana nazo nikiwa mdogo,<br>Ulinizaa nikiwa mdogo sana Susana,<br>Ukanilea nikawa mkubwa. |
| *Wendo wa musyai sweet mother ndwambata, mother ii mother wanzyaie,*<br>*Liu nga na kisomo wandeie nesa ,*<br>*Mother ii ngia akuathimae wi wakwa*<br>*Liu, ngua na kisomo wandeie nesa,*<br>*Mother ii ngai akuathimae wi wakwa.*<br>*Wanzyaie ni munini mother Susana,*<br>*Wandea nginya neana.* | Upendo wa mzazi mama hukuninyima,<br>Chakula, mavazi na elimu ulinilea vyema.<br>Mama Mungu akubariki wewe ni mpenzi Wangu, Mama ewe mama ulinizaa<br>Ulinizaa nikiwa mdogo sana Susana,<br>Ukanilea nikawa mkubwa. |
| *Mauau mathuku ta mukambi kana volio,*<br>*Wandwaie nzanzoni na matyaangwata,*<br>*Nou nyinya wakwa na noue mwendwa wakwa,*<br>*Mother ii ngai akuathimae wi wakwa.*<br>*Wanzyaie ni munini mother Susana,*<br>*Wandea nginya neana.* | Magonjwa hatari kama surua na kupooza,<br>Ulinipeleka kuchanjwa na sikuugua.<br>Ni wewe mama yangu, ni wewe mpenzi Wangu, mama ewe mama Mungu akubariki.<br>Ulinizaa nikiwa mdogo sana Susana,<br>Ukanilea nikawa mkubwa. |
| *Nililikana undu wandavasya yila nai kana,*<br>*Yu ninguwona na ninguwitikila,*<br>*Wambia sani nthi yusuite thina,*<br>*Iyuumisye sua umwe nukona nesa.*<br>*Wanzyaie na munini mother Susana,*<br>*Wandea nginya neana.* | Nakumbuka ulivyoniwasia nikiwa mdogo,<br>Sasa nayaona na ninayakubali.<br>Uliniambia duniani kuna shida,<br>Vumilia siku moja utafanikiwa.<br>Ulinizaa nikiwa mdogo sana Susana,<br>Ukanilea nikawa mkubwa. |
| *Nitungia ngai muvea nundu wa ukumba,*<br>*Mother ii mother ii wanzaie,*<br>*Noue inya wakwa noue mwendwa wakwa,*<br>*Mother ii ngai akuathimae wii wakwa* | Nashukuru Mungu kwa kukuumba,<br>Mama ewe mama ulinizaa,<br>Ni wewe mama yangu ni wewe mpenzi wangu,<br>mama ewe mungu akubariki ni wangu. |

| | |
|---|---|
| *Wanzyaie ni munini mother Susana wandea nginya neana.* | Ulinizaa nikiwa mdogo sana Susana, Ukanilea nikawa mkubwa. |

**KIAMBATISHO III**

**Wimbo wa Ancent Munyambu (Kavola Kamemengele)**

| **KIKAMBA** | **KISWAHILI** |
| --- | --- |
| *Kavola kavola kamemengele, kwa nau na Mwaitu nganengwa ki?*<br>*Kavola kavola kamemengele kwa nau na Mwaitu nganengwa ki?*<br>*Isu ni ng'ombe mukuthinza mukiya ngathi na Ingengeto nakwa mwinenga mavindi,*<br>*Mwinega mavindi ko ni ngiti. Kavola kavola Kamengele,*<br>*Kwa nau na mwaitu nganewa ki?* | Polepole polepole kamengele kwa baba na Mama nitarithi nini?<br>Polepole Kamengele kwa baba na mama Nitarithi nini?<br>Hao ni ng'ombe mnaochinja, mkila minofu na Mimi mkinipa mifupa,<br>Mwanipa mifupa kwani mimi ni mbwa?<br>Polepole polepole Kamengele,<br>Kwa baba na mama nitarithi nini?<br>. |
| *Kavola kavola Kamengele kwa nau na mwaitu nganewa ki?*<br>*Kavola kavola Kamengele kwa nau na mwaitu nganengwa ki?*<br>*Muthenya umwe masuiluni, kindu ta mundu Makumbini kusisya ni kelitu ko utuini,*<br>*Ngakulya kiililila kwika ata?*<br>*Kavola kavola Kamengele kwa nau na mwaitu nganengwa ki?* | Polepole polepole Kamengele kwa baba na mama nitarithi nini?<br>Polepole polepole Kamengele kwa baba na mama nitarithi nini?<br>Siku moja asubuhi na mapema kabla jua kuchomoza,<br>Niliskia kitu kama mtu ghalani, kuangalia ni Msichana wa pale kijijini,<br>Nikajiuliza anafanya nini?<br>Polepole polepole Kamengele kwa baba na Mama nitarithi nini? |
| *Kavola kavola kamengele kwa nau na mwaitu nganewa ki? Kavola kavola Kamengele kwa Nau na mwaitu nganewa ki? Weewa kungulu makumbini, ndukasye ni mbia Ikuya mbemba, ona ti ngulu kana nganga, ni Mwiitu wa mwenyu ukutua mbesa, Kavola Kavola Kamengele kwa nau na mwaitu nganewa ki?* | Polepole polepole Kamengele kwa baba na mama nitariyhi nini? Ukisikia kelele ghalani, Usiseme ni panya wanaokula mahindi, hata si Fukusi wala kanga ni dada yako anatengeneza pesa. Polepole polepole Kamengele kwa baba na mama nitarithi nini? |

**KIAMBATISHO IV**

**Nyinya wa Syana (Mama Watoto) wa Dicky Mulwa**

| **KIKAMBA** | **KISWAHILI** |
| --- | --- |
| *Nyinya wa syana niki ndwikwiwa nthoni,* | Mama watoto kwa nini huna haya, |
| *Nyinya wa syana niki ndwikwiwa nthoni,* | Mama watoto kwa nini huna haya, |
| *Uingunuia maletho ngutwaite,* | Ukinitolea ukali na ni mimi nimekuoa, |
| *Uingunuia maletho ngutwaite,* | Ukinitolea ukali na ni mimi nimekuoa, |
| *Ndukinyange mbuleki* | Punguza mwendo mwanamke, |
| *Ndukinyange mbuleki,* | Punguza mwendo mwanamke, |
| *Noituvya kamunuka* | Wacha kupayukapayuka, |
| *Noituvya kamunuka kiveti* | Wacha kupayukapayuka mwanamke. |
| | |
| *Niuma wiani ngivika uimbitya mbesa* | Nikitoka kazini wadai pesa, nikitoka kazini |
| *Niuma wiani ngivika uimbitya mbesa,* | wadai pesa, |
| *Nenga silingi mbongela kasumuni* | Nipe shilingi niongeze sumuni, |
| *Nenga silingi mbongela kasumuni,* | Nipe shilingi niongeze sumuni, |
| *Nanathelelwa kui mwiwano,* | Nikifilisika hakuna amani, |
| *Nanathelelwa kui mwiwano,* | Nikifilisika hakuna amani, |
| *Ndineena, nditwa katondomo,* | Nikiongea naitwa mpayukaji, |
| *Ndineena nditwa katotondomo, Tondoma twiwe.* | Nikiongea ninaitwa mpayukaji |
| | |
| *Niw'o nguthina ndikoma nzalukitye,* | Nakumbana na changamoto nyingi kazini, |
| *Niwo nguthina ndikoma nzalukitye,* | nakumbana na changamoto nyingi za kazini |
| *Utindiite kivilani kya sofa ,* | Nalala nje penye baridi shadidi, |
| *Utindiite kivilani kya sofa,* | Nalala nje penye baridi shadidi, |
| | |
| *Ndivika uindavya ndeto veveve,* | Nikifika nyumbani sina amani wanitolea maneno veveve, |
| *Ndivika uindavya ndeto veveve,* | Nikifika nyumbani sina amani wanitolea maneno veveve |
| *Utavitwe ni anyanyau,* | Ukiwa umeambiwa na wenzako |
| *Utavitwe ni anyanyau* | Ukiwa umeambiwa na wenzako |
| | |
| *Ninguukulya kwa tei wambe kwisilya,* | Nakusihi kwa heshima ufikirie, |
| *Ninguukulya kwa tei wambe kwisilya,* | Nakusihi kwa heshima ufikirie, |
| *Kitumi nubndu wilikywa kithekani,* | Kwa sababu utaharibu ndoa yako, |
| *Kitumi nundu wilikywa kithekani,* | Kwa sababu utaharibu ndoa yako, |
| *Na itina nukuia we kiveti,* | na baadaye utajuta, |

| | |
|---|---|
| *Na itina nukuia we kiveti* | Baadaye utajuta mwanamke, Utakosa wa kukuvisha. |
| | |
| *Ninguseng'a nundu wa kimosa kyakwa,* | Ninasikitika kwa sababu ya afya yangu, |
| *Ningusenga nundu wa kimosa kyakwa,* | Ninasikitika kwa sababu ya afya yangu |
| *Wiani na no ngosa musaala,* | Nafanya kazi na mshahara napata , |
| *Nani wiani na no ngosa musaala* | Ninafanya kazi na msahara napokea, |
| | |
| *Kai wingenda nundu wa kwithiwa wi a syana,* | Wanidharau kwa sababu ya watoto, |
| *Kai wingenda nundu wa kwithiwa wina syana,* | Wanidharau kwa sababu ya watoto, |
| *Kotesi aume me mavinduka maingi,* | Hujui kuwa wanaume wana mipango mingi, |
| *Kotesi aume me mavinduka maingi,* | Hujui kuwa wanaume wana mipango mingi , |
| *No ndwae kakua mbunguo,* | Ninaweza kuoa mke mwingine, |
| *Nondwae kakua mbunguo.* | Ninaweza kuoa mke mwingine, |
| | Ubaki ukiduwaa, ubaki ukiduwaa |

**KIAMATISHO V**

**Aka ma Taoni (Wanawake wa Mjini)**

| **KIKAMBA** | **KISWAHILI** |
|---|---|
| *Dan mwa ningusenga ni aka ma taoni,*<br>*Dan mwa ningusenga ni aka ma taoni,*<br>*Mwa mendete mbesa yutia yila ya aume*<br>*mwa mendete mbesa yutia tila ya aume* | Dan nashangazwa sana na wanawake wa mjini,<br>Dan nashangazwa sana na wanawake wa mjini,<br>Wao huthamini pesa sana jasho la wanaume,<br>Wao huthamini sana pesa jasho la wanaume |
| *Makwona na mbesa, mo maile kwosa,*<br>*Makwona na mbesa mo maile kwosa,* | Wakikuona na pesa wao huzua mbinu za kuzichukua,Wakikuona na pesa wao huza mbinu za kuzichukua, |
| *Syo siisawa muthekete na syathela mo Maisemba, Syo siisawa mutheketa na Syathela mo masemba* | Wao hukupumbaza kwa mapenzi ya uongo,<br>Wao hukupumbaza kwa mapenzi ya uongo,<br>Ukifilisika wanahepa, |
| *Mo masyaa ila ndia imbiie nikuka ingi.*<br>*Mo masyaa ila ndia imbiie nikuka ingi,*<br>*Vata wakwa ni mbesa, yavika ningumwonya,*<br>*Vata wakwa ni mbesa yavika ningumwonya.* | Wao husema yule mjinga alisema atarudi tena,<br>wao husema yule mjinga alisema atarudi tena,<br>Tambua hawajali haja yao ni pesa, tambua Hawajali haja yao ni pesa. |
| *Aume yu musoanie kuya musyi kwi thina*<br>*Aume yu musoanie kuya musyi kwi thina*<br>*Hasa hasa wa munyu, sukali na mayani,*<br>*Hasa hasa wa munyu, sukali na mayani.* | Wanaume fikirieni mahitaji ya nyumbani,<br>Wanaume fikirieni mahitaji ya nyumbani<br>Hasa hasa mahitaji ya chumvi, sukari na Majani, hasa hasa mahitaji ya chumvi, sukari na majani. |
| *Wosana na malaya, ndukalimya mbesa syaku,*<br>*Wosana na malaya ndukalumya mbesa syaku,*<br>*Na kwikya mbesa neulu ni makosa ni kiumo,*<br>*Na kwikya mbesa neulu ni makosa ni kiumo.* | Ukijihusisha na malaya hakuna kuweka akiba,<br>Ukijihusisha na Malaya, hakuna kuweka Akiba,na kufuja pesa ni makosa na ni laana,<br>Kufuja pesa ni makosa na ni laana |
| *Aka aa mukwona me taoni makuaa ndumba,*<br>*Aka aa mukwona me taoni makuaa ndumba,*<br>*Na maendaa muno kwa awe Mayosa ndumba sya wendo, na naendaa muno kwa awe mayosa ndumba sya wendo.* | Wanawake hawa wa mjini wao hubeba irizi,<br>Wanawake hawa wa mjini wao hubeba irizi,<br>Wao hutazamia kwa waganga na kupewa dawa Za mapenzi, wao hutazamia kwa waganga na hupewa dawa za mapenzi |

**KIAMBATISHO VI**

**Nyinya wa Ndetei (Mamake Ndetei)**

| **KIKAMBA** | **KISWAHILI** |
| --- | --- |
| *Nyinya wa Ndetei, nyinya wa Nthiwa , mami wa Koreta,*<br>*Nyinya wa syana ni ivityo yau yu neekie,*<br>*Nyinya wa syana ni ivityo yau yu neekie*<br>*Kuma wathi ona kavalua ndunandikia*<br>*Kuma wathi ona kavalua ndunandikia* | Mama Ndetei, mama Nthiwa, mama Koreta,<br>Mama watoto ni kosa gani nililokukosea,<br>Mama watoto ni kosa gani nililokukosea,<br>Tangu uende kwenu hata barua hunitumii,<br>Tangu huende kwenu hata barua hunitumii |
| *Nyinya wa Ndetei, nyinya wa Nthiwa , mami wa Koreta,*<br>*Kyeva kya ngoo na kimako nikyambingiviie*<br>*Kyeva kya ngoo na kimako nikyambingiviie*<br>*Kethiwa wi tei ukambona yu wamba kuia*<br>*Kethiwa wi tei ukambona yu ninamosie* | Ndetei, mama Nthiwa, mama Koreta,<br>Ninahuzunika sana mwoyoni<br>Ninahuzunika sana mwoyoni<br>Ukiniona mama unaweza kunihurumia,<br>Hali yangu si hali nimekonda |
| *Nyinya wa Ndetei, nyinya wa Nthiwa , mami wa Koreta*<br>*Wendo witu mwa kowoonekie ni amaitha,*<br>*wendo witu mwa kwowoonekie ni amaitha,*<br>*Na metho moo matunivite ta mwaki ,*<br>*Na metho moo matunivite ta mwaki.*<br>*Ni vandu voo vaati ya mwiai ma kasila,*<br>*Ni vandu voo vaati ya mwiai ma kasila.* | Mama Ndetei, mama Nthiwa,mama Koreta<br>Mapenzi yetu kwani yaliingiliwa na hasidi,<br>Mapenzi yetu kwani yaliingiliwa na hasidi,<br>Na macho yao mekundu kama moto,<br>Na macho yao mekundu kama moto<br>Shauri yao Mungu atawahukumu.<br>. |
| *Nyinya wa Ndetei, nyinya wa Nthiwa , mami wa Koreta*<br>*Nyinya wa syana wavika kwenyu ko Wanzambisye, Nyinya wa syana wavika kwenyu ko wanzambisye,*<br>*Mwa ninesie kutavywa, wimbita mukola,*<br>*Munywi wa vangi, mukuni wa ngitaa,*<br>*Na ngitaa ti ukola mwendwa wakwa nundu wa ngwatie* | Mama Ndetei, mama Nthiwa, mama Koreta,<br>Mama watoto ulipofika kwenu Kwaniulinisengenya,<br>Nilisikia kuwa ulikuwa ukisema mimi ni Mkora, mpiga gitaa, mvuta mbagi.<br>Mpenzi kucheza gitaa si ukora ni talanta |

**KIAMBATISHO VII**

**Aka nima mithemba (Aina mbalimbali za wanawake) wa Wanginga**

| **KIKAMBA** | **KISWAHILI** |
| --- | --- |
| *Natavawa ni susu ngamba kwona ta ithau,*<br>*Natavawa ni susu ngamba kwona ta ithau,*<br>*Aka nima mithemba, ve uko wa kilata na*<br>*Kwi uko wa usavi, aka ni ma mithemba mingi* | Nilikuwa nikiwosiwa na nyanya kama mzaha,<br>Kuna aina mbalimbali za wanawake,<br>Nilikuwa nawosiwa na nyanya kama ni mzaha,<br>Kuna aina mblimbali za wanawake,<br>Kuna wanawake virukanjia na wengine wa umbeya |
| *Ninye natwaie Nzembi kuma ngaluko sye Imali,*<br>*Ninye natwaie Nzambi kuma ngaluko sye Imali, twavika kwakwa angeuka, kai ni uko wa kilata*<br>*Na ni uko wa usavi, ngaemanwa nake,*<br>*Ngalungililya itheka.* | Nilioa Nzembi kutoka pande za Emali,<br>Nilioa Nzembi kutoka pande za Emali,<br>Alipofika kwangu akabadili nia,<br>Kumbe alikuwa kirukanjia na mbeya, nikampa talaka |
| *Auma vu kwakwa ngamwiwila Kajado,*<br>*Atwaitwe ni Masai, ona ku akalunjwa*<br>*Ni uko wa kilata, na ni uko wa usavi,*<br>*Aakalungililwa itheka. Aka nima mithemba mingi* | Alipotoka kwangu alihamia Kajiado,<br>Akaolewa na Maasai, hata huko akapewa<br>Talaka kwa sababu ya umbeya,<br>Kuna aina mblimbali za wanawake. |
| *Auma kajiando ngamwiwila Kikuyu,*<br>*Atwaitwe ni Mwikuyu,*<br>*Ona ku akalunjwa, ni uko wa kilata,*<br>*Ni uko wa kitimba, aka me uko ta indo* | Alipotoka Kajiado alihamia Kikuyu,<br>Alikoolewa na Mgikuyu,<br>Hata huko akapewa talaka,<br>Kwa sababu ya umbeya na uasherati,<br>Wanawake ni wa aina mbalimbali kama mifugo. |

**KIAMBATISHO VIII**

**Kana Nzula(Mpenzi Nzula) wa Bosco Mulwa**

**KIKAMBA**

*Ngililye ngomete muomo wakunangwa,*
*kukila kuvingua nau ngatana muno,*
*vaung'e nzula mwiitu wa Musomba,*
*Wi kana na nusu Nzula wimumbe nesa,*
*Yiya Nzula mwiitu wa Musomba*

*Twi makuuweni Nzula wai kindu wakwa,*
*Natindaa naku ta twi mavatha Nzula,*
*Wamina sukulu waendie Ulaya,*
*Ulaya waendie kusomea mandawa,*
*Kana Nzula wandiie na thina,*
*Ula Nzula mwiitu wa Musomba*

*Niwite nesa kunzyokea we Nzula Ngwetele*
*Nzula umine masomo mwendwa,*
*Ninai na wia ndukatwawe ni musungu,*
*Uka Nzula kana na vata naku,*
*Yiya Nzula ii mwiitu wa Musomba*

*Nivoya ngai twikale maisha maseo,*
*Ma mundu na muka nyumba na wendo Nzula,*
*Tusyae tata, Nzula na mami witu,*
*Ndukethukiisye ndeto sya atui mwendwa,*
*Ikia pamba matu ndukewe nzuku,*
*Yiya Nzula ii mwiitu wa Musomba,*
*Kana Nzula ii mwiitu wa Musomba*

**KISWAHILI**

Nilipokuwa nikilala nilisikia mbisho mlangoni,
Nilipoufungua nilifurahi sana,
Alisimama Nzula binti Musomba,
mpenzi wangu umeumbika vyema,
Kweli Nzula binti Musomba

Tukiwa Makueni Nzula ulikuwa mpenzi wangu. Tulifuatana kila mahali kama pacha,
Ulipokamilisha masomo ulienda Uingereza,
Uingereza ulienda kusomea udaktari,
Mpenzi Nzula uliniacha na upweke,
Kweli Nzula binti Musomba.

Ninafurahia kurudi kwako Nzula,
Nilikuwa nikihuzunika sana mpenzi,
Nikikusubiri ukamilishe masomo,
Nilikuwa nahofia utaolewa na mzungu,
Njoo Nzula mpenzi wangu nakupenda,
Kweli Nzula binti Musomba

Naomba Mungu atujalie maisha mema,
Ya mume na mke, tuzae watoto wetu Nzula,
Usifuate maneno ya watu mpenzi,
Tia pamba masikioni usisikie ya umbeya,
Kweli Nzula binti Musomba.

**KIAMBATISHO IX**

**Aka me vata (Wanawake ni wa kuthaminiwa) wa Justus Myello**

| **KIKAMBA** | **KISWAHILI** |
| --- | --- |
| *Yii nikalite thayu uu ngethia aka me vata na<br>Maile ukumwa nundu aka nimo matusyaie,<br>Nina muvea kwaku we mundu muka mwailu,<br>Nayu niina nielesye mauseo maku mami.* | Nimeishi maisha haya na kutambua kuwa<br>Wanawake wanastahili kupongezwa kwani<br>Wao ndio waliotuzaa, nakushukuru mwanamke<br>Unayestahili, na sasa ninaimba kueleza mazuri yako mama. |
| *Andu aa muona meiseka suka na ikoi na<br>Itambaa, Andu me vata muno thayuni wa kila<br>Mundu aka meutonyi mwingi na vinya waika maundu manene,<br>Keka maikwo nthi ino maundu makitakuema,<br>Tumakunie moko, tumakunie mbi,<br>Pongesi we mami mwaiyu wi mundu wa vata nthi ino.* | Hawa watu mnaowaona wakijifunga leso na vitambaa<br>Ni watu wa thamani kubwa katika maisha ya kila mtu,<br>Wanawake wana uwezo mkubwa na nguvu za kutenda makuu,<br>Kama wasingekuwa katika ulimwengu huu,<br>Maisha yangekuwa magumu,<br>Tuwapongeze kwa kuwashangilia. |
| *Myai keenda ukangua utesi niilye ata,<br>Kwaunya na woo mwingi kunzyaaa netina kundea,<br>Mauwau me itai ta ini, kiumati,<br>Kung'ang'athuka monthe ndesi wanzuvia,<br>Wendo waku wi mwanya.* | Miezi tisa tamima, ulinihimili pasi kujua mimi ni kiumbe cha aina gani,<br>Kuvumilia machungu ya uzazi na hatimaye kunizaa.<br>Magonjwa sugu ya utotoni ulinikinga dhidi yake,<br>Kweli mapenzi yako ni ya kiaina. |
| *Andu aa muona meiyova suka na ikoi na itambaa,<br>Nandu mevata sana thayuni wa kilamundu,<br>Aka me utonyi mwingi na vinya waika maundu manene,<br>Keka maikwo thino maundu Makita kuema,<br>Tutonya kumane ki, tumakunie moko na ngemi,<br>Pongesi we mami mwaitu wi mundu wa vata nthi ino.* | Hawa watu mnaowaona wakijifunga leso na vitambaa<br>Ni watu wa thamani kubwa katika maisha ya kila mtu,<br>Wanawake wana uwezo mkubwa na nguvu za kutenda makuu,<br>Kama wasingekuwa katika ulimwengu huu,<br>Maisha yangekuwa magumu,<br>Ttuwapongeze kwa kuwashangilia. |

*Maisye maithi nguni na mbisu yi iko,*
*Usini kiw'u no kuuta na indo nowe ukathasya,*
*Syana syatina kuiyany'a mami nowe ikwenda,*
*Kitanda nowe ukalany'a na usuvia musee*
*Aka me utonyi mwingi na vinya waika maundu manene,*
*Andu aa me vat asana thayuni wa kila mundu,*
*Maikambile kuvuthywa.*

Watazame wakienda kuchanja kuni, chungu
Jikoni na maji mtoni wao ndio huchota, mifugo
Wao ndio hushughulikia, watoto wakilia mama ndiye wanataka
Pamoja na kutunza mume wake.
Watu hawa ni wa kuthaminiwa na kuheshimiwa.

*Angi matatite maundu tuviasala,*
*Vai kindu kivinya Ukamba ta kuea syana,*
*Kuta maluu na manga na mavokando,*
*Mekiite vitii kulungy'a ukya musyi.*

Wengi wamejaribu baishara mbalimbali, kuuza viazi, mihogo na maparachichi.
Hakuna jambo ngumu katika maisha ya
Ukambani kamba kufanya biashara kama hizi.
Haya yote wanafanya kuzikimu familia zao na
Kumaliza umaskini katika familia.

*Amwaitu aya mukwona nimwia me vata,*
*Sambuli uyu mukwona nimwia wi mwoo,*
*Andu ta aya mukwona nimwia me vata mwingi,*
*Muthemba uyu mukwona nimwia ni wa vinya*
*Aa mwaitu niasya masuviwe, ndaia nene manengwe,*
*Amwaitu niasya masonokwe itui sya kwaka musyi.*

Akina mama hawa mnaowaona nasema ni wa thamani kubwa,
Aina hii nawaambia ni nadra sana kupatikana,
Hawa watu mnaowaona nasema ni wa kipekee,
Waheshimiwe na kutunzwa kwani ni nguzo za kujenga familia

*Andu aa nienda matunzwe muno, ndaia nene manengwe.*
*Ooh itui sya kwaka musyi.*
*Yuyu nooka nine nasye aka ithyi twikwo na*
*Tunengetwe utonyi ni mumbi witu, akili na*
*Kisomo tutuite nasyo, ona maovisi manene tutua kw'o.*

Ooh oo ni nguzo za kujenga familia.
Sasa nasema wanawake tupo,
Tumepewa nguvu na uwezo na Muumba wetu,
Akili tambuzi na elimu tunazo,
Hata nyadhifa za uongozi tunazo.
Tunaweheshimu wakati wote.

**KIAMBATISHO X**

**Kiveti Ngungu (Mwanamke tasa) wa Kakai Kilonzo**

| **KIKAMBA** | **KISWAHILI** |
|---|---|
| *Mwiitu mukuvi mwiu nongi muasa mweu,*<br>*Mwiitu mukuvi mwiu nongi muasa mweu*<br>*Kwasisya undavasye ula wi kavala ngamanya.*<br>*Kivetu ngungu na kingi kisyau,*<br>*Kwa sisya undavasye ula wi kavala ngamanya.* | Msichana mfupi mweusi na mwingine mweupe mrefu,<br>Hebu niambie ni yupi mzuri nielewe.<br>Mwanamke tasa na mwingine mwenye watoto,<br>Hebu niambie ni yupi mwema nifahamu |
| *Mutumia wi kiveti nongi utai,*<br>*Mutumia wi kiveti nongi utai,*<br>*Kwasisya undavasye ula wikavala ngamanya,*<br>*Kwa sisya undavasye ula wi kavala ngaweta* | Mwanamume ambaye ameoa na mwingine asiye na mke ,<br>Mwanamume ambaye ameoa na mwingine asiye na mke,<br>Hebu niambie ni yupi ni afadhali,<br>Hebu niambie ni yupi afadhali nijue. |
| *Kiveti ngungu na muoi me nduu,*<br>*Kiveti ngungu na muoi me nduu,*<br>*Na nundu nandu matendete umesye kindu,*<br>*Na nundu nandu matendete umesye kindu muoi.* | Mwanamke tasa na mchawi ni sawa,<br>Mwanamke tasa na mchawi ni sawa,<br>Kwani ni watu wasiotakia wengine mema,<br>Kwani ni watu wasiowatakia wengine mema<br>Wacha niseme ukweli |
| *Muio ndendete kwona kindu kiseo,*<br>*Muoi ndendete kwona kindu kiseo,*<br>*Onetha ni alusi we okite kwananga,*<br>*Onetha win a ngali euvoyea uvaluke muoi.* | Mchawi hapendi kuona wengine wakiendelea,<br>Mchawi hapendi kuona wengine wakiendelea,<br>Ukiwa na gari anakuombea ajali ,<br>Ukiwa na gari anakuombea ajali,<br>Hata kama ni arusi kusudi lake nikuharibu,<br>Hata kama ni arusi kusudi lake ni kuharibu. |

**KIAMBATISHO XI**

**Syoka Mami ( Rudi mama) wa John Muasa**

| **KIKAMBA** | **KISWAHILI** |
|---|---|
| *Mami niki watwathukiie, mama niki*<br>*Watwathukiie na nengi noue watusyaie,*<br>*Niki watutiie na ndati wathi uendo.* | Mama kwa nini ulitutelekeza na ni wewe uliyetuzaa,<br>Kwa nini ukatuachia baba ukaenda kwenu,<br>Kwa nini ukatuacha na baba ukaenda kwenu |
| *Lilikana uyuma kwaku, lilikana uyuma kwaku ,*<br>*Watavisye ndati yithi soko*<br>*Kumbe wai na mupango wa utoloka* | Kumbuka ulipotoka nyumbani, kumbuka<br>Ulipotoka nyumbani ulimwambia baba unaenda sokoni,<br>Kumbe ulikuwa na njama ya kutoroka. |
| *Na yuyu ni myaka mingi, na yuyu ni myaka mingi,*<br>*Twikalite twina kimako nue*<br>*Tuikulya ndandi mami kula waendie* | Umepita muda mrefu tukihuzunika kwa sababu yako,<br>Umepita muda mrefu tukihuzunika kwa ajili yako,<br>Tukiuliza baba ulikoenda. |
| *Kalungukalungu tukewa uvumi,*<br>*Kalungu kalungu tukewa uvumi,*<br>*Wioneka Kibera kisaki,*<br>*Ilovi wikalitwe ni mwikuyu wa maleve.* | Punde si punde tukasikia uvumi,<br>Punde si punde tukasikia uvumi,<br>Unaonekana Nairobi mtaa wa Kibera ukiwa na mwanamume mwingine.<br>Unaonekana Nairobi mtaa wa Kibera ukiwa na mwanamume mwingine. |
| *Mami niki utaingwa kyeva,*<br>*Mami niki utaingwa kyeva na tei*<br>*Ukithi utie musyi waku tuteseke na noue mami watustaie* | Mama kwa nini huna huruma, kwa nini mama huna huruma,<br>Kuacha watoto wako na ni wewe uliyetuzaa,<br>Kuacha watoto wako na ni wewe uliyetuzaa |
| *Kusoma kwitu kwai na muisyo,*<br>*Kusoma kwitu kwa na muisyo,*<br>*Itumi nundu mami niwaendie,*<br>*ndi kalivu syoka kwaku uthumue.* | Masomo yetu yalikumbwa na changamoto tele,<br>masomo yetu yalikumbwa na changamoto tele,<br>kwa sababu mama ulituacha,<br>Sasa karibu kwako nyumbani upumzike. |
| *Niki tukosa wendo waku na nengi mami witu wiothayu,*<br>*Syoka noitulia musyi niwaku mwaitu.* | Kwa nini mama tunakosa mapenzi yako na ungali hai,<br>Kwa nini tunakosa mapenzi yako na ungali hai. |

*Uka mami nitukumisi onaethiwa makosa.* Rudi mama tunakupenza.

## KIAMBATISHO XII

THIS IS TO CERTIFY THAT:
*MISS. DORCUS KASIVA KIMONDIU*
of MACHAKOS UNIVERSITY, 136-90100
Machakos,has been permitted to
conduct research in *Kitui* , *Machakos* ,
*Makueni* Counties

on the topic: *USAWIRI WA MWANAMKE KATIKA NYIMBO ZA SIFO ZA WAKAMBA*

for the period ending:
*15th November,2019*

Permit No : NACOSTI/P/18/84613/26812
Date Of Issue : 16th November,2018
Fee Recieved :Ksh 1000



.............................
*Applicant's Signature*

.............................
*Director General*
*National Commission for Science, Technology & Innovation*

**KIAMBATISHO XIII**

**NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE, TECHNOLOGY AND INNOVATION**

Telephone:+254-20-2213471, 2241349,3310571,2219420
Fax:+254-20-318245,318249
Email: dg@nacosti.go.ke
Website : www.nacosti.go.ke
When replying please quote

NACOSTI, Upper Kabete
Off Waiyaki Way
P.O. Box 30623-00100
NAIROBI-KENYA

Ref: No. **NACOSTI/P/18/84613/26812**

ate: **16th November, 2018**

Dorcus Kasiva Kimondiu
Machakos University
P.O. Box 136 – 90100
**MACHAKOS.**

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION**

Following your application for authority to carry out research on ***"Usawiri wa mwanamke katika nyimbo za sifo za Wakamba"*** I am pleased to inform you that you have been authorized to undertake research in **Kitui, Machakos and Makueni Counties** for the period ending **15th November, 2019.**

You are advised to report to **the County Commissioners and the County Directors of Education, Kitui, Machakos and Makueni Counties** before embarking on the research project.

Kindly note that, as an applicant who has been licensed under the Science, Technology and Innovation Act, 2013 to conduct research in Kenya, you shall deposit **a copy** of the final research report to the Commission within **one year** of completion. The soft copy of the same should be submitted through the Online Research Information System.

**GODFREY P. KALERWA MSc., MBA, MKIM**
**FOR: DIRECTOR-GENERAL/CEO**

Copy to:

The County Commissioner
Kitui County.

The County Director of Education
Kitui County.

National Commission for Science, Technology and Innovation is ISO9001 2008 Certified